

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA SABA

Kikao cha Tisa – Tarehe 19 Aprili, 2017

(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Naibu Spika (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) Alisoma Dua

NAIBU SPIKA: Tukae Waheshimiwa Wabunge. Katibu.

NDG. RAMADHAN ISSA ABDALLAH - KATIBU MEZANI:

MASWALI NA MAJIBU

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tutaanza na Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Fredy Atupele Mwakibete, Mbunge wa Busokelo, sasa aulize swalie lake.

Na. 70

Maombi ya Halmashauri ya Busekelo kuwa Wilaya

MHE. FREDY A. MWAKIBETE Aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itayakubali maombi ya wananchi wa Halmashauri ya Busokelo ya kuifanya Halmashauri hiyo iwe Wilaya?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKO NA SERIKALI ZA MITAA Alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Fredy Atupele Mwakibete, Mbunge wa Busokelo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Halmashauri ya Wilaya ya Busokelo ilianzishwa kwa Tangazo la Serikali GN Namba 286 ya tarehe 9 Septemba, 2011 ikiwa ni sehemu ya Wilaya ya Rungwe kwa lengo la kusogeza karibu huduma zilizokuwa zikitolewa na Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, mapendekezo ya kuifanya Halmashauri ya Busokelo kuwa Wilaya yaliwasilishwa katika Kikao cha Kamati ya Ushauri ya Mkoa (RCC) iliyokutana tarehe 4 Julai, 2013. Kamati illiagiza Sekretarieti ya Mkoa kupitia maombi hayo ili kujiridhisha kama Halmashauri hiyo inakidhi vigezo kuwa Wilaya kamili.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sekretarieti ya Mkoa ilifanya tathmini ya maombi ya wananchi wa Busokelo ya kuwa Wilaya kamili kwa kuzingatia vigezo mbalimbali vilivyotolewa na Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatambua nia njema na juhudni kubwa ya Mheshimiwa Mbunge, lakini kwa kuzingatia taarifa ya tathmini iliyofanywa na Sekretarieti ya Mkoa, hususan katika idadi ya watu, ukubwa wa eneo pamoja na kuwepo kwa tarafa moja pekee, imesababisha kutokidhi vigezo vya uanzishwaji wa Wilaya ya kiutawala ya Busokelo.

MHE. FREDY A. MWAKIBETE: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

Pamoja na majibu ya Serikali kwamba Halmashauri ya Busokelo haijakidhi vigezo vya kuwa Wilaya, nina maswali mawili kwa Mheshimiwa Naibu Waziri.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo vigezo anavyosema haijakidhi sijui ni vipi kwa sababu vigezo ambavyo vinazingatiwa, hasa ni idadi ya watu pamoja na jiografia ya eneo husika, kwetu kwa sababu hii tathmini ilishafanyika tangu miaka 2013 na sasa hivi ni 2017. Hauoni kwamba kuna umuhimu sasa wa kuanzisha hiyo Halmashauri ya Busokelo iwe inaitwa Wilaya ya Busokelo badala ya sasa ilivyo?

Swali la pili, kwa kuwa Mkuu wa Wilaya pamoja na *DAS* wanafanya kazi nzuri katika Wilaya ya Rungwe, kwa bahati mbaya kwa sababu ya jiografia ya Rungwe ilivyo kuna zaidi ya kata 40 na huyu Mkuu wa Wilaya hawezu kusimamia ama kufuatilia zote kwa wakati mmoja kufuatana na jiografia ilivyo.

Je, hauoni pia ni mionganoni mwa sababu ambayo inaweza ikasababisha ianzishwe Wilaya ya Busokelo na hivyo iweze kuanzishwa haraka iwezekanavyo?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, hayo majibu na mimi nayasikiliza kwa makini hapa. (*Kicheko*)

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwa sababu *specification* inataka angalau eneo hilo liwe na eneo lisilopungua kilometra za mraba 5,000 nwakati pale kiuhalisia ziko kilometra za mraba 969. Kwa hiyo, hii ilikuwa ni kigezo kimojawapo ambacho kimesababisha isiweze ku-*qualify*. Kipindi kile idadi ya watu kwa muongozo inatakiwa watu wasiopungua 250,000 lakini katika kipindi kile tathmini ilivyofanyika kulikuwa na watu takribani 96,348.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninafahamu muda mrefu sasa hivi umeshapita kutoka kipindi kile mpaka sasa hivi hii tathmini ukiangalia huenda *population* imeongezeka, lakini vilevile hata ukiangalia suala zima la tarafa, vigezo lazima angalao kuwe na tarafa tatu pale ukiangalia ni tarafa moja. Ninafahamu kwamba mlikuwa na juhudhi ya kuitenga ile Tarafa moja mpate tarafa nyingine tatu, hii nilidhani kwa sababu Mbunge mnafahamu kama ulivyosema mna kata

zipatazo 40, mnaweza mkakaa kwa pamoja sasa na RCC yenu kuangalia mnaweza kuishauri vizuri nini cha kufanya. Baadae ikionekana vigezo hivi sasa vimekaa vizuri basi Serikali itaona nini cha kufanya na jinsi gani ya kupata eneo hili kuwa eneo la kiutawala la Kiwilaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala kwamba Mkuu wa Wilaya ya Busokelo anahudumia eneo kubwa sana, kwa hiyo kuna haja ya kuona hili jambo sasa ikiwezekana Wilaya ile sasa Busokelo iwe Wilaya kamili. Kama nilivyosema pale awali ni kwamba hivi sasa ninyi angalieni jinsi ya kufanya. Nafahamu kwamba ni kweli Mkuu wa Wilaya ya Rungwe anafanya kazi kubwa sana, nilikuwa nae pale *site* siku ile tulipopata lile tatizo, kweli ni miongoni mwa Wakuu wa Wilaya ambao wanajituma sana katika kazi yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa vile wote kama Viongozi Wakubwa na Mheshimiwa Naibu Spika uko hapa, nadhani mtaliangalia kwa uzito wenu kwa jinsi gani mtafanya, kama Busokelo, kama Rungwe kwa wakati mmoja ni jinsi gani hata mtafanya mipaka yenu na kila kitu. Lengo kubwa ni kupeleka huduma kwa wananchi na Serikali mkiona kwamba mmekidhi vigezo hivyo, haitasita kufanya maamuzi sahihi.

MHE. YAHAYA O. MASSARE: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii na mimi niulize swali dogo la nyongeza.

Matatizo yaliyopo huko Busokelo yapo pia katika Halmashauri ya Wilaya ya Itigi. Katika Wilaya ya Manyoni kuna Halmashauri ya Manyoni na Hamashauri ya Itigi; Halmashauri ya Itigi *square kilometer* zinakidhi na maombi yamekuwa yakipelekwa kila mara na toka mwaka 1980 Serikali imekuwa ikiwaahidi wananchi wa Itigi kwamba watapatiwa Wilaya kamili.

Je, sasa ni lini Serikali itaipa Halmashauri ya Itigi kuwa Wilaya kamili?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli ukiangalia Manyoni, lazima tufahamu juhudikubwa ya Serikali iliyofanya pale, mwanzo ile yote ilikuwa inaitwa Wilaya na Halmashauri ya Manyoni. Hapa katikati ndiyo tukapata Halmashauri mpya ya Itigi na wewe Mheshimiwa Mbunge unafahamu hata suala zima la upelekaji wa fedha ndiyo kwanza tumepeleka kwa ajili ya kujenga miundombinu ya Halmashauri ile.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo hili ninafahamu kwamba, siku ile nilikuwa na Mkuu wa Wilaya pale na alisikitika katika hilo alisema kwamba mafuta anayoyatumia ni kwamba, akiamua kuzunguka eneo lake matufa yanaisha kwa sababu Manyoni ukijumlisha na Itigi ni eneo kubwa sana.

Naomba niseme japokuwa maombi hayo inawezekana mwanzo yalikuja yalidondoka kwa sababu yалиshindwa kupata sifa, hizo sifa sasa hivi zikikamilika basi naomba mfanye ile michakato ya kisheria kama inavyokusudiwa kuanzia katika ngazi za *Ward DC*, Baraza la Madiwani, *DCC*, *RCC*na ikifika katika Ofisi ya Rais – TAMISEMI na Waziri wangu yuko hapa, hawezo kushindwa kufanya maamuzi sahihi kwa kadri anavyoona jambo hilo linafaa kwa maslahi mapana ya wananchi wa Itigi.

MHE. KANGI A. N. LUGOLA: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kuniona.

Mheshimiwa Naibu Spika, Halmashauri ya Wilaya ya Bunda yenyeye majimbo ya Mwibara na Bunda ni majimbo mawili ambayo hayapakanii. Jimbo la Bunda liko kwingine na Jimbo la Mwibara liko kwingine, lakini ndiyo yanaunda Halmashauri ya Wilaya ya Bunda.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa jambo hili tulishampelekea Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI, na kwa kuwa Mwibara iliyahi kuwa Jimbo tangu mwaka 1974, lakini tulishapeleka TAMISEMI iwe Wilaya mpaka leo vigezo ilishatimiza lakini hatupatiwi.

Je, Mheshimiwa Naibu Waziri anawaambia nini wana-Mwibara juu ya jambo hili ambalo ni changamoto ya miaka mingi?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Naibu Spika, wasiofahamu hili Jimbo la Mheshimiwa Kangi Lugola ni sawasawa kama unazungumza kama lile bakuli halafu katikati kuna kile kisahani. Katikati ya kisahani pale unapata Jimbo la Dada yangu Mheshimiwa Ester Bulaya, Jimbo la Bunda Mjini. Ukienda huku utakuta Jimbo la ndugu yangu Mheshimiwa Boniphace Getere na huku unakuta Jimbo la Mwibara, kwa hiyo anachozungumza ni kweli.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niwaambie Waheshimiwa Wabunge, wakati mwingine tunapoenda kufanya maamuzi ya mgawanyo wa haya maeneo wakati mwingine hatuweki mipaka sahihi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, pale hata ukiangalia ni kama yai, katikati kiini cha yai ndiyo Jimbo la Mheshimiwa Ester Bulaya hata ninaamini inawezekana ukatokea ugomvi mkubwa wa wapi Halmashauri ya Jimbo hilo itajengwa inawezekana ni kutokana na huko mwanzo maamuzi yetu hayakuwa sahihi. Inawezekana ilikuwa ni mihemko ya kisiasa ya kugawanya, jinsi gani tugawanye, hatukufanya maamuzi sahihi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niseme kwamba hili kweli ni changamoto kubwa. Kama Mheshimiwa Kangi Lugola nafahamu kweli changamoto yako ni kubwa na nimefika mpaka kule ziwani siku ile nilivyofika, nimechanginyikiwa kweli Jimbo lako lilivyo. Basi mtajadiliana kwa pamoja kule katika vikao vyenu kuangalia nini cha kufanya. Jukumu letu kubwa Serikali ni kuona jinsi gani tutafanya ili wananchi waweze kupata huduma. Hivi sasa ninaamini wewe na Mbunge mwenzako ni lazima mkae vizuri la sivo inawezekana mkapishana wapi Makao Makuu yenu itaenda kujengwa kwa maslahi mapana ya maeneo yenu. Ahsante sana.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Ryoba Chacha swali fupi tafadhali.

MHE. MARWA R. CHACHA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

Vilevile katika Wilaya ya Serengeti ni moja ya Wilaya kongwe ambayo kimsingi ni Wilaya ambayo iliizaa Bunda; na ni Wilaya ambayo ina changamoto kubwa sana kijigrafia, ni Wilaya ambayo ni kubwa kwa eneo, pia, ni Wilaya ambayo ina kata nyingi kweli.

Je, ni lini Wilaya hii itagawanywa kuwa Wilaya mbili?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Spika, naomba tuweke kumbukumbu sawa, hapa ukiwa unajibu maswali haya lazima kidogo akili yako ikae vizuri. Kwa sababu Wabunge wengine wanasema maeneo yasigawanywe, wengine wanasema maeneo yagawanywe.

Mheshimiwa Mbunge, nadhani unakumbuka siku ile tuliendo wote mpaka usiku tumetoka kule tukiwa Serengeti kwako. Ni kweli Kata zako zimekuwa *scattered* sana, ndiyo maana nalifananisha Jimbo lako na lile Jimbo la Ngorongoro, ukiingalia jiografia yake ni jiografia yenyе changamoto kubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, tutaangalia jinsi gani tutafanya kwa sababu Serikali hii hatuwezi kugawanya kila maeneo tu, ni lazima kuangalia jinsi gani kuweza kuyahudumia yale maeneo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pale kwenye haja na michakato halali na vikao vyetu huko ambako mamlaka tulizopita mamlaka za Wilaya na mamlaka za Mikoa, zikifanya maamuzi hayo basi jambo hilo litakuja katika Ofisi ya Rais TAMISEMI na Waziri wangu ataliangalia, atalipima, pale atakapoona linakidhi basi atafanya maamuzi sahihi, kutokana na uhalisia wa eneo hilo.

Na. 71

Kupeleka Maji Vijiji vya Jimbo la Chilonwa

MHE. JOEL M. MAKANYAGA Aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuwapatia maji wananchi wa vijiji vya Jimbo la Chilonwa?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA Alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Joel Mwaka Makanyaga, Mbunge wa Chilonwa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kuititia Mpango wa Maendeleo ya Sekta ya Maji nchini, kuanzia mwaka 2012/2013 hadi mwaka 2014/2015 imetekeleza miradi ya maji kwa vijiji vya Itiso na Membe kwa jumla ya shilingi milioni 758.7 vikiwa na jumla ya vituo vya kuchotea maji 23 ambavyo vinahudumia wakazi wapatao 7,475.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha 2016/2017 Halmashauri inakamilisha mradi wa maji katika kijiji cha Wilunze ambao utahudumia jumla ya watu 2,867 kwa maeneo ya Makaravati, Mbelezungu, Majengo na Chalinze Nyama kwa jumla ya shilingi milioni 347.9 katika Jimbo la Chilonwa.

Aidha, katika mwaka wa fedha 2017/2018 Halmashauri imepanga kutumia shilingi bilioni 1.053 kwa ajili ya kujenga miradi ya maji ikiwa ni pamoja na vijiji vya Magungu na Segala katika Jimbo la Chilonwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali itaendelea kuboresha huduma ya maji katika Jimbo la Chilonwa na maeneo mengine nchini kwa kadri rasilimali fedha itakavyopatikana.

MHE. JOEL M. MAKANYAGA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

Nashukuru kwa majibu mazuri ya Naibu Waziri, lakini niweke wazi tu kwamba vijiji vilivyofaidika mpaka sasa ni vijiji vitatu ambavyo ukilinganisha na jumla ya vijiji 47 vya Jimbo langu ni sawa na asilimia 6.4. Kuna vijiji kama 12 hivi vilikuwa na huduma hii ya maji kabla, vinakuwa vijiji 15 vinavyofaidika ambavyo ni sawa sawa na asilimia 31.9.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu Tanzania tunakimbilia kwenye Tanzania ya Viwanda. Tanzania inayotaka wananchi wafanye kazi kwa bidii, kwa nguvu bila maji, tukijua kwamba, maji ni muhimu katika maisha ya binadamu, tusipopata maji safi na salama uwezekano wa kuwa na magonjwa ya hapa na pale yatakayotufanya tushindwe kufanya kazi inayostahili na kwa hiyo, tushindwe kuipeleka Tanzania katika Tanzania ya Viwanda.

Je, Serikali ina mpango gani kuongeza kasi ya upatikanaji wa maji safi na salama kwa wananchi wa Jimbo la Chilonwa?

Swali la pili, je, Serikali haioni kwamba kuna umuhimu sasa siyo lazima kila kijiji kichimbiwe kisima chake au kiwe na chanzo chake, wakati mwingine chanzo kimoja kiweze kuhudumia hata vijiji viwili/vitatu. Serikali haloni kwamba kuna umuhimu wa kufanya hivyo? Ahsante.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Naibu Spika, nafahamu *concern* ya Mheshimiwa Mbunge ndiyo maana tukiangalia eneo la Wilaya ya Chamwino liko karibu katika Makao Makuu sasa ya nchi yetu. Mheshimiwa Mbunge ndiyo maana unafahamu takribani zipatato wiki Nne nilikuwa katika mradi wa maji wa Wihunze ambao nimeona kwamba Mkandarasi anafanya kazi kwa kusucasua na kutoa maagizo ikifika tarehe Tatu mwezi huu tulioanza nao mradi huo uweze kukamilika na ninasikia hali kidogo inaenda vizuri. Hiyo yote ni juhudzi ya Serikali kuangalia jinsi gani tutafanya miradi hiyo ipatikane.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hali hiyo, ndiyo maana hapa nimezungumza katika majibu yangu ya awali kwamba, mwaka huu tumetenga shilingi bilioni 1.058 kwa ajili ya kupeleka juhudii hii ya maji, hata hivyo naomba nikuhakikishie kwa sababu, eneo la Wilaya ya Chamwino hasa Jimbo lako ni eneo la kimkakati na lkulu yetu ya Mheshimiwa Rais ndiyo inapojengwa pale. Naomba nikuhakikishie kwamba Serikali itafanya kila liwezekanalo kuhakikisha wananchi wa maeneo yale wanapata huduma ya maji kwa sababu, ndiyo sehemu ambayo ni pumulio la katikati la Jiji la Dodoma, lazima tuweke juhudii za kutosha. Naomba ondoa hofu, Serikali itakuwa na wewe daima kuhakikisha kwamba mambo yanakuwa vizuri katika Jimbo lako.

MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipatia nafasi.

Wananchi wa Tarafa ya Mikese, Wilayani Morogoro Vijijini, wameahidiwa muda mrefu mradi wa maji, lakini mpaka sasa wanapata taabu sana kwa kupata maji.

Je, ni lini wananchi wa Mikese watapata maji kusudi waondokane na tatizo hilo?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niweke kumbukumbu sawa. Mheshimiwa Mama Ishengoma alikuwa mionganii mwa Wajumbe wa Kamati ya Maji katika Bunge la Kumi na mimi tulikuwa katika Kamati moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, bahati nzuri wakati ule Profesa Mark Mwandsosya akiwa Waziri wetu wa Maji wa kwanza alikuwa akizungumzia sana suala zima la Mikese. Nadhani hapa tutakapo-table katika Bajeti ya Wizara ya Maji itakapofika, watazungumza jinsi gani Mfuko wa Maji ambaao mwaka huu tunatenga fedha kidogo za kutosha utagusa katika vijiji mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba tusubiri Wizara ya Maji itakapokuja kuweka bajeti yake pale, tutajadili kwa

upana zaidi jinsi gani tutawasaidia wananchi wa Mikeses ambao najua kwamba kweli wana shida kubwa ya maji, lazima wapate mradi wa maji na ahadi ya siku nyingi.

MHE. DAVID E. SILINDE: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana.

Kwa kuwa tatizo la maji limekuwa ni kero ya nchi nzima, ni kwa nini sasa Serikali, hususan kuitia kwenye bajeti ya Bunge hili, isikubali kutengeneza Wakala wa Maji Vijijini ambaye atasaidia kupeleka maji vijijini kote kama ambavyo tumefanya katika REA ambapo kwenye suala la umeme wameweza kufanikiwa vizuri. Kwa nini wasifanye hivyo ili maji yafike hata kule Momba, Chitete, pamoja na vijiji vingine? Ahsante.

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, Bunge lako Tukufu katika bajeti iliyopita liliagiza Wizara ya Maji ianzé taratibu za kuunda Wakala wa Maji nchini, tayari tumeshaanza kazi hiyo na wakati wowote itawasilishwa hapa kwa ajili ya kupewa mjadala na kupitishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo suala hilo taylori linafanyiwa kazi. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge tunaendelea, Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Mheshimiwa Savelina Silvanus Mwijage, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swalii lake.

MHE. SAVELINA S. MWIJAGE: Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru sana.

Kabla sijaauliza swalii langu napenda kuwapa wananchi wangu wa Bukoba Mjini waliopata mafuriko makubwa sana na kuwaathiri. Ninawapa pole waendelee kuwa wavumilivu, wasishtuke kwa ajili ya jambo la kusema mwafa.

Na. 72

Kuzifanya ukarabati Nyumba za NHC

MHE. SAVELINA S. MWIJAGE Aliuliza:-

Nyumba za Shirika la Nyumba la Taifa (*NHC*) ni za muda mrefu na zimekuwa chakavu sana na nyingine zimeanza kubomoka.

(a) Je, ni lini Serikali itafanya operesheni kubaini uharibifu ulioko kwenye nyumba hizo?

(b) Je, ni lini Serikali itatenga bajeti kwa ajili ya kukarabati au kujenga upya nyumba hizo?

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, mnakumbushwa mfuate utaratibu wa Kikanuni tafadhalii, tusiwe kila saa inabidi tuongeleshane kuhusu haya. Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi majibu.

NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI Alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Savelina Silvanus Mwijage, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifutavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kuna nyumba za Shirika la Nyumba la Taifa (*NHC*) ambazo ni za muda mrefu na kati ya hizo zipo zilizo katika hali chakavu ambazo idadi yake si kubwa sana ukilinganisha na nyumba zilizo katika hali nzuri kimatengenezo. Ili kuhakikisha nyumba zote zinakuwa katika hali nzuri na bora kimatengenezo, Shirika limeweka mpango mkakati wa kuhakikisha kwamba nyumba zote zilizo katika hali ya uchakavu zinafanyiwa ukarabati mkubwa na kwa nyumba ambazo kiwango cha ukachakavu ni kikubwa sana (*beyond repair*) shirika limeweka utaratibu wa kuzivunja

na kuendeleza upya viwanja hivyo kwa kujenga majengo ya kisasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Shirika la Nyumba la Taifa limefanya uhakiki wa nyumba zake zote na kubaini hali halisi ya kila nyumba na kuweka mpango wa kuzifanyia ukarabati nyumba hizo kwa awamu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2016/2017 shirika lilitenga takriban shilingi bilioni 11, kwa ajili ya kuzifanyia ukarabati nyumba zake ambapo hadi Machi, 2017 jumla ya nyumba 2,451 zilikuwa zimekwishafanyiwa ukarabati mkubwa kupitia bajeti hiyo. Aidha, idadi ya nyumba zilizofanyiwa ukarabati mkubwa inatarajiwa kuongezeka ifikapo mwisho wa mwezi Juni, 2017.

Mheshimiwa Naibu Spika, shirika linatarajia kumaliza kuzifanyia ukarabati nyumba zote katika Mwaka wa Fedha 2017/2018. Hata hivyo, ni vema ikafahamika kuwa matengenezo ya nyumba ni kazi endelevu kwa shirika, hivyo bajeti ya matengenezo itaendelea kutengwa kila mwaka ili wapangaji wa nyumba za shirika waendelee kuishi katika nyumba na mazingira bora.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Savelina Mwijage, swali la nyongeza.

MHE. SAVELINA S. MWIJAGE: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Napenda kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Kwa kuwa nyumba nyingi zimefanyiwa ukarabati kama alivyosema Naibu Waziri, Bukoba Mjini kuna majumba ya *NHC* yaliyochakaa yanaonesha Mji kuchafuka kwa ajili ya nyumba hizo za *NHC*.

Je, ni lini Serikali itafanyia ukarabati au kujenga majengo mapya ya *NHC*?

Swali la pili, kuna majengo ambayo yamechakaa yako kwenye mtaa wa Miembeni watu wameishi muda mrefu

hayana miundombinu hayana sehemu za kuingilia watu wenyewe waliopanga mle ndio wanajiwekea miundombinu na Serikali inakusanya ushuru na inakusanya kodi za majengo.

Je, ni lini Serikali itajenga nyumba mpya au kuwaruhusu wale waliomo ndani kuzinunua?

NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI: Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Mwijage amezungumzia suala la ukarabati wa nyumba za Bukoba zilizo chakavu. Kama nilivyojibu katika jibu langu la msingi nimesema suala la ukarabati ni suala endelevu na pale ambapo nyumba zinaonekana zimechakaa haziwezi tena kufanyiwa ukarabati, shirika linabomoa nyumba zile na kujenga majengo mengine mapya.

Kwa hiyo, niseme kwamba kama nyumba za Bukoba anavyosema kwamba zimechakaa, zinahitaji ukarabati nadhani bado tutaangalia kwa sababu Meneja yupo pale anaziona na anajua na ndiyo maana nimesema ukarabati huu unaendelea nchi nzima, kwa hiyo na Bukoba pia ni moja ya eneo ambalo litaangaliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, swalii la pili eneo la Miembeni nyumba zilizoko ni chakavu na hazina miundombinu. Kama nilivyojema jibu la msingi kama ni chakavu na haziwezi kufanyiwa ukarabati nadhani jukumu lililopo ni kubomoa na kujenga nyumba nyingine mpya na watu wakakaa katika mazingira yaliyo mazuri. Hatakubali kuendelea kuwa na nyumba ambazo ni chakavu na hazina uwezekano wa kufanyiwa *repear*. Kwa hiyo, ni jukumu la Shirika la Nyumba tutawatuma waende waangalie hizo ambazo hazina miundombinu na haziwezi kukarabatika tena tuone utaratibu wa kuweza kuzijenga upya katika hali hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, umilikishaji kwa wananchi ni kwamba sasa hivi kuna ule utaratibu wa mpangaji mnunuzi, kwa hiyo, kuna maeneo ambayo kuna hizo nyumba ambazo zinajengwa bado mpangaji anaweza kuwa mnunuzi kwa hiyo mtu atamilikishwa nyumba pale

atakapokuwa amelipia nyumba yake na amefikia mwisho wa gharama ya nyumba husika. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Innocent Lugha Bashungwa, swali la nyongeza.

MHE. INNOCENT L. BASHUNGWA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, utaratibu wa Serikali wa kuhamisha nyumba zilizokuwa chini ya Halmashauri kwenda Serikali Kuu umeacha watumishi katika Halmashauri ya Karagwe bila makazi, takribani kaya za Watumishi 60 hivi sasa hazina makazi kwa sababu Serikali Kuu imechukua nyumba ambazo zilikuwa chini ya Halmashauri ya Wilaya ya Karagwe.

Je, Wizara haioni kwamba inabidi iwasaidie watumishi hawa kwa kuiomba *NHC* ishirikiane na Halmashauri, Halmashauri tunaweza tukawapa eneo la kujenga nyumba nafuu kwa ajili ya watumishi hawa? Nashukuru

NAIBU SPIKA: Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, majibu.

WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI: Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba nyumba zilizokuwa awali za Wizara ya TAMISEMI baadae zikaenda *NHC* sasa zimerudishwa Serikali Kuu. Hivi sasa wataalam wangu na Wataalam wa Wizara ya Ujenzi wanapima maeneo hayo ili yamilikishwe kwa Serikali Kuu.

Lengo la Serikali ni kujenga nyumba mpya ili ziweze kuboresha mandhari ya Miji, kwa sababu nyumba hizi tangu zimemilikiwa na Serikali za Mitaa na *NHC* ingawa maeneo yale ni mijini lakini nyumba zimekuwa chakavu na hivyo zinaleta mandhari mbaya katika miji. Hivyo, lengo la Serikali ni kuzijenga upya.

Pili, kuchukua zile nyumba kuziweka Serikali Kuu hakumaanishi kwamba wale wanaokaa katika nyumba zile sasa wafukuzwe. Mheshimiwa Rais ameagiza kwamba zoezi hili linakoendelea kupima mpaka itakapofikia zamu ya kujenga nyumba mpya katika maeneo hayo, waliomo wanaopanga sasa wabaki katika nyumba hizo wasibughudhiwe na wasifukuzwe. *Whether* ni watumishi wa leo au watumishi wa zamani wenye mikataba ya kukaa kwenye nyumba hizo wabaki wale wale.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, wale wa Karagwe hao hawapaswi kutoka, wakae humo humo *whether* ni watumishi au wananchi wa kawaida. Nyumba hizi ingawa si lazima wakae watumishi tu lakini kuna sehemu nyingine watumishi wa Serikali wanakaa na wananchi wa kawaida. Kwa hiyo, waliomo kwenye nyumba hizo wasifukuzwe. Huko Karagwe kama wanansikia wanafikiri kwamba hao wafanyakazi wanatakiwa kufukuzwa hapana. Tunahaulisha tu utaratibu wa umiliki wa Serikali lakini hatuwaondoi wapangaji.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Abdallah Mtolea, swali la nyongeza.

MHE. ABDALLAH A. MTOLEA: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kuniona na mimi niulize swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa lengo la kuboresha nyumba hizi za *National Housing* ni kuwaondolea bugudha wapangaji wanaoishi katika nyumba hizo; sasa pale kwenye nyumba zilizoko Keko Juu, Kata ya Keko njia panda ya kwenda Uwanja wa Taifa wapangaji katika nyumba nne kati ya nyumba Nane zilizokuwa pale waliwahi kupewa *notice* ya kutaka kuhama bila sababu za msingi na wapangaji wakaamua kwenda mahakamani. Mpaka tunapozungumza sasa kesi hiyo ipo mahakamani. Mahakama imesema kwamba wakati kesi bado inaendelea pande zile mbili kati ya *National Housing* na wapangaji sizibughudhiane, lakini mara kwa mara...

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Mtolea uliza swali muda wetu hautoshi.

MHE. ABDALLAH A. MTOLEA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakuja kwenye swali. Kinachoendela sasa kila baada ya muda mfupi *National Housing* wanawatuma madalali kupeleka *notice* kwa wapangaji wale. Kwa kuwa, kesi ipo Mahakamani na kuwapelekea *notice* ni kuwabughudhi wapangaji wale na kuingilia Mahakama, Mheshimiwa Waziri anaweza kutoa kauli hapa leo ya kuwaambia *National Housing* waache kuwabughudhi wapangaji wale mpaka kesi itakapoisha? (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Wazari Angelina Mabula, majibu.

NAIBU WAZIRI WA ARDHI NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwamba Wizara kama Wizara haiwezi kutoa kauli hapa kwa maamuzi ambayo yako nje ya muhimili wa Bunge. Maamuzi ya Mahakama yatabaki kama yalivyo na kwa maana hiyo yale yaliyoagizwa na Mahakama ndiyo yatakayoendelea kuheshimiwa mpaka hapo uamuzi sahihi utakapokuwa umetoka.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Mashimba Ndaki, swali la nyongeza.

MHE. MASHIMBA M. NDAKI: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Kwa kuwa Halmashauri ya Wilaya ya Maswa imeshatenga eneo ambalo Shirika la Nyumba la Taifa wanatakiwa kujenga nyumba, sasa ni miaka miwili.

Je, Shirika la Nyumba bado lina mpango wa kujenga nyumba kwenye Mji wa Maswa au mpango huu umesitishwa?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Mandeleo ya Makazi, majibu.

NAIBU WAZIRI WA ARDHI NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI: Mheshimiwa Naibu Spika, *National Housing* bado

inayo dhamira ya dhati ya kujenga nyumba katika maeneo yetu kwa nchi mzima na hasa pale Halmashauri zenyewe zinapokuwa ziko tayari zimetenga maeneo kwa ajili ya kazi hiyo. Kwa eneo na Maswa bahati nzuri nilifika na nafahamu eneo lilipo bado dhamira ya Shirika iko pale pale.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo kubwa ambalo linatakiwa kufanyika kwa sababu mara nyangi pia tumekuwa tukilalamika kuwa bei ya nyumba kuwa kubwa, sasa Halmashauri ambazo zina maeneo kama Maswa wanatakiwa kuwa wamefanya maandalizi ya miundombini katika maeneo yao, ikiwepo suala la barabara, suala la maji na suala la umeme ili watakapo kuja kujenga zile nyumba basi ziwe na gharama nafuu kama ambavyo inatarajiwa kuwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo napenda kumhakikisha Mheshimiwa Mbunge kwamba dhamira ya shirika bado ipo pale pale kujenga nyumba kwa kihakikisha Watanzania wanakuwa na makazi bora.(*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa tunaendelea. Wizara ya Fedha na Mipango, Mheshimiwa Catherine Valentine Magige, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swalı lake.

Na. 73

Kuhusu Mafao ya Waliokuwa Wafanyakazi wa Hoteli ya Seventy Seven Arusha

MHE. CATHERINE V. MAGIGE Aliuliza:-

Waliokuwa wafanyakazi wa Hoteli ya *Seventy Seven* ya Arusha hawajalipwa mafao yao hadi sasa:-

Je ni lini watalipwa mafao yao?

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO Alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa

Fedha na Mipango, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Catherine Valentine Magige, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, waliokuwa wafanyakazi wa Hoteli ya *Seventy Seven* - Arusha wapato 238 waliachishwa kazi mwaka 2000 na kulipwa mafao yao kwa mujibu wa taratibu na sheria. Katika zoezi la ulipaji wa mafao ya wafanyakazi hao, Serikali kupitia iliyokuwa *PSRC* ilitoa na kulipa kiasi cha shilingi 217,366,296 mwezi Januari, 2000 kama mafao ya wafanyakazi hao. Baada ya malipo hayo watumishi hao waliwasilisha malalamiko kuwa wamepunjwa. *PSRC* ilihakiki madai hayo na baada ya kujiridhisha mwezi Agosti, 2000 Serikali ilitoa idhini ya kulipa tena kiasi cha shilingili 273,816,703 kugharamia mapunjo ya mishahara na mafao ya wafanyakazi hao.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo basi, wafanyakazi hao tayari walishalipwa mafao yao kwa mujibu wa sheria na taratibu na hawastahili kudai malipo yoyote ya nyongeza.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Catherine Magige, swalii la nyongeza.

MHE. CATHERINE V. MAGIGE: Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu yasiyordhisha ya Mheshimiwa Naibu Waziri nina maswali mawili ya nyongeza.

Kwa kuwa katika jibu la msingi Mheshimiwa Naibu Waziri amesema wafanyakazi hao wa *Seventy Seven* walilipwa, siyo kweli walilipwa awamu ya kwanza, awamu ya pili haikuwafikia wafanyakazi hawa na baada ya malalamiko Wizara ilituma wakaguzi mwaka 2003 wakakagua wakajua kuna tatizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa watu hao wamekuwa wakihangaika muda mrefu kutafuta haki zao waliandika barua Ofisi ya Rais, tarehe 17 Machi, 2016 walijibowi barua kutoka Ofisi ya Rais ikienda kwa Waziri wa Maliasili kuwa ashughulikie tatizo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, siyo hivyo tu, vilevile walilalamika Ofisi ya Waziri Mkuu na kuna barua ilikuja ya tarehe 4 Novemba, 2016 kuwa tatizo hili lishughulikiwe.

Je, Serikali haioni kwamba wanyonge hawa wanapoteza muda mwangi wakitafuta haki yao huku yenye we ikidai imewalipa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Waziri wa Maliasili alishapewa agizo kutoka Ofisi ya Rais ashughuliki, ni kwa nini wanasuasua wananchi wakiendelea kupata taabu? (*Makof*)

NAIBU SPIKA: Hili swali naona lina sehemu mbili za kujibiwa. Moja ni ya Maliasili, nydingine ni ya Fedha. Fedha inavyoonekana ninyi mnasema wamelipwa lakini hawajafikiwa. Sasa nani kati yenu anajibu hilo swali, maana naona wote mmekaa. Sasa sielewi nimuite nani hapa. Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii. (*Kicheko*)

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa ni swali la nyongeza ambalo limejitokeza na hoja ambayo nimeisikia kwa mara ya kwanza hapa, basi nimwombe tu Mheshimiwa Mbunge anipe fursa katika kipindi cha mapumziko leo hii nilifanyie kazi halafu nimpe majibu ambayo yatakuwa ni ya uhakika zaidi. (*Makof*)

NAIBU SPIKA: Sawa. Mheshimiwa Kakunda swali la nyongeza.

MHE. JOSEPH G. KAKUNDA: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana.

Hapo kwenye hilo swali, napenda kuiuliza Serikali wapo wastaafu kule kwangu wengi zaidi ya 20 ambaao wananiufata ofisini, ni wazee, wengine wameshafariki hawajalipwa waliokuwa watumishi wa Afrika Mashariki, waliokuwa watumishi kama *Game Officers*.

Sasa kwa nini Serikali isiwe *proactive* kuwafuatilia hao

wazee huko waliko ili waweze kulipwa mafao yao, badala ya kutusumbua Wabunge ambao tumeingia hivi karibuni? (*Makof*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha na Mipango majibu.

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Naibu Spika, kama ambavyo Watanzania wote ni mashahidi, Wizara ya Fedha na Mipango ina zaidi ya miezi mitatu sasa ikizunguka mikoa mbalimbali kufanya tathmini na kuhakiki wastaifu wote. Kwa hiyo, hilo alilolisema Mheshimiwa Kakunda, Wizara ya Fedha ilishafika Tabora na tayari imeshafika Sikonge. Kama wapo ambao hawakufikiwa tuna utaratibu zoezi hili ni endelevu waweze kufika na kuhakikiwa na haki yao watapata bila tatizo. (*Makof*)

MHE. SUSAN A. J. LYIMO: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwa na majibu ya Serikali hususan Wizara ya Fedha kwamba wastaifu wote wa iliyokuwa Jumuiya ya Afrika Mashariki walishalipwa mafao yao. Hapa nina *checkya* mzee mmoja ambaye anaitwa Mzee Malembeka na Mheshimiwa Naibu Waziri unamfahamu, katika madai yake alikuwa anadai shilingi milioni 15 Serikali imemlipa shilingi milioni tano tu. Sasa na hapa ni wazee wengi sana, naomba kauli ya Serikali.

Je, ni kweli kwamba wazee wastaifu wote wa Afrika Mashariki wamelipwa fedha zao na kwamba hawaidai Serikali? Atoe tu tamko ili tujue hili jambo limekwisha au bado wazee hawa wanaidai Serikali. (*Makof*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri Fedha Mipango majibu.

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Naibu Spika, Bunge lako Tukufu linajua ilishatolewa kauli ya Serikali ndani ya Bunge hili kuhusu malipo ya wastaifu wa

Afrika Mashariki kwamba wastaafu wote walishalipwa. Kama nilivyosema hiyo ndiyo kauli ya Serikali iliyotolewa ndani ya Bunge hili, tulishafungua milango mtu ambaye anaona hajalipwa ana udhibitisho Wizara ipo tayari kumpokea na tuweze kuhakiki na kumlipa malipo yake.

NAIBU SPIKA: Ahsante. Waheshimiwa Wabunge tunaendelea na Wizara ya Maliasili na Utalii Mheshimiwa Mohamed Omary Mchengerwa, Mbunge wa Rufiji, sasa aulize swali lake.

MHE. MOHAMED O. MCHENGERWA: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Warufiji wote duniani ninaomba sasa swali langu liweze kupatiwa majibu. (*Kicheko*)

Na. 74

**Matatizo ya Mipaka ya Wananchi
na Eneo la Hifadhi - Rufiji**

MHE. MOHAMED O. MCHENGERWA Aliuliza:-

Matatizo ya mipaka kati ya wanakijiji na maeneo ya hifadhi husababisha migogoro kati ya wanakijiji na watumishi wa hifadhi.

Je, Serikali inachukua hatua gani kurejesha mahusiano kati ya watumishi wa hifadhi na wananchi?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Mchengerwa ninyi wana Rufiji mmetawanyika kiasi gani mpaka ututangazie sisi kwamba dunia nzima? Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii majibu. (*Kicheko*)

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII Alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mohamed Omary Mchengerwa, Mbunge wa Rufiji, kama kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba matatizo ya mipaka kati ya vijiji na maeneo ya hifadhi mara kadhaa imesababisha migogoro kati ya wananchi na wahifadhi na wakati mwengine hata kusababisha maafa katika baadhi ya maeneo.

Wizara yangu imeendelea kuchukua hatua mballimbali katika kudumisha na kuboresha mahusiono baina ya wananchi na wahifadhi zikiwemo:-

(a) Kuendelea kutoa elimu ya uhifadhi na faida zake na kuwakumbusha wahifadhi juu ya umuhimu wa kuendelea kutekeleza majukumu yao kwa kuzingatia sheria, kanuni na utaratibu.

(b) Kusaidia kuimarisha uwezo wa usimamizi wa maliasili katika ngazi za vijiji na Wilaya ikiwemo kuhamasisha uanzishwaji wa Jumuia za Hifadhi za Wanyamapori (*Wildlife Management Areas – WMAs*) na kuimarisha zilizopo.

(c) Kuhakikisha wananchi wanaoishi katika maeneo yanayopatikana na hifadhi wanafaidika na faida zitokanazo na uhifadhi katika maeneo yao kwa mujibu wa kanuni na taratibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu itaendelea kushikiana na wadau mballimbali katika kutekeleza sera taratibu za uhifadhi shirikishi ili kuboresha uhifadhi na kudumisha mahusiano na mashirikiano kati ya wahifadhi na wananchi.

MHE. MOHAMED O. MCHENGERWA: Mheshimiwa Naibu Spika, nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sekunde moja naomba niendelee kutoa pole kwa wananchi wangu wa Rufiji hususan tukio la jana ambapo Mwenyekiti wa Kijiji cha Nyambuji alitaka kuuawa lakini alisalimika baada ya kukimbia kugundua majambazi wale wameshaingia nyumbani kwake, taarifa ambazo nimezipokea muda huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nina maswali mawili tu ya nyongeza; la kwanza nimuulize Mheshimiwa Naibu Waziri migogoro baina ya wananchi na wahifadhi imechangiwa na kuondolewa kwa mipaka ya awali iliyokuwepo hususan katika Kata ya Mwaseni na wananchi kuzuiliwa kuvua samaki wale ambao wapo katika vijiji vinavyopakana na hifadhi.

Naomba kufahamu Serikali ina mpango gani sasa ili yale mabwawa matano niliyoyaomba kwenye Wizara ya Maliasili na Utalii yaweze kuchimbwa haraka katika Kata ya Mwaseni, Kata ya Kipugira hususan maeneo ya Nyaminywili, Kipo na Kipugila pia katika Kata ya Ngorongo?

Naomba kufahamu Serikali inaharakisha vipi mchakato wa uchimbwaji wa mabwawa ya samaki kwa wananchi wangu wa maeneo hayo?

Mheshimiwa naibu Spika, lakini pili.....

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Mchengerwa umeshauliza maswali mawili tayari sasa hilo litakuwa la tatu labda kama unafuta mojawapo tuambie unafuta lipi kati ya hayo mawili uliyouliza ndiyo uulize swali la pili.

MHE. MOHAMED O. MCHENGERWA: Mheshimiwa Naibu Spika, ninafuta hilo swali la samaki, naomba la mgogoro wa mipaka libaki.

Swali la pili, watumishi wa hifadhi wamekuwa wakiweka *beacons* na alama kadhaa katika baadhi ya nyumba hususani katika maeneo ya Kipugila maeneo ya Nyaminywili na maeneo mengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchakato wa uwekaji wa *beacons* unakiuka Ibara ya 13 ya Katiba, pia unakiuka Ibara ya 16 ya Katiba ambayo inazungumzia haki za msingi za wananchi ubinafsi wao, ufamilia wao pamoja na uhifadhi wa maskani zao.

Ninaomba kufahamu je, Wizara hii ya Maliasili na

Utalii imedhamiria kabisa kukiuka Katiba ya haki za msingi ya Ibara ya 13 na Ibara ya 16, katika kuweka *beacons* na kusababisha uhuru wa wananchi wa mnaeneo husika kukosa haki zao za msingi? (*Makof!*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii majibu.

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuanza na swali lake la pili. Uchukuaaji wa hatua wa wawekaji mipaka kwenye maeneo yote ya hifadhi unafanyika hivyo kwa mujibu wa sheria. Kama tunavyofahamu zimetungwa na Bunge lako Tukufu jambo ambalo limefanyika pia kwa mujibu wa Katiba.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa ule ni utekelezaji wa sheria ambazo zipo kwa mujibu wa Katiba, napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba hata mara moja Serikali kupitia Wizara ya Maliasili haiwezi kuvunja Katiba. Iwapo kuna jambo lolote mahususi ambalo anadhani kwamba linaweza kufanana na hicho anachokisema basi namkaribisha aweze kuja kuniona tuweze kulijadili na kuweza kulipatia ufumbuzi zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika swali la pili ambalo lilikuwa la kwanza la uwekaji wa mipaka au uwekaji wa alama. Uwekaji wa alama ni hatua inayochukuliwa baada ya kuwa tayari mipaka ilikuwepo miaka mingi iliyopita. Wakati wa utekelezaji wa zoezi la uwekaji wa alama Wizara inafanya mazoezi haya kwa kushirikisha wananchi katika maeneo yanayohusika.

Mheshimiwa Naibu Spika, naamini katika maeneo ambayo ameyataja Mheshimiwa Mchengerwa zoezi hili limefanyika kwa utaratibu huo wa kushirikisha wananchi, iwapo kuna hoja mahsusizi zinazohusiana na alama hizo basi anaweza kuzileta kwa kutaja vijiji vyenyewe hasa ili tuweze kuona namna ambavyo tunaweza kwenda kuona namna bora zaidi ya kwenda kuweka alama hizo. Nisisitize kwamba zoezi hili kwamba zoezi hili ni agizo la Serikali kupitia maagizo

ya Viongozi Wakuu wa Serikali akiwemo Mheshimiwa Waziri Mkuu na kwa hiyo litaendelea lakini jambo la msingi tutaendelea kushirikisha wananchi ili liweze kuwa zoezi rafiki.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Joshua Nassari swali la nyongeza.

MHE. JOSHUA S. NASSARI: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kuniona na mimi niulize swali moja dogo la nyongeza.

Migogoro ambayo imeendelea kuwepo baina ya vijiji ambavyo vinazunguka hifadhi haviko kwa Mheshimiwa Mchengerwa peke yake, pale Arumeru kuna Hifadhi ya Taifa ya Arusha (*Arusha National Park*) na imekuwa na mgogoro wa siku nyingi sana hususani kijiji cha Momela, kitongoji cha Momela na hifadhi. Hifadhi ya Taifa ya Arusha ni milongoni mwa hifadhi changa ambazo zimekuja kuanzishwa miaka ya juzi juzi tu.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Nassari muda wetu ni mfupi tafadhali liwe fupi.

MHE. JOSHUA S. NASSARI: Swali langu kwa Mheshimiwa Waziri Makani ni kwamba ni lini basi atakuwa tayari tuende Arumeru ili tuweze kwenda kuhuisha mgogoro ambaao umekuwepo baina ya Kijiji cha Momela wananchi wa King'ori na wananchi wa Kiburuki na Hifadhi ya Taifa ya Arusha ili tuweze kurudisha mahusiano?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii majibu.

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Naibu Spika, kama ambavyo amesema ni kweli kwamba masuala yanayohusiana na migogoro ya mipaka baina ya maeneo yaliyohifadhiwa na maeneo wanayoishi wananchi yapo maeneo mengi katika nchi nzima.

Mheshimiwa Naibu Spika, Hifadhi ya Taifa ya Arusha

(Arusha National Park) ni mojawapo tu ya maeneo hayo, lakini nilikumbushe Bunge lako Tukufu kwamba hivi tunavyozungumza ile Kamati ambayo tayari ilkwishaundwa inayoshirikishwa Wizara zaidi ya nne bado inaendelea na zoezi lake, watakapokuwa wamekamilisha kazi yao watakuwa wametoa ushauri Serikalini kuhusu namna bora zaidi ya kushughulikia migogoro hii ambayo tumekuwa tukiishughulikia kwa miaka mingi, lakini pengine tulikuwa hatujapata dawa ambayo ni sahihi. Sasa wakati tunasubiri kamati hii ikamilishe kazi yake pengine itakuwa si jambo muhimu sana kwenda mahali ambapo pengine Kamati hii itakuwa imekwenda.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo nafikiri itakuwa ni bora zaidi mimi na Mheshimiwa Nassari baada ya kuwa nimewauliza Kamati wamefikia wapi kama ni suala la kwenda kuona mimi na yeye tunaweza kwenda kama itasema kwamba bado haijakamilisha zoezi hili kwenye eneo analolizingumzia.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa tunaendelea, Wizara ya maji na Umwagiliaji Joseph Leonard Haule, Mbunge wa Mikumi sasa aulize swalı lake.

Na. 75

Kukarabati Miundombinu ya Mradi wa Maji wa Madibira

MHE. JOSEPH L. HAULE Aliuliza:-

Mradi wa maji Madibira ulianzishwa mwaka 1975 na sasa miundombinu yake imechakaa sana na banio (*intake*) lake imekuwa dogo sana wakati idadi ya watu imeongezeka sana.

Je, Serikali haioni umuhimu wa kukarabati miundombinu hiyo ili kuwaokoa wananchi wa Mikumi na taabu ya maji?

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI Alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji na Umwagiliaji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Joseph Leonard Haule, Mbunge wa Mikumi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ilikwishabaini changamoto zinazoukabili mradi wa maji wa Madibira unaotumiwa na wananchi wa Mikumi. Changamoto hizo kwa sehemu kubwa zinachangiwa na uchakavu wa miundombinu ya mradi pamoja na ongezeko la watu, hivyo kusababisha kiasi cha maji kinachozaishwa kutokidhi mahitaji ya maji kwa wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tayari Serikali imechukua hatua za kutatua changamoto ya maji katika eneo la Mikumi, ambapo Wizara ya Maji na Umwagiliaji chini ya programu ya maendeleo ya sekta ya maji inatekeleza ujenzi wa mradi mpya wa maji wenye thamani ya shilingi milioni 809.4, hadi kufikia Machi, 2017 mradi huo umekamilika kwa wastani wa asilimia 86 na unatarajiwa kukabidhiwa mwishoni mwa mwezi Mei, 2017 kukamilika kwa mradi huo, kutaboresha hali ya huduma ya maji katika Mji wa Mikumi. Baada ya kukamilika kwa mradi huo mpya, Serikali itaanza pia kufanya ukarabati wa mradi wa maji wa Madibira ili kuwezesha uendelee kutoa huduma ya maji katika Mji wa Mikumi.

MHE. JOSEPH L. HAULE: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana.

Pamoja na jitihada za Serikali za kukamilisha huu mradi wa *World Bank*, Mji wa Mikumi ni Mji wa kitalii na umekuwa ukipata wageni mbalimbali na idadi ya watu imeongezeka wamekaribia wakazi 30,000, lakini Mikumi kuna vyanzo vingi kama lyovi, Madibila na pia Mto Muhanzi.

Je, Serikali haioni umuhimu wa kuweza kutumia vyanzo vingine ili viweze kusaidiana na mradi huu ili iweze kusaidia wananchi wa Jimbo la Mikumi na kadhia hii?

Swali la pili, katika ziara ya Naibu Waiziri ulipokuja uliagiza watalaan waje kuangalia chanzo cha maji cha Sigareti pale Kata ya Ruaha ambapo kingeweza kusaidia Kata ya Ruaha na Rwembe, wameshafanya hivyo na kukuletea taarifa na imeonekana takribani shilingi bilioni mbili zinahitajika ili kuwezesha wananchi wa Ruaha waweze kupata mradi huo.

Je, Mheshimiwa Waziri unaweza kuwaahidi viyi wananchi wa Ruaha ambao sasa wanakutazama kwamba je, huu mradi utaingizwa katika Bajeti ya 2017/2018 ili uweze kuwasaidia wananchi wa Jimbo la Mikumi kwa ujumla? (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji na Umwagiliaji, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:

Mheshimiwa Naibu Spika, kama alivyotaja kwamba ni kweli nilishawahi kutembelea Jimbo la Mikumi kwenda kuangalia miundombini ya maji. Ni kweli tulienda na ye ye mpaka Kijiji cha Ruaha na tukaona chanzo cha Segereti na tukaagiza. Kwa sababu kwa sasa hivi tuna utaratibu Wizara kwamba tunaweka fedha kila Halmashauri, basi kwa kutumia nafasi hili niagize ule mradi ambao tuliagiza kamba waufanyie mchakato wa kufanyiwa usanifu ukikamilika basi watumie fedha tutakazozitenga katika Bajeti ya mwaka 2017/2018.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia chanzo cha Madibira tayari tumeshamuagiza Mkurugenzi wa Maji wa Mamlaka ya Morogoro (*MORUWASA*) ambaye Aprili anatanganza *tender*, ifikapo Juni na Julai tayari atakuwa amempata mkandarasi kwa ajili ya kuboresha kile chanzo cha Madibira ambacho kina umbali wa kilometra 17 kutoka chanzo kuja mjini Mikumi na kazi zitakazofanyika ni pamoja na kwanza kuboresha chanzo chenyewe cha maji cha Madibira ili kiweze kupanuliwa kuongeza kiwango cha maji na kuweka mabomba mapya ambayo yataleta maji katika Mji wa Mikumi.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Mboni Mhita swali la nyongeza.

MHE. MBONI M. MHITA: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuniona.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Jimbo la Handeni Vijijini, Kata ya Mkata tulibahatika kupata mabwawa mawili, moja likiwa Mkata lakini la pili likiwa eneo la Manga.

Mheshimiwa Naibu Spika, mabwawa haya yako chini ya kiwango na mpaka sasa hayajaweza kuanza kutumika. Nimshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri katika ziara yake katika Jimbo la Handeni Vijijini alipita na kujionea hali halisi ya yale mabwawa. Pia aliweza kutuahidi wananchi wa Jimbo la Handeni.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa uliza swali la nyongeza.

MHE. MBONI M. MHITA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakuja hapo. Mheshimiwa Naibu Waziri alituahidi baada ya kuona yale mabwawa kwamba wangefanyia kazi na kuweza kutupa ripoti ili hatua stahiki ziweze kuchukuliwa kwa wale ambao wamefanya ubadhilifu ili kuweza kupata utatuzi wa maji.

Wananchi wa Handeni Vijijini wangependza kujua, je, utatuzi umefanyika na ripoti imeshafanyiwa kazi ili tuweze kujua na hatua stahiki ziweze kufanyika kwa wale ambao wamefanya ubadhilifu huu? Nashukuru sana.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji na Umwagiliaji majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, nilitembelea kweli eneo hilo la Mkata nikakuta kazi iliyofanyika na kazi hiyo nilizungumza kwenye vyombo vya habari kwamba hata mimi sikuridhika nayo. Baada ya hatua hiyo Katibu Mkuu aliunda Tume ya Wahandisi kwenda kukagua hilo eneo, sasa hivi

wanakamilisha kuandaa taarifa ili iweze kuwasilishwa Wizarani ili kuweza kuchukua hatua.

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hilo lengo letu ni kuhakikisha wananchi wanapata maji. Tuliweka utaratibu mwingine tumeshatangaza tenda tayari kwa ajili ya kupanua mradi wa *HTM* pale Korogwe ili uhakikishe kwamba unapeleka maji hadi Handeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia tulishasema tunaweza tukatumia chanzo cha Wami ili tuweze kuchukua yale maji kuhakikisha kwamba eneo la Handeni Vijijini linapata maji ya kutosha. (*Makof*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Oran Njenza, swali la nyongeza.

MHE. ORAN M. NJENZA: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana, suala la Mji Mdogo wa Mbalizi kuna changamoto kubwa za maji kama iliyokuwa kwa Mji wa Mikumi. Je, ni lini mtatatua changamoto kubwa ya maji kwenye Mji Mdogo wa Mbalizi? Ahsante.

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa wa Mbeya tuliwasiliana nae nikiwa kwenye ziara Mbeya na tukawa tumekubaliana kwamba tufanye mapendeleko, Wizara imeshaagiza tayari kwamba Mamlaka ya Maji ya Mkoa wa Mbeya ijipanue ili iweze kuhudumia mpaka eneo la Mbalizi. Tayari wanaendelea na utaratibu huo wameshafanya mazungumzo na Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mbalizi na Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mbalizi ameonekana kuridhia ili Mamlaka ya Maji ya Mbeya iweze kupeleka miundombinu mpaka Halmashauri ya Mbalizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, niahidi kwamba taratibu hizi zitakamilishwa na wananchi wa Mbalizi watapata huduma ya maji kutokana na Mamlaka ya Maji ya Mji wa Mbeya.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Mussa Mbarouk swali la nyongeza.

MHE. MUSSA B. MBAROUK: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

Mheshimiwa Naibu Spika, takribani mwezi sasa wakazi wa Jiji la Tanga wanapata maji kuitia mamlaka ya maji ambayo siyo safi na salama.

Je, Serikali ina taarifa kwamba wakazi wa Tanga wanaweza kupata maradhi ya milipuko kutokana na kutokunywa maji ambayo siyo safi na salama? (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji na Umwagiliaji, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, katika mamlaka ambazo zinaongoza kutoa huduma ya maji iliyo bora ni pamoja na Mamlaka ya Maji ya Tanga na Mamlaka ya Maji ya Moshi. Sasa kama hilo limejitokeza basi Mheshimiwa Mbunge nikuahidi kwamba tutalifuatilia kuona ni nini kimejitokeza katika hilo. Kwa taarifa tulizonazo ni kwamba mamlaka zinazoongoza ni pamoja na Mamlaka ya Maji ya Moshi na Tanga. Kwa hiyo, nikuahidi kwamba tutalifuatilia kuona ni eneo gani ambalo liliptata hiyo shida ya maji kutokuwa salama. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea. Mheshimiwa Pauline Philip Gekul, Mbunge wa Babati Mjini, sasa aulize swali lake.

Na. 76

Tathmini ya Miradi ya Maji ya Visima 10

MHE. PAULINE P. GEKUL Aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itafanya tathmini ya miradi ya maji ya visima kumi katika vijiji inayofadhiliwa na Benki ya Dunia?

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI Alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji na Umwagiliaji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Pauline Philipo Gekul, Mbunge wa Jimbo la Babati Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kwa kushirikiana na Benki ya Maendeleo ya Afrika ilifanya tathmini ya awamu ya kwanza ya Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji mwaka 2015 ambapo katika Halmashauri ya Mji wa Babati, Serikali ilipanga kutekeleza miradi ya maji katika vijiji vya Mutuka, Chemchem, Kiongozi, Malangi, Managhat, Halla, Himti, Haraa, Nakwa na Imbilili. Ujenzi umekamilika katika vijiji vinne vya Mutuka, Himti, Chemchem na Managhat ambapo wananchi wanapata huduma za maji. Ujenzi wa miradi mingine katika vijiji sita unaendelea na umefikia hatua mbalimbali za utekelezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali itahakikisha inazifanya kazi changamoto zilizojitokeza katika kutekeleza awamu ya kwanza ya Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji. Baadhi ya changamoto hizo ni kuchelewesha manunuzi ya miradi, upungufu wa wataalam wa maji, kukosa wataalam wabobezi wa taaluma za kifedha pamoja na baadhi ya maeneo yaliyokusudiwa kuchimba visima kukosa maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile Halmashauri zote zinaendelea kupewa mafunzo ili kujenga uwezo wa kusimamia miradi, kusajili na kuunda vyombo na kuimarisha usimamizi wa mfumo wa ukusanyaji wa takwimu za miradi ya maji vijijini ili kuwa na takwimu sahihi.

MHE. PAULINE P. GEKUL: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri alifanya ziara katika Jimbo la Babati Mjini na akabaini kero za maji. Kwa hiyo, haya nitakayoyaauliza anayafahamu vema na atanipa majibu.

Swali la kwanza, kwa kuwa mradi wa maji wa kijiji cha Malangi umechukua muda mrefu sana na kwa kuwa mradi huu ultelekezwa na mkandarasi wa awali, na kwa kuwa mradi huu sasa thamani yake siyo shilingi milioni 400 ni shilingi milioni 600.

Je, Serikali iko tayari kutupatia fedha hizo shilingi milioni 600 kwa ajili ya kukamilisha mradi wa maji Malangi ili wananchi hao wapate maji kwa muda mrefu ambaeo walikuwa wameyakosa?

Swali la pili, kwa kuwa mradi wa maji wa kijiji cha Nakwa wenye thamani ya shilingi milioni 801 umekuwa na changamoto nyingi, mabomba yapojuu hayajawekwa chini, yamekuwa yakipasuka wakati huu ambapo mradi unafanyiwa majoribio, na kwa kuwa vijana ambaeo pia walichimba mitaro kwa ajili ya kulaza yale mabomba hawajalipwa na mkandarasi ambaye anafanya kazi hiyo. Ilikuwa vijana hao walipwe shilingi 4,000 kwa kila mita wamelipwa shilingi 700.

Je, Naibu Waziri yako iko tayari kuunda timu ya wataalam kwenda kukagua mradi wa kijiji cha Nakwa ambaeo umekuwa ukisumbua wananchi hawa kwa mradi huo kuchakachuliwa? (*Makofii*)

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ni kweli nilitembelea Babati na hizi changamoto tukiwa pamoa na Mheshimiwa Mbunge tuliziona na tulizijadili na kutoa maekelezo. Nikuahidi Mheshimiwa Mbunge kwamba kwa utaratibu tuliuweka kwamba kila Halmashauri inapata bajeti.

Kwa hiyo, hii fedha kwenye mradi wa Malangi tutahakikisha sasa unasimamiwa vizuri na pale nilitoa maelekezo kwamba Waheshimiwa Wabunge mnapoona inasua sua kwenye Halmashauri kama Mamlaka ya Maji ya Mkoa ambayo ipo chini ya Wizara ya Maji basi ni lazima tushirikiane katika utaalam ili kuhakikisha kwamba miradi inatekelezwa katika viwango vinavyotakiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tumetenga fedha katika mwaka wa fedha unaokuja. Ile bakaa ya upungufu iliyobaki itaongezwa kuhakikisha kwamba mradi huu unakamilika. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili ni kijiji cha Nakwa, Mheshimiwa Mbunge mwenyewe ni shahidi unakumbuka kwanza tulitengeneza utaratibu kwamba kama mradi wa maji uliotekelawa na Halmashauri uko karibu na Mamlaka ya Maji ya Mkoa, wakati wanapotekeleza ule mradi inabidi washirikiane ili kuhakikisha kwamba vile viwango vinavyotakiwa katika mradi viweze kufikiwa na hasa kwa kuwa mara nyingi miradi kama hiyo kwa sababu mamlaka za maji zina maji mengi, kumekuwa na tabia ya Wakurugenzi wanaomba mradi huo uunganishwe kwenye Mamlaka ya Maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa suala hili pale tuliajiza kwamba Mkurugenzi wa Maji wa Babati sasa ashirikiane na Halmashauri ili kuweza kuhakikisha kwamba huu mradi ambao haukutengenezwa vile inavyotakiwa basi uhakikishe kwamba kwanza wanautekeleza katika viwango vinavyotakiwa. Pia nakubaliana na wewe kwamba Serikali italiangalia hili ili kuhakikisha wale walioharibu hatua stahiki zinachukuliwa. (*Makof*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Kanyasu, swali la nyongeza.

MHE. CONSTANTINE J. KANYASU: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mji wa Geita na Kasamwa kuna shida kubwa sana ya maji na Mheshimiwa Waziri tangu mwaka jana alisema wamepata pesa kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya maji katika Mji wa Geita. Je, ni lini sasa mradi huo wa maji utatekelezwa?

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, Mji wa Geita una miradi miwili, mradi mmoja ni ule ambao tunashirikiana na *GGM* na

umeshatekelezwa mpaka tukafikia asilimia 30 tayari Mji wa Geita unapata maji. Pia unapata kutokana na ufadhilli unaotokana na uboreshaji wa mazingira wa Ziwa Victoria.

Mheshimiwa Kanyasu, tayari katika mkopo tulio pata wa milioni 500 kutoka Serikali ya India, sehemu ya fedha hiyo inatarajiwa kuboresha maji katika Mji wa Geita. Sasa hivi tunaendelea vizuri kwa ajili ya kumpata *consultant* atakayefanya mapitio na kuandaa *tender document* baada ya hpo kutangaza tenda ili tuweze kupata sasa maji ya uhakika kwa Mji wa Geita. (*Makofii*)

MHE. HAWA S. MWAI FUNGA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kuniona.

Mheshimiwa Naibu Spika, Jimbo la Tabora Mjini lina kata 29, katika kata hizo kata 11 hazipati maji kabisa. Ni tatizo linalotokana na Serikali kudaiwa kiasi cha shilingi bilioni mbili na mkandarasi. Je, ni lini Serikali italipa pesa hizo ili hizi kata 11 ziweze kupatiwa maji? (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji na Umwagiliaji, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza bahati nzuri kwenye sherehe ya Pasaka nillienda Jimboni kwangu nimepita Tabora, nimekuta Mamlaka yetu ya Tabora imenunua mabomba mengi kuhakikisha kwamba katika hizi kata zilizosalia ni kata tisa ambazo zimebaki hazipati huduma ya maji mjini. Kwa hiyo, kata moja tayari inawekewa miundombinu ya maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuititia mradi ambao tarehe 22 Mheshimiwa Waziri anakwenda kushuhudia kusaini mikataba ya mradi wa kutoa maji Solya kupeleka Nzega, Igunga na Tabora, kata zote zilizobaki sasa zitapata huduma ya maji kutoka kwenye huu mradi mpya. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge baada ya mwaka mmoja au miwili Mji wa Tabora tutakuwa tumemaliza kabisa matatizo ya maji. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa tunaendelea, Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Mheshimiwa Balozi Dkt. Diodorus Buberwa Kamala, Mbunge wa Nkenge sasa aulize swali lake.

Na. 77

Agenda ya Mabadiliko – Jumuiya ya Ulaya

MHE. BALOZI DKT. DIODORUS B. KAMALA Aliuliza:-

Jumuiya ya Ulaya inatekeleza Mkakati wa Ajenda ya Mabadiliko.

Je, Tanzania imejipangaje kukubaliana na changamoto zinazotokana na Ajenda hiyo ya Mabadiliko ya Jumuiya ya Ulaya?

NAIBU WAZIRI, MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI Alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Balozi Dkt. Diodorus Buberwa Kamala, Mbunge wa Nkenge, naomba kutoa maelezo mafupi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, agenda ya Mabadiliko ya Umoja wa Ulaya ilipitishwa mwaka 2011 ikiwa na lengo la kuongeza ufanisi wa Sera ya Maendeleo ya Umoja huo. Mabadiliko haya yanahusisha kanuni mbalimbali za kutoa misaada ya maendeleo. Kanuni hizo ni pamoja na utofautishaji wa kiwango cha maendeleo kilichofikiwa na kila nchi inayotarajiwaa kupatiwa msaada.

Katika kutekeleza hili, Umoja wa Ulaya unalenga kutoa misaada kwa nchi zenyet uhitaji zaidi na mkazo ukiwa katika kusaidia kupunguza umaskini katika nchi hizo. Kanuni nyingine ni kuelekeza misaada yake katika sera za kipaumbele ambazo zimebainishwa katika Mkakati wa Kimataifa wa

Maendeleo Endelevu wa 2030. Mkakati wa Ajenda ya Mabadiliko umeainisha maeneo yatakayopewa kipaumbele katika utekelezaji wake ikiwemo masuala ya haki za binadamu na utawala bora, usawa wa jinsia, vyama vya kiraia na Serikali za Mitaa, rushwa, sera, usimamizi wa kodi na usimamizi wa sekta ya umma.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na maelezo hayo, napenda kuliarifu na Bunge lako Tukufu kuwa Serikali imechukua hatua mahsusizi zifuatazo katika kukubaliana na changamoto zitokanazo na Agenda ya Mabadiliko ya Umoja wa Ulaya:-

- (i) Serikali imeimarisha ukusanyaji wa mapato ya ndani na kusimamia matumizi ya fedha za umma ili kuhakikisha tunapunguza utegemezi kwa kiasi kikubwa katika utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo;
- (ii) Serikali inaendelea kuhamasisha sekta binafsi kushiriki katika utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo kwa kuzingatia Sera ya Ubia baina ya Serikali na Sekta binafsi ya mwaka 2009 na Sheria ya Ubia baina ya Serikali na Sekta Binafsi ya mwaka 2010. Mkakati huu unasaидia kuongeza wigo wa vyanzo vya fedha za kugharamia miradi ya maendeleo na kupunguza utegemezi kwa wahisani;
- (iii) Serikali inaendelea kuwashawishi wawekezaji kutoka nchi mbalimbali kuja kuwekeza zaidi hapa nchini. Jitihada hizi zinaenda sambamba na uboreshaji wa mazingira ya kufanya biashara nchini na kupunguza gharama za kufanya biashara na uwekezaji ili kuvutia wawekezaji zaidi kuwekeza hapa nchini; na

- (iv) Wizara yangu imeanzisha idara maalum ya kuratibu masuala ya *diaspora* kwa lengo la kuratibu uhamasishaji wa Watanzania waishio ughaibuni kushiriki katika shughuli za maendeleo ya nchi yetu, ikiwa ni pamoja kuwekeza hapa nyumbani. (*Makof*)

MHE. BALOZI DKT. DIODORUS B. KAMALA: Mheshimiwa

Naibu Spika, ahsante sana. Ninayo maswali madogo mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Swali la kwanza, kwa kuwa Jumuiya ya Ulaya katika mpango wake wa miaka mitano au kwa lugha nyepesi *Multiannual Financial Framework* waliahidi kuisaidia Tanzania Euro milioni 629, kwa kuwa hii inaendana na mpango wa *Agenda For Change* ina dalili ya kupungua misaada hiyo.

Je, kwa Tanzania misaada hiyo itatoka kama walivyoahidi au inapungua kwa kuzingatia sera yao ya ajenda ya mabadiliko?

Swali la pili, kwa kuwa hivi sasa tunaandaa *GSP*, Tanzania tumefanya uamuzi katika Bunge hilli kwamba sasa *EPA* basi ikiwezekana, lakini sasa kwa uamuzi huo maana yake sasa tutafanya biashara ya kuititia *GSP* au *DSP Plus*.

Je, kulingana na hii ajenda ya mabadiliko tunajiandaaje sasa kuingia katika mlolongo huu? (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, majibu.

NAIBU WAZIRI, MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI: Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kuthibitisha au kusema kwamba ahadi ambayo ilifanywa na Jumuiya ya Ulaya ya kuahidi kuisaidia Tanzania Euro milioni 628 kwamba itabaki pale pale au itapungua au kuongezeka.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema katika vigezo ambavyo wao wameviweka kama *framework* ya kuweza kutoa misaada hiyo ni kuhakikisha kwamba nchi inaweza kuhakikisha inasimamia vizuri suala la la haki za binadamu na utawala bora, usawa wa jinsia, kuhakikisha kwamba vyama vya kiraia vinafanya kazi zake vizuri, kusimamia shughuli zinazofanywa na Serikali za Mitaa, kusimamia vizuri na kuhakikisha kwamba tunapambana na rushwa, kuhakikisha kwamba tunasimamia sera za usimamizi wa kodi na usimamizi wa sekta ya umma. Hivi vyote

vinafanyika ndiyo maana unakuta kwamba mpaka sasa hivi hata *World Bank* wanaendelea kutupa misaada.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunachotakiwa kufanya kama Watanzania ni kuhakikisha kwamba tunaendelea kuishi na kusimamia utawala bora na sekta ya umma inasimamiwa vizuri. Hilo ndiyo jibu langu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kwamba katika Bunge hili liliamua kwamba suala la kusaini mkataba wa *EPA* sasa basi, kwa hiyo, sasa Tanzania inafanyaje. Tanzania imejipanga vizuri kama nilivyosema katika majibu yangu ya msingi kuhakikisha kwamba inahamasisha sekta binafsi ifanye kazi pamoja na Serikali. Vilevile inahamasisha mashirika ya nje na nchi nyngine za nje kuja kuwekeza katika nchi yetu. Wizara yangu imefanya kazi hiyo vizuri na mifano mmeionna.

Vilevile kama nilivyosema kwamba *diaspora* tunaendelea kuwasimamia na kuwahamasisha katika Balozi zetu, Mabalozi wanafanya mikutano na hawa *diaspora* ili kuhakikisha kwamba wao pia wanatumia fursa ya kuwekeza katika nchi yetu. Katika mwelekeo huo tutakuwa tunalinda maslahi ya nchi yetu na siyo kuyapoteza. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Mheshimiwa Subira Khamis Mgusu, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 78

Ujenzi wa Barabara ya Kisarawe – Maneromango

MHE. SUBIRA K. MGALU Aliuliza:-

Je, ni lini ujenzi wa barabara ya kutoka Kisarawe - Mwanerumango kilometra 64 itajengwa kwa lami na kukamilika kama ilivyoahidiwa kwenye llani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2015?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA
MAWASILIANO** Alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Subira Khamis Mgalo, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara ya Kisarawe - Mpuyani - Maneromango yenye urefu wa kilometra 54 ni sehemu ya barabara ya Mkoa ya Pugu - Kisarawe - Maneromango - Vikumburu ambayo jumla yake ni kilometra 97.7 inayohudumiwa na Wakala ya Barabara wa Mkoa wa Pwani. Upembizi yakinifu na usanifu wa kina kwa ajili ya ujenzi wa kiwango cha lami wa barabara hii umekamilika. Aidha, mpaka sasa kilometra 7.67 zimeshajengwa kwa kiwango cha lami. Mkandarasi anaendelea na ujenzi wa kipande kingine cha mita 800.

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu iliyobaki ya barabara hii ni ya changarawe na hufanyiwa matengenezo ya kawaida na ya muda maalum kila mwaka ili ipitike muda wote. Ujenzi kwa kiwango cha lami utaendelea hatua kwa hatua kulingana na upatikanaji wa fedha.

Aidha, katika mwaka wa fedha 2017/2018 jumla ya shilingi bilioni 3,157 zimependekezwa kwa ajili ya kuendelea kuijenga kwa kiwango cha lami barabara hii. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Subira Mgalo, swalii la nyongeza.

MHE. SUBIRA K. MGALU: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru.

Kwanza namshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa jibu zuri lenye kuleta matumaini kidogo kwamba mwaka huu wa fedha wamependekeza kutenga kiasi cha shilingi bilioni tatu. Kwa kuwa kiwango hiki ni kidogo na kwa kuwa barabara hii imeahidiwa tangu llani ya 2005.

Je, Serikali haioni sasa ni wakati muafaka wa kutafuta chanzo kingine, mfano mikopo yenyeye masharti nafuu kutoka Benki ya Dunia, Benki ya Maendeleo ya Afrika ili kuweza kuikamilisha kwa kuwa eneo hili linataka kuwa la viwanda?

Swali la pili, kwa kuwa wakazi wa maeneo hayo yanayopita barabara hii ya Kisarawe - Mpuyani - Manerumango, maeneo ya Kazimzumbwi, Masaki, Kibuta pamoja na Marumbo na Manerumango yenyewe, wakazi hawa walizuiwa maeneo yao wasiyaendeleze wala kukarabati nyumba zao lakini mpaka sasa wakazi hawa hawajui fidia gani watakayolipwa. Kwa kuwa katika jibu la msingi amesema upembuzi yakinifu umekamilika.

Je, ni lini wakazi wa maeneo haya watalipwa fidia yao wale wanaostahili? Ahsante. (*Makofii*)

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO: Mheshimiwa Naibu Spika, nimepokea ushauri wake wa kutafuta vyanzo vingine ili kuhakikisha barabara hii tunaikamilisha, tutakwenda kuufanyia kazi ushauri wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu fidia kwa wananchi wa Kazimzumbwi, Mabuta na maeneo mengine, hadi Maneromango, kwanza ningeomba hii dhana ya fidia ielewewe wazi na Waheshimiwa Wabunge wote na mtusaidie kwa wananchi. Tukiwa na kauli moja wananchi hawatahangaika, kwa sababu kauli yetu kupitia sheria tuliyopitisha ndiyo ilikuwa kwa umoja wetu, sasa ni vizuri tunapolishughulikia hili suala la fidia katika maeneo ambayo barabara zinapita au miradi mingine ya miundombinu inapita, tuwe na kauli inayofanana na sheria tulizopitisha ili tuisiwachanganye wananchi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuwekewa alama ya 'X' iwe ya kijani au iwe nyekundu maana yake ni kwamba nyumba hiyo au jengo hilo au shamba hilo au miti hiyo iko ndani ya hifadhi ya barabara. Waliowekewa kijani maana yake ni kwamba watakuja kufidiwa, lakini haina maana kwamba wanafidiwa wakati huo huo au waendeleze

nyumba zao, maana yake ukiendeleza unaongeza gharama tena za kufidia, unaipa gharama zaidi Serikali na lengo la Serikali ni kipeleka miundombinu katika maeneo hayo, *prime objective* siyo kufidia, *prime objective* ni kujenga miundombinu, lakini ni lazima tuwafidie wale ambaو wana haki ya kufidiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, niwaombe wananchi wote ambaو wamewekewa 'X' wajue kwamba wako ndani ya eneo la mradi, watafute maeneo mengine, tena ni vizuri wakatafuta taratibu kwa muda wa kutosha badala ya kuja kuhangaika dakika za mwisho, mara nyingi kwa mfano wale ambaو wana 'X' nyekundu watakuja kubomolewa bila fidia na wale wa kijani kwa vyovyote kabla barabara haijajengwa au kupanuliwa tutawafidia mara tunapopata fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba sana Mheshimiwa Subira Mgalo, kuitia kwako natambua mchango mkubwa unaotolewa na pacha wako, Mheshimiwa Selemani Jafo katika suala hili...

NAIBU SPIKA: Ahsante Mheshimiwa...

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO: Ninawapongeza sana kwa kazi kubwa mnayofanya kwa pamoja...

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO: Kwa ushirikiano huo tutahakikisha barabara hii inajengwa. (*Makof!*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, nadhani haya maswali ya kuwekewa alama na fidia yanajirudia kila wakati. Sasa nadhani ili tupunguze maswali ya namna hiyo, zinapowekwa hizo 'X' watu wajue ni lini watapata fedha za kutafuta maeneo kama wewe ulivyosema, kwamba

watafute, sasa watatafuta vipi wakati walishajenga na wanahitaji sasa fedha ili wakanunue eneo lingine. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa hiyo mtusaidie ili ukashatoa jibu ni rahisi kumwambia Mbunge tulishajibu hili namna hii, kuliko yanarudia hayo kila wakati.

Mheshimiwa Dkt. Raphael Masunga Chegeni, Mbunge wa Busega, swali lake litaalizwa kwa niaba na Mheshimiwa William Mganga Ngeleja. (*Makof*)

Na. 79

Kujenga Upya Gati la Nyamikoma

MHE. WILLIAM M. NGELEJA (K.n.y. MHE. DKT. RAPHAEL M. CHEGENI) Aliuliza:-

Kumekuwa na ahadi ya kujenga upya Gati la Nyamikoma – Busega ili kuboresha usafirishaji wa mizigo na mazao ya samaki katika Ziwa Victoria:-

Je, ni lini utengenezaji huo utaanza na kukamilika?

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO Alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Raphael Masunga Chegeni, Mbunge wa Busega, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ujenzi wa Gati la Nyamikoma utaanza mara tu baada ya ramani zitakazotoa taarifa za kijografia (*Geographical Information System - GIS*) kwa bandari na magati katika mwambao wote wa Maziwa Makuu kukamilika na kuthibitika kuwa eneo hilo la Nyamikoma linafaa kujengwa gati. Ramani hizo zinatarajiwa kukamilika Oktoba, 2017.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Serikali inatoa wito kwa Halmashauri ya Wilaya ya Busega kutoa ushirikiano wa kutosha kwa Wataalam wanaoendelea na ukusanyaji wa taarifa za kijiografia.

MHE. WILLIAM M. NGELEJA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Pamoja na majibu mazuri ya Serikali naomba kuongezea maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Moja, kwa kuwa eneo la Nyamikoma kihistoria lilikuwa na gati, gati hilo lilikuwa linatumika kusafirisha marobota ya pamba kuyapeleka Kisumu nchini Kenya, enzi zile wakati kilimo cha pamba kipo juu. Napenda kusikia kauli ya Serikali kama katika mazingira hayo bado kunahitajika utafiti wa kijiografia ambao Mheshimiwa Naibu Waziri ameuzungumza ukilinganisha na maeneo mengine ambako hakuna gati?

Pili, eneo la Nyamikoma linafanana na maeneo mengi ya mwambao wa Kanda ya Ziwa au Maziwa Makuu kama alivyosema Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa mfano, *Magu Ginnery, Nasa Ginnery, Mwabagole Ginnery* pale Misungwi, Sengerema Buyagu *Ginnery* ambako ndiko ninakotoka pamoja na Buchosa – Nyakarilo. Napenda kujua kama katika mpango huo ambao Mheshimiwa Naibu Waziri amesema Oktoba watakamilisha ramani zinazohitajika.

Je, anatoa kauli gani za matumaini kwa wananchi wa maeneo haya ambako pia wanatarajia magati yajengwe ili kuboresha zao la pamba ambapo kwa sasa hivi Serikali imewekeza nguvu nyingi katika kufufua viwanda na hasa viwanda ambavyo vinategemea rasilimali ya hapa nchini? Ahsante sana. (*Makofii*)

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nakubaliana nae kwamba Gati la Nyamikoma lilikuwepo toka zamani, lakini taarifa tunazozikusanya sasa hivi tunataka tupate picha kamili kwa sasa ya maeneo ya magati yote na bandari zote ili hatimae tujue tupange vipi vipaumbele vyetu

katika uendelezaji wa magati na bandari hizo. Kwa hiyo, pamoja na kwamba ilikuwepo na unafahamu kwamba matumizi yake yamepungua sana itaingia katika mpango huo na bahati nzuri kama nilivoyosema katika jibu langu la msingi kwamba kazi hiyo tunatarajia kuikamilisha mwishoni mwa Oktoba, 2017.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa swalii la pili; maeneo yote aliyoyataja yapo katika mpango kabambe wa kupitiwa kuandaa hizo taarifa za *G/S* na baadaye kuja kuamua maeneo gani tuanze, maeneo gani tufuatie katika gati zote na bandari zote kwenye Maziwa yote Makuu; Ziwa Victoria, Ziwa Tanganyika na Ziwa Nyasa, nimhakikishie kwamba wananchi wa maeneo yake na maeneo mengine aliyoyataja tutahakikisha kwamba tunayapitia na tunapata taarifa kamili zitakazotuwezesha kuamua wapi tuanze na wapi tufuatie. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tumefika mwisho wa kipindi cha maswali na majibu. Nitaleta kwenu matangazo yaliyotufikia hapa mezani.

Tangazo la kwanza linahusu wageni; tunao wageni mbalimbali wa Waheshimiwa Wabunge pamoja na wageni ambaao baadhi yao ni wanafunzi waliokuja kutembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo. Karibuni sana wageni wetu. (*Makofii*)

Tangazo la pili ni kwa Waheshimiwa Wabunge wote na linatoka Utawala, linahusu mwaliko wa maadhisho ya sherehe za kutimiza miaka 53 ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar. Kamati ya Maandalizi ya Maadhisho ya Sherehe za Kitaifa imetoa mwaliko kwa Waheshimiwa Wabunge wote wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Wabunge wa Afrika Mashariki, kushiriki kwenye sherehe za kutimiza miaka 53 ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar, tarehe 26 Aprili, 2017. Sherehe hizi zitafanyika katika Uwanja wa Jamhuri Dodoma na mgeni rasmi atakuwa Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, ambaye ni Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. (*Makofii*)

Ofisi ya Bunge itatoa usafiri wa pamoja wa mabasi kwa Wabunge watakaohudhuria kutoka Uwanja wa Mashujaa hadi Uwanja wa Jamhuri na kuwarejesha mara sherehe zitakapomalizika. Aidha, Waheshimiwa Wabunge mtakaoshiriki kwenye sherehe hizo mnaombwa kuorodhesha majina yenu ili kusaidia uratibu wa usafiri na mambo mengineyo muhimu. (*Makofii*)

Tangazo lingine linatoka kwa Mheshimiwa Cecilia Paresso ambaye ni Katibu wa *St. Thomas More*, Bunge. Anawatangazia Waheshimiwa Wabunge Wakristo Wakatoliki kwamba leo, siku ya Jumatano, tarehe 19 Aprili, 2017, kutakuwa na ibada ya misa mara baada ya kuahirishwa Bunge saa saba mchana katika kanisa dogo lililopo ghorofa ya pili, Ukumbi wa Msekwa. Waheshimiwa Wabunge wengine wote mnakaribishwa kushiriki ibada hii takatifu.

Waheshimiwa Wabunge, hayo ndiyo matangazo tuliyonayo kwa siku ya leo. Tunaendelea.

MWONGOZO WA SPIKA

MHE. JUMA S. NKAMIA: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii. Nimesimama kwa Kanuni ya 68(7) na kwa sababu ya muda nadhani sina haja ya kuisoma.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo asubuhi hapa wakati wa kipindi cha maswali na majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki amezungumzia suala la kuwahuisha *diaspora* katika maendeleo ya Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwongozo wangu unasimama katika mazingira yafuatayo:-

Katika siku za karibuni Jumuiya ya Ulaya na *Arab Maghreb* zimekuwa zikiimarisha uhusiano na nchi za Afrika na maeneo mengine ya dunia, lakini kumekuwa na matukio ya kutisha hasa katika nchi za Kiarabu ambako baadhi ya

Watanzania wamekuwa wakipigwa hasa wasichana na wanawake, wakinyanyaswa na wengine wakiuawa na hata Kenya kwa mfano, limetokea tukio pia kule Kisii ambapo mwanamke mmoja ameuawa aliyejikuwa anafanya kazi katika nchi za Kiarabu, hata katika Jimbo ya Chemba na Kondoa wasichana wawili wameuawa tayari wamerudishwa na wamekuja kuzikwa huku nyumbani.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwongozo wangu ni kwamba naomba Serikali kama inawahusisha Mabalozi katika kuleta wawekezaji hasa Watanzania wa *diaspora*, je, hawa Watanzania wanaonyanyaswa na kuteswa katika nchi za Kiarabu, naamini na wao pia wako *diaspora*, pengine Serikali ije na tamko, inachukua hatua gani kuhakikisha kwamba hawa Watanzania walioko nchi hizi, matukio ya kunyanyaswa, kupigwa na wengine kuuawa, Serikali inasemaje juu ya hili? (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mwongozo wangu unasimama hapo kwamba nikuombe Serikali ije na tamko inachukua hatua gani, hawa Mabalozi kwa mfano Balozi wa Tanzania aliyeo nchini Oman ambako Watanzania wengi wamekwenda kufanya kazi wananyanyaswa na kuteswa kwa kiwango kikubwa sana. Nikuhakikishie tu, mimi ni mionganini mwa watu ambao tumetoa michango kuhakikisha tunasafirisha maiti za Watanzania waliouawa huko, lakini Serikali hasa Wizara ya Mambo ya Nje imekuwa kimya kabisa kuhusu jambo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba mwongozo wako kuhusu jambo hili. Ahsante sana. (*Makof!*)

NAIBU SPIKA: Nadhani mpeane nafasi kidogo ya kuwashaa *microphone* kwa sababu sasa *mic* zingine zinakuwa haziwaki. Mheshimiwa Mchengerwa.

MHE. MOHAMED O. MCHENGERWA: Mheshimiwa Naibu Spika, nasimama kwa mujibu wa Kanuni ya 68(7) kama ilivyorekebishwa Januari, 2016, kwa manufaa ya muda sitaisoma. Pia nasimama kwa ajili ya umma wa wana Rufiji

kwa mujibu wa ibara ya 63(3)(a) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambayo pia sitaisoma.

Mheshimiwa Naibu Spika, asubuhi niliuliza swalii kuhusiana na wananchi wangu kule kwangu ambao wamekuwa wakiwekewa *beacons* na watu wa Maliasili ambao wamekuwa wakiingia kwenye nyumba zao moja kwa moja na kuweka vifaa mbalimbali kwenye nyumba, hususan katika kata ya Kipugira, maeneo ya Nyaminywili na maeneo mengine na kata ya Ngarambe.

Mheshimiwa Naibu Spika, niliuliza swalii langu hapa ambalo Mheshimiwa Waziri hakulijibu kiufasaha japokuwa maswali mengine aliyajibu kiufasaha vizuri tu, lakini suala hili hakulijibu vizuri na ninaona linaweza likaleta tataruki kwa wananchi wangu kwamba kinachofanywa kinyume na ibara ya 13 ya Katiba na ibara ya 16 ya Katiba kwamba ni haki kwa wale watumishi wa hifadhi kuvamia maeneo ya wananchi na kuweka baadhi ya vifaa vyao kwa wananchi, kwamba ni haki.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba noisome ibara ya 16 (1) kwamba: "Kila mtu anastahili kuheshimiwa na kupata hifadhi kwa nafsi yake, maisha yake binafsi na familia yake na unyumba wake, na pia heshima na hifadhi ya maskani yake na mawasiliano yake ya binafsi."

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaona Mheshimiwa Waziri aliposema kwamba ni haki ya Kikatiba, ninaona haki hii inakinzana na ibara ya 16 ya Katiba, ninamuomba Mheshimiwa Naibu Waziri kama suala hili halifahamu vizuri basi aangalie wakati mwengine wa kulitolea ufanuzi vizuri ili wananchi wasione kwamba kinachofanywa kinyume na Katiba ni haki ya msingi na tunaona kabisa inakinzana na Katiba. Kama ni kanuni au ni sheria ambayo imetungwa, ipo inasimamiwa na Wizara ya Maliasili na Utalii basi watambue kwamba wanakiuka ibara ya 30 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

NAKALA YA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Ninaomba suala hili alitolee ufanuzi ili wananchi wangu, hususan wa kata ya Kipugira na maeneo mengine wawewe kuelewa kinachoendelea. Ahsante. (*Makof!*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Mchengerwa, hebu tusaidie, ni vifaa gani vinawekwa huko majumbani?

MHE. MOHAMED O. MCHENGERWA: Mheshimiwa Naibu Spika, wanasema ni *beacons* lakini ni vifaa haieleweki ni vifaa gani, lakini watu wa maliasili wanavamia kwenye nyumba wanaweka vitu vyao na wamekuwa wakifuatilia mienendo ya wananchi wetu, watu wa maliasili na utalii, ni maeneo mengi ya vijiji hususan kijiji cha Nyaminywili. (*Makof!*)

NAIBU SPIKA: Sawa ahsante. Mheshimiwa

MHE. MARWA R. CHACHA: Chacha Ryoba.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Chacha nimekuona, naenda kwa utaratibu. Mheshimiwa Raphael.

MHE. RAPHAEL J. MICHAEL: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba mwongozo wako kwa Kanuni ya 68(7) ikienda sambamba na Kanuni ya 47(1), sitazisoma lakini nakuomba kwa ridhaa ya Kiti chako kama kuna uwezekano Bunge liahirishwe ili kujadili jambo la dharura.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwa tena na upungufu mkubwa wa sukari katika nchi yetu. Baadhi ya maeneo sasa hivi sukari inauzwa shilingi 2,900 mpaka shilingi 3,000 kwa kilo. Inavyoelekea huu upungufu utaendelea mpaka kipindi hiki cha mvua kishe ndiyo viwanda vyetu vifanyi kazi kikiwemo Kiwanda cha *TPC*. Nalionna kama ni jambo la dhahura linalohitaji mjadala wa Bunge kwa sababu tayari hali ya wananchi inaendelea kuwa ngumu ukizingatia pia kwamba kuna shida ya tatizo la chakula nchini na mfumuko wa bei unazidi kupanda. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba mwongozo wako katika hili ili ikikupendeza Bunge liahirishe

shughuli zake lijadili jambo hili kama jambo la dharura ili kupata mjadala wa Bunge na tamko la Serikali katika hoja hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja.

(Hapa baadhi ya Wabunge walisimama kuunga mkono hoja ya Mhe. Raphael J. Michael)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, naomba tukae. Mheshimiwa Chacha Ryoba.

MHE. MARWA R. CHACHA: Mheshimiwa Naibu Spika, nasimama kwa mujibu wa Kanuni ya 69(1), hoja ya kuahirisha mjadala. Kanuni hiyo inasema; "Mbunge anayependa mjadala unaondelea juu ya hoja yoyote uahirishwe hadi wakati wa baadaye, anaweza kutoa hoja kwamba mjadala sasa uahirishwe na atataja mjadala huo uahirishwe hadi wakati gani na pia atalazimika kutoa sababu kwa nini anataka mjadala uahirishwe."

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Jimbo langu la Serengeti hali ya njaa inatisha. Wilaya ya Serengeti ni tofauti kidogo na Wilaya zingine, Wilaya ya Serengeti, Bunda na Tarime kwa sasa hali ya chakula ni mbaya sana. Sasa hivi debe la mahindi ni shilingi 25,000 hadi shilingi 30,000, tangu nizaliwe haijawahi kutokea. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kibaya zaidi hali hii ya njaa katika Wilaya yetu hii imesababishwa na tembo. Kila wananchi wanapajaribu kulima, mazao yanapokuwa yamefikia wakati wa kuvunwa yote yanaliwa na tembo. Jambo hili nimeliongea kwenye Kamati ya Kilimo, nimemwambia Waziri, kimsingi nimeiambia Serikali lakini sijapata majibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, juzi kwenye Jimbo langu kuna watu watatu wamefariki, mama na watoto wawili kwa sababu ya kukosa chakula wakaamua kutumia mihogo michanga, wamekufa wote. Hali ni mbaya (*worse*).

NAKALA YA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi watu wa Serengeti hatuhitaji mahindi ya bure, tunataka mahindi ya Serikali ambayo yataenda ku-*lower price* kule. Tumeenda Shinyanga kwenye ghala la Serikali tumekuta mahindi yako pale yanaoza. Sasa tunahitaji mahindi haya yaende maeneo ya Serengeti kupunguza mfumuko wa bei ya mahindi pale. Ni lini mahindi ambayo yako kwenye maghala yatatumika kama siyo wakati huu wa njaa, wakati wa hali ngumu? (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kwa mujibu wa Kanuni hii, naomba kuahirisha hoja ili tujadili suala la njaa. Katika nchi hii suala la njaa ni kubwa na hususani Wilaya ya Serengeti.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofii*)

(Hapa baadhi ya Wabunge walismama kuunga mkono hoja ya Mhe. Marwa R. Chacha)

NAIBU SPIKA: Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, naomba tukae. Mheshimiwa Mussa ulikuwa umesimama ama umeridhika?

MHE. MUSSA B. MBAROUK: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kuniona. Nimesimama kwa Kanuni ya 68(7), sitaisoma kwa kuokoa muda.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo katika kipindi cha Maswali na Majibu wakati Naibu Waziri wa Fedha, Mheshimiwa dkt. Ashatu Kijaji akijibu maswali ya nyongeza alipoulizwa na Mheshimiwa Susan Lyimo kwenye swali namba 73 alisema kuwa katika suala la Jumuiya ya Afrika Mashariki, kuna Tume inazunguka mikoani kuhakiki wale watu wanaodai. Vilevile pia alieleza kwamba wanaodai wafuatilie lakini hakueleza wafuatilie wapi, Wizarani au wapi? Kama ni wafanyakazi wa Posta, Bandari au Railway wafuatilie katika maeneo yao ya kazi au wapi?

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini mimi niseme wazee hawa wanahangaika juu ya haki zao. Cha kushangaza hizi fedha zimekuja tangu mwaka 1977, wenzetu tuliokuwa nao katika Jumuia ya Afrika Mashariki, Kenya na Uganda walikwishalipa na Serikali zao hazidaiwi. Najuliza Tanzania kuna nini mpaka leo wazee wengine wanakufa na vihoro, hawalipwi fedha zao. *Na-declare interest* kwamba mzee wangu ni mmoja wa watu waliothirika na madai haya ya Afrika Mashariki. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile ukirudi nyuma kuna aliyekuwa Waziri wa Fedha, Mama Zakhia Meghji aliyehi kusema kwamba mtandao waiba mabilioni na taarifa hii ilitoka katika Gazeti la Jumatatu, tarehe 13 Agosti, 2007. Siishii hapo, hata katika Gazeti la Mtanzania la tarehe 02 Septemba, 2008 aliyekuwa Waziri Mkuu, Mheshimiwa Cleopa David Msuya alizungumza kwenye vyombo vya habari kwamba Serikali imedhulumu fedha za wastaifu wa *East Africa*, ushahidi huu hapo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka Waziri atueleze, kwanza, wanaodai wafuatilie wapi wakati wamefuatilia miaka nenda miaka rudi? Pili, je, hakuna mpango kama huu uliosemwa na Mheshimiwa David Cleopa Msuya aliyekuwa Waziri Mkuu wa Tanzania kwamba Serikali ina mpango wa kuwadhulumu hawa wazee wetu fedha zao za Jumiya ya Afrika Mashariki? (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine niombe mwongozo wako, wakati Mheshimiwa Mchengerwa akiuliza swali la nyongeza asubuhi, alitoa pole kwa wananchi wake wa Kijiji cha Nambunju, kata ya Mbwala, Wilaya ya Rufiji, Mkoa wa Pwani kwamba usiku wa kuamkia leo, kuna Mwenyekiti wa Kijiji anaitwa Charles Mbonde ametaka kuuawa na majambazi hayo hayo maeneo ambayo wameuliwa askari wetu nane. Jana tulipewa taarifa na Mheshimiwa Spika kwamba jambo hili mpaka lifike kwenye Kamati na Kamati itakapojadili ndiyo liletwe hapa lakini majambazi hawasubiri vikao vya Bunge, wala hawasubiri vikao vya Kamati. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kama siyo kuwa na mbio huyu Mwenyekiti Charles Mbonde saa hizi ingekuwa watu wanaandaa mazishi. Nataka unipe mwongozo wako, inakuwaje vikosi vyetu vya ulinzi na usalama vimesambaa huko na kuweka kambi lakini bado wananchi wetu wanataka kuuawa? (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba mwongozo wako. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, Wabunge kadhaa leo wameomba miongozo kwa maana ya kwamba wao waonavyo Kanuni ya 68(7) kuna mambo yalifanyika humu Bungeni ambayo yako kinyume na utaratibu. Kanuni hii ni ya muhimu sana kwetu sote japokuwa Wabunge huwa tunajaribu kutunza muda kwa kutokuisoma Kanuni hii na kutoa maelezo chini ya Kanuni hii.

Waheshimiwa Wabunge, ili wote tuende sawasawa kwa hii miongozo nitakayoitao, nitawosomea hiyo Kanuni ya 68(7) inasemaje; "Hali kadhalika, Mbunge anaweza kusimama wakati wowote ambapo hakuna Mbunge mwingine anayesema na kuomba Mwongozo wa Spika kuhusu jambo ambalo limetokea Bungeni mapema, ili Spika atoe ufanuzi kama jambo hilo linaruhusiwa au haliruhusiwi kwa mujibu wa Kanuni na taratibu za Bunge na majibu ya Spika yatatolewa papo hapo au baadaye, kadri atakavyoona inafaa."

Waheshimiwa Wabunge, tukumbushane tu, unaposimama kuomba mwongozo ni kwa ajili ya kuonesha namna ambavyo kuna jambo humu ndani limefanyika unataka kujua, je, linaruhusiwa au haliruhusiwi, ndiyo Kanuni yetu hii ya 68(7) inavyosema.

Waheshimiwa Wabunge, nimeombwa mwongozo na Mheshimiwa Nkamia, ameitaja Kanuni ya 68(7) ambayo nimeshaisoma na ameenda kwenye majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki akaonesha uhusiano wa majibu yaliyotolewa na

Naibu Waziri na namna ambavyo nchi nyingine pia zinazo utaratibu kama huo wa kuwajali watu wake walio nje ambao wanaitwa *diaspora*.

Mheshimiwa Nkamia akataka kuelewa, je, wasichana ambao taarifa zao zimekuwa zikizunguka kwamba walienda kufanya kazi katika nchi za Kiarabu, sitataka kuzirudia nchi hizo alizozitaja Mheshimiwa Nkamia kwa sababu binafsi sina ushahidi huo, lakini amezitaja nchi kwa mifano kwamba wako wasichana ama binti zetu walioenda kufanya kazi huko kwenye nchi hizo wakapata tabu. Amesema pia wako wengine walitoka Kenya na wamerudishwa wakiwa wameshafariki na ametoa maelezo marefu kuhusu matukio ya kuteswa, kunyanyaswa, kupigwa na hata kuuawa.

Sasa Mheshimiwa Nkamia aksauliza, je, hawa wasichana kama ambavyo Wizara inasema inafuatilia *diaspora* ili waweze kusaidia kuleta maendeleo, hawa hawawezi kuhesabika kama na wao ni *diaspora* ili Wizara pamoja na Mabalozi pia washughulike na hawa watu wetu wanaoenda kufanya kazi huko?

Mheshimiwa Nkamia mwongozo wake haukuwa kuonesha kwamba pengine swali lilijibowi labda kwa namna tofauti ama kwamba kuna jambo ambalo katika kujibu maswali hayo kuonesha kwamba hili alilolisema Naibu Waziri linaruhusiwa humu ndani ama haliruhusiwi, nimewasomea hii kanuni hapa iko wazi.

Waheshimiwa Wabunge, niseme wazi kwamba mambo kama haya tunapotaja nchi na watu kuuawa huko ni lazima sisi tuijweke katika mazingira ambayo kama chombo kikubwa sana kama Bunge tusizitoe taarifa humu zitakazotupa taabu ya mahusiano yetu na hizo nchi. Labda kama mtu analo jambo mahsusila mtu liliyempata na ana uhakika mtu huyo aliyeuawa, nchi yetu inao utaratibu, sheria zipo kwa ajili ya kufauatilia mambo kama hayo. Hata mtu mwingine anaweza kuwa ameuawa Tanzania lakini ukisema mtu ameuawa maana yake utararibu mwingine uchukuliwe. Haiwezekani nchi ya huko nje ambayo sisi tuna mahusiano

nayo ya kupeleka wafanyakazi, mtu akauawa halafu wao wakamrudisha tu. Kwa hiyo, ni lazima tuwe tumejiridhisha na hizi taarifa ili tusije tukaleta mkanganyiko kati yetu na hizo nchi tunazohusiana nazo.

Waheshimiwa Wabunge, sasa nitoe ushauri wa jumla kwa Mheshimiwa Nkamia kwa sababu ameonyesha kwamba hata Jimboni kwake wako watu wanaoenda kufanya kazi huko, wapitie vyombo vilivyowekwa na Serikali kwa ajili ya kupeleka watu kwenda kufanya kazi nje na hivi vyombo viro. Kama kuna Mbunge havifahamu viro, kuna *Tanzania Employment Services Agency*na hii ndio inayotakiwa kuingia mkatuba na hiyo nchi, kufuatilia huyo mtu anakwenda kufanya kazi wapi na kitu kama hicho. Kwa hiyo, hata anaporudishwa, wao watajua amerudishwa katika mazingira gani lakini sasa kama watu walikubaliana majumbani namna ya kuondoka hawa watu, sisi Wabunge tuwasaidle wasitumie utaratibu ambao Serikali inakuwa hajui. Kwa hiyo, niwaombe tusilete hapa taarifa zitakazotuingiza katika mgogoro.

Waheshimiwa Wabunge, nimeombwa mwongozo mwingine na Mheshimiwa Mchengerwa aliyeonesha kwamba Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii alipokuwa anajibu swali lake hakuweka msisitizo ama hakulijibu swali hilo kipengele kilichohusu kuvunjwa kwa ibara ya 16 ya Katiba kwa sababu wako wananchi ambao wamekekewa hicho walichokiita yeche vifaa kwamba vimewekwa nyumbani kwao. Nilipomuuiliza ni vifaa gani akatoa maelezo kwamba ni vifaa vile vinavyowekwa kama mpaka kati ya ardhi ambayo inamiliikiwa na mtu binafsi ama vijiji na mpaka wa hifadhi. Akaonesha kwamba mipaka ya hifadhi iko mingine ambayo imewekwa majumbani kwa watu na jambo hili anasema Waziri hakuwa ameliwekea uzito.

Waheshimiwa Wabunge, yeche ameomba mwongozo wangu kuhusu sauala hili. Kwa hili ni lazima nikaangalie swali liliulizwa vipi na Waziri alijibu vipi. Kwa hivyo, kwa mujibu wa Kanuni yetu ya 68(7) tutaangalia swali liliulizwa vipi na majibu yalitoka vipi halafu tutatoa mwongozo kama kanuni zetu

zinavyosema kama swali litakuwa halikujibiwa kikamilifu basi tutatoa maelekezo hayo ya kulijibu swali kikamilifu.

Waheshimiwa Wabunge, pia nimeombwa mwongozo na Mheshimiwa Raphael ambaye ametumia Kanuni ya 68(7) lakini pia akataja Kanuni ya 47(1) kwamba zote hizi zisomwe kwa pamoja. Kanuni ya 47 inahusu Bunge kutaka kujadili jambo la dharura na ametoa maelezo kwamba jambo hilo la dharura linahusu upungufu wa sukari na kwamba kwa sasa bei imezidi shilingi 3,000 maeneo kadhaa, ametoa mifano ya maeneo, kwa hivyo, akasema bei ni kubwa na yeye angependa Bunge lijadili jambo hilo.

Waheshimiwa Wabunge, taarifa za kupanda kwa sukari Kiti ndiyo kinazisikia kutoka kwa Mheshimiwa Raphael. Kwa sababu hizo hakuna namna ya Bunge kuanza kujadili jambo hilo sasa maana hizo taarifa hatunazo. Kwa hiyo, hata kama tunataka kujadili, tunajadili kwa taarifa zipi? Kwa hiyo, Kanuni ya 47(4) Mheshimiwa Raphael hatutaweza kulijadili jambo hilo na ndiyo maana nikawaambia Waheshimiwa Wabunge wakae japokuwa walismama kuonesha kuunga mkono hoja.

Waheshimiwa Wabunge, nimeombwa pia siyo mwongozo lakini Mheshimiwa Marwa Chacha Ryoba kwa kutumia Kanuni ya 69(1) ameomba Bunge liahirishe shughuli zake ili liweze kujadili jambo ambalo yeye amelitaja hapo na sababu zake pia amezitaja. Ameeleza kwamba hali ya njaa Jimboni kwake Serengeti ni mbaya na inatisha na anasema bei ya debe la mahindi ni kati ya shilingi 25,000 na shilingi 30,000. Anasema sababu ya hili hiyo ni kutoptera na tembo kula mazao ya wananchi. Ametueleza hapa kwamba kuna mama huko na watoto wawili wamefariki kwa kula mihogo ambayo pengine ilikuwa na sumu.

Mheshimiwa Chacha anasema walipozunguka walikuta mahali mahindi yanaoza lakini hayo yangeweza kutolewa kwa wananchi ili waweze kupunguziwa bei. Waziri wa Kilimo yuko hapa na siku za nyuma Bunge hili lilihakikishiwa kwamba chakula kipo cha kutosha.

Mheshimiwa Waziri wa Kilimo umemsikia Mbunge wa Serengeti akikueleza kwamba kule kwake mahindi yako bei juu lakini pia kuna hao watu ambao wamefariki kwa yeye kwa taarifa zake ni kwamba wamefariki kwa kula mihogo lakini hatujui wamefariki kwa sababu zipi. Sasa kwa kuwa uko hapa, tafadhalii hilo jambo lifuatiliwe na vyombo vinavyohusika tupate taarifa na hayo mahindi yapelekwe huko kuliko huko yanakooza kwenye hayo maghala kama alivyotoa maelezo Mheshimiwa Ryoba. (*Makofii*)

Waheshimiwa Wabunge, nimeombwa pia mwongozo na Mheshimiwa Mussa kwa mujibu wa Kanuni ya 68(7). Mheshimiwa Mussa anasema wakati Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha na Mipango akijibu swalii liliohusu mafao ya watu ambao walikuwa wanafanya kazi kwenye hoteli ya *Seventy Seven*- Arusha alijibu swalii la nyongeza la Mheshimiwa Susan Lyimo kuonesha kwamba malipo ya wastaa fu waliokuwa wanafanyakazi *East African Community* ile iliyovunjika yalishalipwa na kwamba kama kuna mtu anadai chochote na anavyo vielelezo aende akafuatilie.

Mheshimiwa Mussa akataka kujua hawa watu wakafuatilie wapi, kwa sababu kwa maelezo yake hawa watu ama hawa wazee wamefuatilia sana maeneo mbalimbali ambayo wao walidhani kwamba wanaweza kufuatilia. Pia kwa vyombo vyaya habari ambavyo yeye amevinukuu, kuna mahali ameonesha kwamba Serikali imedhulumu ama vyombo hivyo vilitoa taarifa kwamba Serikali imedhulumu fedha za wazee hao wakati upande wa Serikali unasema umemaliza kulipa. Yeye alikuwa na mambo kadhaa, hili ni la kwanza halafu aliomba na mwongozo kwenye jambo lingine.

Waheshimiwa Wabunge, sasa hili la wanaodai wafuatilie wapi, kwa sababu hawa wafanyakazi ama hawa wastaa fu hawapo eneo moja wametawanyika nchi nzima, nitamtaka Mheshimiwa Naibu Waziri uniletee hapa taarifa nitampa Mheshimiwa Mbunge wafuatilie wapi, kwa sababu wametawanyika nchi nzima hakuna sehemu moja ambayo utawaambia waende pale. Ukiwaambia wote waende Dar

es Salaam inaweza ikawa ngumu kidogo. Kwa hiyo, nisaidie hiyo taarifa mimi nitampa Mheshimiwa Mbunge na nitawasomea na wengine ambao wanao hao wastaa fu wajue wapi pa kwenda kufuatilia. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mussa pia ameomba kuhusu swalii illokuwa ameuliza Mheshimiwa Mchengerwa kuhusu Mwenyekiti wa Kijiji ambaye jana usiku alinusurika kuuwawa na majambazi na kwamba aliweza kukimbia ndio nusura yake. Mheshimiwa Mussa wakati akitoa maelezo haya ametukumbusha kwamba Mheshimiwa Spika alikuwa ameshatoa maelezo kwamba jambo hili linafanyiwa kazi na vyombo vy ya Serikali vimetawanyika huko kwa ajili ya kazi hiyo na kwamba mauaji ya hawa watu hayasubiri vikao vy Kamati wala hivyo vikosi, sasa kama hivyo vikosi viko kule huyu mzee kwa nini alikuwa katika mazingira haya.

Waheshimiwa Wabunge, kwenye jambo hili pamoja na kwamba Mheshimiwa Mchengerwa ameliuliza na lilipata majibu hayo, kwa sababu tulipewa hapa kauli ya Serikali na Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi yupo hapa kwamba wanayafanya kazi mambo haya na vikosi viro huko tayari, naomba Mheshimiwa Mchengerwa awape hawa watu taarifa za huyo mtu ili waweze kufuatilia vizuri zaidi, kwa sababu Mheshimiwa Mchengerwa amepewa hiso taarifa kwamba ni majambazi wameingia na walitaka kumuua huyo mtu, lakini sisi kama Bunge hatuna utaalam huo.

Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi nadhani umesikia, kwa hiyo, ulifuatilie hilo jambo tafadhali ili huyu mzee ambaye ametumia uwezo wake wa kukimbia aweze kuishi maisha ambayo si ya hofu huko Rufiji.

Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo, nitapata taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha halafu nitawasomea. Mheshimiwa Waziri wa Kilimo ameshapewa maelekezo kwa hiyo tutaendelea. Katibu.

NDG. RAMADHANI ISSA ABDALLAH - KATIBU MEZANI:

HOJA ZA SERIKALI

**Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali
kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018 - Ofisi ya Rais, Tawala za
Mikoa na Serikali za Mitaa na Ofisi ya Rais, Menejimenti
ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora**

(Majadiliano yanaendelea)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, wakati Mheshimiwa Spika akiahirisha shughuli za Bunge jana aliwataja Waheshimiwa Wabunge wawili, kwa hiyo, tutaanza na hao Waheshimiwa Wabunge wawili halafu tutataja wengine kadri tunavyoendelea. Mheshimiwa Juliana Shonza, Mheshimiwa George Lubeleje watafuatiwa na Mheshimiwa Alhaj Abdallah Bulembo.

MHE. JULIANA D. SHONZA: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii na mimi niweze kuchangia katika bajeti hii ya TAMISEMI. Awali ya yote nichukue nafasi hii kumpongeza Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI pamoja na Naibu wake kwa kazi kubwa na nzuri ambayo wanafanya kwenye Taifa letu. Niseme kwamba walikuja kwenye Mkoa wangu wa Songwe na hakika wameacha alama ambayo haiwezi kufutika. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, moja kwa moja naomba nielekeza mchango wangu katika kuchangia masuala ya elimu. Nichukue nafasi hii kuishukuru sana Serikali ya Chama cha Mapinduzi chini ya Rais wake Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli kwa kuweza kusimamia vizuri Sheria ya Haki ya Mtoto ya mwaka 2009 inayohusu haki ya mtoto kupata elimu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, matokeo yake yamekuwa ni makubwa kwa sababu tumeshuhudia kuititia llani ya Chama cha Mapinduzi idadi ya wanafunzi ambao wameandikishwa darasa la kwanza mpaka kidato cha nne

imekuwa ikiongezeka mwaka hadi mwaka. Ukitumba hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI amesema kwamba katika mwaka huu 2017 zaidi ya wanafunzi 300,000 wamedahiliwa ukilinganisha na idadi ya wanafunzi ambayo walidahiliwa kwa mwaka jana.

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme kwamba haya ni mafanikio makubwa sana kwa Serikali hii kwa sababu unaweza kujiuliza kwamba endapo hawa watoto wasingepata hiyo haki yao ya msingi ya kupata elimu bure wangekuwa wapi. Sera hii imesaidia sana kwani vilevile imepunguza matabaka katika jamii yetu kwamba kwa sasa hivi mzazi ambaye hana uwezo na mwenye uwezo watoto wao wanakuwa na haki ya kupata elimu, lakini vilevile imepunguza mimba za utotonii hususani kwa mabinti. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi binafsi huwa nashangaa sana napoona Mbunge katika Bunge hili anasimama na kuponda Serikali ya Chama cha Mapinduzi kwamba imeshindwa kusimamia elimu bure. Hilo jambo si kweli na uzuri ukiangalia hao watu ambao kila siku wamekuwa ni watu wa kuponda wao wenyewe mpaka leo hii wameshindwa kujenga jengo moja la makao makuu. (*Makof/Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ni jambo la kusitisha sana, kama umeshindwa kujenga Ofisi ya Makao Makuu utaweza kutoa elimu bure? Ni kitu ambacho hakiwezekani. Kwa hiyo, niseme kwamba Wabunge tujifunze kusimamia ukweli na tujifunze kusifia pale ambapo Serikali inafanya vizuri. Vilevile tujifunze kushukuru hata kwa kidogo ambacho Serikali ya Chama cha Mapinduzi imekuwa ikifanya. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kama hiyo haitoshi mimi kama Mbunge nilitegemea mtu anapokuja kuponda Serikali ya Chama cha Mapinduzi kuona hata kwenye zile Halmashauri ambazo wao wanaziongoza wangefanya vizuri, lakini matokeo yake sioni jipya lolote kwenye hizo Halmashauri. Hata ukiangalia kwenye suala la madawati, wamesubiri mpaka Serikali ya Chama cha Mapinduzi imefikiria

namna gani ya kuweza kuhakikisha kwamba wanafunzi wa nchi hii wanapata madawati. Ni vema Watanzania wakaelewa kwamba hizi ni porojo tu ambazo tumeshazizoea. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema haya naomba nielekeze mchango wangu kwa masuala mbalimbali ya elimu na wote tunafahamu kwamba kinachosababisha mwanafunzi akafeli ni mazingira magumu ya mwalimu na wala sio mazingira magumu ya mwanafunzi. Nasema hivyo kwa sababu kama mwalimu akirekebishiwa mazingira yake na akipewa motisha ya kutosha mwanafunzi hata kama anatoka kwenye mazingira magumu lakini akikutana na mwalimu ambaye ameandaliwa vizuri ni rahisi sana kwa mwanafunzi huyo kufanya vizuri. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hilo limejldhahirisha hata katika hotuba hii ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais – TAMISEMI, ukurasa wa 31 ambapo amezunguzia motisha kwa Walimu Wakuu wa Shule na Waratibu Elimu Kata. Hotuba hii imesema kwamba katika mwaka wa fedha 2016 kuanzia Julai mpaka Machi, 2017, Serikali imeanza kupeleka fedha kwa ajili ya kutoa motisha kwa Walimu Wakuu wa Shule. Mpaka sasa Serikali imepeleka shilingi bilioni 25.7 kwa Walimu Wakuu wa Shule za Msingi lakini imepeleka shilingi bilioni 7.20 kwa ajili ya walimu wa sekondari lakini imepeleka shilingi bilioni 7.79 kwa ajili ya Waratibu wa Elimu Kata.

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme kwamba huu ni mwanzo mzuri wa kuhakikisha kwamba tunaboresha viwango vyetu vya elimu. Hata hivyo, kwa utaratibu huo, ni kwamba sasa kila Mwalimu Mkuu wa Shule ya Sekondari anapata kiasi cha shilingi 250,000 kwa kila mwezi lakini vilevile Mratibu pia anapata shikingi 250,000 na Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi anapata motisha ya shilingi 200,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, haya ni mafanikio makubwa, lakini nataka kushauri machache. Nimejaribu kusoma sana hiyo hotuba ya TAMISEMI lakini sijaona mahali ambapo Serikali imezungumzia kuwapa motisha wale walimu

ambao ni wa hali ya chini, walimu ambao ni wa kawaida. Sote tunafahamu kwamba unapozungumzia Idara ya Mwalimu Mkuu, Mwalimu Mkuu ni taasisi. Unapozungumzia Mwalimu Mkuu, unazungumzia mwalimu wa taaluma, mwalimu wa nidhamu, mwalimu wa michezo pamoja na mambo mengine. Serikali kupeleka fedha hizi moja kwa moja kwa Mwalimu Mkuu peke yake, mimi kama Mbunge limenipa shida kidogo. Ni vema Serikali ikaangalia namna nzuri ambayo inaweza kuhakikisha kwamba hata wale walimu wengine wa masomo ya kawaida wanapata hii motisha ya Serikali. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, wote tunatambua kwamba Walimu Wakuu hawa ndiyo ambao hata semina mbalimbali ambazo huwa zinafanyika zinawalenga wao moja kwa moja. Waratibu wa shule, semina hizi zinawalenga moja kwa moja. Hata ukija kwenye masuala ya nyumba za walimu, wanufaika wa kwanza ni hao Walimu Wakuu wa Shule, lakini wale walimu ambao wanafundisha masomo ya kawaida, walimu ambao kimsingi wao ndiyo wanabeba jukumu kubwa la kuhakikisha wanaboresha mifumo ya elimu, ndiyo wanaohangaika na wanafunzi asubuhi mpaka jioni, naona kama Serikali imewasahau kidogo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutoa ushauri wangu kwa Serikali kwamba iweze kuangalia suala hili. Afadhalii hii fedha ikapelekwa katika shughuli za uendeshaji wa ofisi. Kwa kupeleka fedha hiyo kwenye uendeshaji walimu wote wataweza kunufaika. Vilevile tunatambua kwamba walimu wana changamoto ambazo zinafanana, fedha hii ikipelekwa katika shughuli za ofisi naamini kwamba walimu wote pamoja na Walimu Wakuu wataweza kunufaika.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wangu ulikuwa ni huo, nashukuru sana.

TAARIFA

MHE. GOODLUCK A. MLINGA: Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa.

MHE. JULIANA D. SHONZA: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Mheshimiwa Simbachawene atakapokuja kutoa maelezo aniambie ni kitu gani ambacho wao wamekitumia katika kuona kwamba motisha hii ipelekwe kwa Walimu Wakuu wa shule peke yao.

MHE. GOODLUCK A. MLINGA: Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Shonza naomba ukae kidogo.

MHE: GOODLUCK A. MLINGA: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kumpa taarifa Mbunge aliozungumza. Hao aliosema wameshindwa kujenga ofisi, pamoja na Tanzania hii kuwa na mapori mengi lakini hata kiwanja kimoja hawamiliki. Kwa hiyo, siyo tu wameshindwa kujenga ofisi tu hata kiwanja hawana. (*Makofii/Kicheko*)

MHE. JULIANA D. SHONZA: Mheshimiwa Naibu Spika, nimepokea hiyo taarifa kwa sababu ni taarifa ambayo ni ya kweli na ndiyo uhalisia wa mambo.

MHE. HALIMA J. MDEE: Mheshimiwa Naibu Spika, Kuhusu Utaratibu.

MHE. JULIANA D. SHONZA: Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Shonza, muda wako umekwisha, lakini Mheshimiwa Mlinga, Mheshimiwa Shonza muda wake ulikuwa umekwisha taarifa inabidi itolewe mtu akiwa bado anazungumza ili aipate vizuri.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea, nilimtaja Mheshimiwa George Lubeleje atafuatiwa na Mheshimiwa Abdallah Bulembo na Mheshimiwa Murad Saddiq ajiandae.

MHE. GEORGE M. LUBELEJE: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili nami nichangie hoja hizi

NAKALA YA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

mbili za Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI na Utumishi. Kwanza niwapongeze sana Mawaziri hawa wawili, Makatibu Wakuu, Naibu Makatibu Wakuu na Watendaji wote wa Wizara hizi kwa kazi nzuri walizofanya katika mazingira magumu sana ya upungufu wa ufinyu wa bajeti. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, TAMISEMI ni chombo kikubwa sana na TAMISEMI inatakiwa ipewe bajeti ya kutosha pamoja na Utumishi kwa sababu idara zote zipo TAMISEMI, ukitaka afya – TAMISEMI, maji – TAMISEMI, ujenzi – TAMISEMI. Kwa hiyo, inatakiwa ipate fedha za kutosha ili waweze kutekeleza miradi mbalimbali. Hivi sasa kuna miradi viporo katika majimbo yetu kwa sababu fedha hazipo na zimechelewa kufika TAMISEMI. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili ambalo nataka kuzungumzia ni Jimbo langu la Mpwapwa hasa barabara za Mjini Mpwapwa. Mji wa Mpwapwa ulianzishwa tangu 1905, sasa una zaidi ya miaka 100 lakini hakuna hata barabara moja ambayo ina lami. Kwa hiyo, wakati umefika sasa barabara za Mpwapwa Mjini zote ziwekwe lami ili ziweze kupidika bila wasiwasi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara nyingine ninayotaka kuzungumzia ni barabara kutoka Gulwe - Berege - Chitemo - Mima - Egoji - Sazima mpaka Seruka. Barabara hii ni mbaya sana, Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI anaifahamu, ni barabara mbaya inapitika kwa shida. Tangu mwaka jana nimeomba Serikali itenye fedha kwa ajili ya barabara hii ili ifanyiwe marekebisho makubwa, lakini mpaka sasa hajatengenezwa. Halmashauri ya Wilaya ya Mpwapwa haina uwezo wa kukarabati barabara hii kwa sababu uwezo wao ni mdogo. Naomba sasa TAMISEMI ikabidhi barabara hii *TANROADS* ili iwe chini yake na iweze kufanyiwa matengenezo makubwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ni kuhusu tatizo la maji vijiji vya Mima, Iyoma pamoja na Bumila. Nashukuru sana Serikali imechimba visima vitatu, imechimba kisima vijiji vya Mima, Iyoma pamoja na Bumila. La

kushangaza sasa ni zaidi ya miaka nane visima hivyo havijawekwa pampu, mabomba wala matenki kwa ajili ya kusambaza maji. Naiomba Serikali visima hivyo viwekwe pampu na kusambaza maji katika vijiji hivyo. Wananchi wa maeneo hayo wana shida kubwa sana ya maji. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ninalotaka kuzungumzia ni posho za Madiwani. Madiwani posho wanayopata ni kidogo. Bahati nzuri mimi nimewahi kuwa Diwani na Mwenyekiti wa Halmashauri miaka kumi na tano. Mwaka 2012 TAMISEMI waliunda Tume ya kushughulikia maslahi ya Madiwani na iliongozwa na Mheshimiwa George Malima Lubeleje na ikaitwa Tume ya Lubeleje. Bahati nzuri nilifanya kazi nzuri sana pamoja na wajumbe wangu mpaka Madiwani wakakongezwa posho. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini posho ile waliyoongezewa sasa ni zaidi ya miaka mitano, sita hajaongezwa. Udiwani wa zamani ilikuwa ni vikao tu, lakini Udiwani wa sasa lazima Diwani usimamie miradi. Ikianza kujengwa shule Diwani ushinde pale, ikianza kujengwa zahanati Diwani ushinde pale mpaka jioni na posho yao ni ndogo sana. Kwa hiyo, nashauri waongezewe posho ili waweze kutekeleza majukumu yao. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Madiwani wanaitwa ni *civic leaders*. Kwa nini waitwe *civic leaders*? Maana katika uchaguzi tunakwenda mafiga matatu, Diwani, Mbunge na Rais lakini baada ya uchaguzi hawa Madiwani tunawaweka pembeni, anabaki Mbunge pamoja na Rais. Kwa nini waitwe *civic leaders*? Kuna Sheria ya *Political Leaders Retirement Benefit*, nashauri kama inawezekana sheria hii irekebishiwe ili Madiwani waingizwe katika sheria ile nao wajulikane kama ni viongozi kama sisi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya hawakuwemo kwenye sheria hiyo, walikuwa kama watumishi wa Serikali. Mwaka 1999 nikiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Kudumu ya Katiba, Sheria na Utawala tulirekebisha sheria sasa hivi Mheshimiwa Mkuu wa

NAKALA YA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Mkoa na Mkuu wa Wilaya wapo kwenye sheria hiyo. Kwa hiyo, kazi ya Mkuu wa Mkoaa na Mkuu wa Wilaya ni *contract* ya miaka mitano, akimaliza miaka mitano analipwa mafao yake, basi kama atateuliwa tena na Rais anayekuja ni jambo lingine. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine nimpongeze sana Waziri wa Utumishi ndiye anayesimamia *TASAF* na MKURABITA. Tumetembelea Mikoa kama name kwa ajili ya kuangalia utendaji wa *TASAF*, wanafanya kazi nzuri sana. Kila Halmashauri ya Wilaya ina Mratibu wa *TASAF*, ina mratibu wa MKURABITA, hawa ndio walioandikisha kaya maskini, walijua kabisa wanaandikisha kaya maskini lakini leo nashangaa kusikia kwamba walikosea na kuna wengine kati ya walioandikishwa wana uwezo wanatakiwa warejeshe hizo fedha. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi najuliza mwenye kosa ni nani kati ya aliyeandikisha na kuthibitisha kaya maskini na aliyeandikishwa? Inakuwaje leo unamwambia kwamba hapana wewe una uwezo urejeshe hizi fedha? Naomba Mheshimiwa Waziri kwa kushirikiana na *TASAF* mljadili hili suala, lakini *TASAF* inasaidia kaya maskini kwa sababu watu wanaboresha maisha yao, wanajenga nyumba, wanasomesha watoto na wanapeleka watoto kliniki. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu MKURABITA mradi wa kurasi mishi mali, mashamba yanapimwa na wananchi wanapata hati miliki, wanakwenda kukopa benki. Zamani zile hati milliki zilikuwa hazitambuliwi na vyombo vya fedha lakini nashukuru sana Serikali imeshauri mabenki kama *CRDB*, *NMB* wamekubali wanazitambua hati miliki za kimila. Kwa hiyo, wananchi wanapata mikopo, wanajenga nyumba bora na wanasomesha watoto. Kwa hiyo, naipongeza sana Serikali na nashauri MKURABITA na *TASAF* iendelee.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana, huo ndiyo mchango wangu, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Ahsante Mheshimiwa Alhaj Abdallah Bulembo atafuatiwa na Mheshimiwa Suleiman Saddiq Murad, Mheshimiwa Upendo Furaha Peneza ajiandae.

MHE. ABDALLAH M. BULEMBO: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Awali ya yote, nichukue nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kuniingiza katika jengo hili, lakini pili, nichukue fursa hii kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano, Mheshimiwa Dkt. John Joseph Pombe Magufuli. Tatu, nimpongeze Makamu wa Rais, Mheshimiwa Mama Samia, anawawakilisha wanawake wote hapa, mambo anayoyafanya mnayaona. Nne, nimpongeze Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano, Mheshimiwa Mwalimu Majaliwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika nichukue nafasi hii kuwapongeza TAMISEMI kupitia Waziri wake wa TAMISEMI kwa kazi wanayoifanya. Nimpongeze Naibu Waziri wake kamanda Mheshimiwa Jafo kwa ziara anazopiga. Katibu Mkuu Injinia lyombe, mzee maarufu yuko pale TAMISEMI inasonga mbele. Nirudi kwenye Utawala Bora, nimpongeze Mheshimiwa Angellah kwa kazi anazozifanya na Dkt. Ndumbaro.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi sina ajenda kubwa sana, ninayo mambo kama mawili au matatu. La kwanza kwa nini TAMISEMI inapongezwa. TAMISEMI ndiyo inashughulika na kila Mtanzania TAMISEMI kwa sababu ukienda kule kwenye Serikali ya Mtaa, Mtendaji wa Mtaa, Mtendaji wa Kata, Diwani na Mbunge ni wa TAMISEMI. Tunawapongezeni sana TAMISEMI na tuna haki ya kuwapongeza kwa kazi kubwa wanayoifanya kwa sababu TAMISEMI ndiyo imebeba mzigو wa Watanzania waliokuwa wengi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini namba mbili nihamie Utumishi. Utumishi kwenye kitabu chao wametuonyesha wameweza kugundua watumishi hewa zaidi ya 13,000. Si kazi ndogo, ni kazi ya Chama cha Mapinduzi kuelekeza lazima tuwaondoe mafisadi ndani ya Serikali yetu, tunakupongezeni sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia niwapongeze Utawala Bora kwenye eneo la TAKUKURU. Kwenye taarifa ya juzi ambayo TAKUKURU waliwasilisha kwa Mheshimiwa Rais imeonyesha wameokoa shilingi bilioni 53. Siyo kazi ndogo, ni kazi ya kusifia. Vilevile tayari tumeanzisha Mahakama ya Mafisadi tuwaombe TAKUKURU basi wale mnaookoa zile fedha waende kwenye Mahakama, msikae na mafaili pale mezani ili *impact* ya kuokoa na watu wameenda kufanywa nini ionekana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, elimu sitasema sana, lakini mdogo wangu pale amesema, jana hapa kuna watu wanabeza elimu bure. Tumeenda pale kwenye semina ya TWAVEZA watu wanabeza elimu bure, sielewi, inawezekana hoja ya mpinzani ni kupinga. Kama ilikuwa shule watoto wanaenda 200 leo darasa linaenda watoto 400 kwa sababu elimu ni bure kuna haja gani ya kutoipongeza Serikali hii? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tunatekeleza llani ya Chama cha Mapinduzi tulioiuza kwa wananchi waliokuwa wengi na tukasema elimu itakuwa bure. Leo mwezi mmoja shilingi bilioni 18 zinaenda si kazi ndogo, ni kazi kubwa sana.

MHE. HAMIDU H. BOBALI: Mheshimiwa Spika, Taarifa.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Bulembo, naomba usubiri kidogo, Mheshimiwa Bobali.

MHE. HAMIDU H. BOBALI: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru. Pamoja na kumheshimu sana Mzee wangu Mheshimiwa Bulembo, naomba nimpe taarifa kwamba nchi hii tangu imepata uhuru hajawahi kuongozwa na chama kingine zaidi ya Chama cha Mapinduzi. Kwa hiyo, kama kuna upungufu wa ujisadi na kadhalika anayoeleza yalikuwa ndani ya Chama cha Mapinduzi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba aipokee taarifa hiyo. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Bobali, siyo kwamba chama kingine hakijawahi kupewa hiyo ridhaa na wananchi maana siyo suala la kuongoza tu, ni suala la kupewa ridhaa na wananchi. Mheshimiwa Bulembo, taarifa hiyo unaipokea ama unaikataa? (*Makofi*)

MHE. ABDALLAH M. BULEMBO: Mheshimiwa Naibu Spika, ni taarifa ambayo imeletwa na wale wanaojifunza Chama cha Mapinduzi kinafanya nini. Kwa hiyo, ngoja tuwaunge mkono kwa njia hiyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeisema na nashukuru imetoka kule, wao walikuwa na ajenda wanasema ujisadi, ujisadi lakini kwenye kutafuta kura wao wakakumbatia mafisadi. Nafikiri hiyo kumbukumbu wanayo vizuri tu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba njielekeze kwenye kitabu cha mse maji wa jana wa Kambi ya Upinzani. Wakati anailaumu TAMISEMI kwa kupeleka maombi ya kutaka kujenga *stand* Moshi, sijui Halmashauri gani imetaka nini lakini mwisho akasema, TAMISEMI inakataa kuwaruhusu wasijenge *stand* kwa sababu wao ni wapinzani na akasema inaruhusiwa Morogoro na Tanga. Naomba nimjulishe vizuri ni Diwani mwenzangu huyo, ni mzoefu wa muda mrefu anaelewa taratibu za *Local Government* lakini ukisema Morogoro ni ya CCM, Tanga je? Umesahau una mtu wa hapa wa CUF ni Mbunge wa Tanga Mjini? Umesahau Halmashauri ya Tanga ni ya upinzani? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini unavyokwenda kuomba...

MHE. RAPHAEL J. MICHAEL: Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Raphael, Taarifa.

MHE. RAPHAEL J. MICHAEL: Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Bulembo ni vizuri akajua tunamheshimu sana si

vizuri na ye ye akaanza kuingia kwenye mambo ya mipasho humu Bungeni. (*Makofii*)

WABUNGE FULANI: Aaah!

MHE. RAPHAEL J. MICHAEL: Mheshimiwa Naibu Spika, Tanga imepewa kibali wakati ikiwa ni Halmashauri chini ya Chama cha Mapinduzi.

MBUNGE FULANI: Chuma kimeingia.

MHE. RAPHAEL J. MICHAEL: Halikadhalika Morogoro. Sizungumzii Tanga sasa hivi ikiwa chini ya Madiwani wengi wa UKAWA pamoja ya kwamba Meya wa Tanga anatoka CCM. Kwa hiyo, ni vizuri akaelewa hoja yangu kwamba tusiligawe Taifa hili katika itikadi za kisiasa. Moshi tuna-*qualify* kupewa kibali, tupewe kibali tuendeleze maisha ya wananchi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimpe taarifa Mheshimiwa Bulembo, namheshimu sana. (*Makofii*)

MHE. ABDALLAH M. BULEMBO: Ni kawaida Madiwani wanaheshimiana.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Bulembo, subiri kidogo. Mheshimiwa Raphael, wakati nataka kumuuliza Mheshimiwa Bulembo kuhusu taarifa, umesema kwamba alikuwa anazungumza mipasho, nadhani anachangia kama ambavyo mtu yeyote atachangia. Kama ameenda kinyume na Kanuni wewe unasi mama kuonesha utaratibu, lakini tusiende huko.

MHE. RAPHAEL J. MICHAEL: Mheshimiwa Naibu Spika, natoa neno hilo.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Raphael, naomba ukae tafadhali. Mheshimiwa Bulembo unaipokea hiyo taarifa?

MHE. ABDALLAH M. BULEMBO: Mheshimiwa Naibu Spika, sisi tulikuwa Madiwani zamani hawa nao wakaja vijana, kwa hiyo, Diwani ukimsema lazima itafikia hatua hiyo. Mimi nimesoma kilichoandikwa kwenye kitabu maelezo ya ziada ameyatoa kwenye mdomo wake saa hizi, kwa maana leo Tanga iko chini ya Upinzani na mradi unafanyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini nyongeza unavyoandika mradi kama Diwani katika Halmashauri yenu kwa nini TAMISEMI anapatikana? TAMISEMI ndiyo *guarantor* wa hiyo hela mnayotaka kukopa. Ni sawasawa na unapoandika mradi unaupeleka benki ni lazima Meneja akubali huwezi kumlazimisha. Kwa hiyo, nashauri yale majiji yanayoandika miradi kuomba Serikali iwadhamini, andikeni miradi kwa kujifunza kwa wenzenu ambao wameshapata huduma hiyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nahamia kwenye kitabu cha mama mmoja namheshimu sana. Huyu mama ni Mheshimiwa Mbunge, eeh ni mama kwa sababu hata nikimsema utajua ni mama.

MBUNGE FULANI: Mheshimiwa bwana.

MHE. ABDALLAH M. BULEMBO: Mheshimiwa mama, mama haifutiki. Huyu Msemaji wa Kambi ya Upinzani kwenye Utawala Bora, Mheshimiwa Ruth Mollel, jana amesema hapa kauli nzito kidogo. Akasema Mheshimiwa Rais kwenye uteuzi wake wale wote waliogombea ndani ya CCM wakashindwa ndiyo wamekuwa Wakurugenzi, ma-DC na kadhalika. Swali langu dogo, Mama Mollel tangu amestaafu ni juzi, anataka kutushawishi kwamba aliingiaje CHADEMA, wale aliokuwa anaajiri alikuwa anaajiri Wakurugenzi kwa ajili ya maandalizi ya CHADEMA? Kwa sababu ni mtumishi ambaye amekuwa Serikalini mpaka amestaafu, anaheshima yake, anakula pensheni aliwezaje kutengeneza ajira ya wapinzani wengi na leo siku tano anakuwa Mbunge anatokea ndani ya Chama cha Upinzani? Sasa nasema hivi Rais anayo mamlaka ya kuona nani anamfaa, nani amteue, nani amwakilishe katika Serikali yake anayoiongoza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini nyongeza, heshima anayopewa huyu mama hebu aendelee kuiheshimu pamoja na kuwa yuko upinzani, ana siri nyingi za nchi yetu huyu. Ikiwa ataonekana huko alikotoka alikuwa anaandaa mazingira ya CHADEMA basi tutaangalia sheria zinasema nini. (*Makof/ Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimalizie kwa kusema kwamba hoja zilizopo mbele yetu Tanzania ni moja. Kuna mwenzangu jana wa Kigoma alikuwa anasema barabara yangu, eneo langu la wapinzani, sijui Mheshimiwa nini mwalimu lakini, nataka kuuliza mmaposema maeneo ya wapinzani hayahudumiwi elimu bora kuna mwanafunzi wa CCM na mwanafunzi wa CHADEMA? Mbona wote mnasoma elimu bure, mbona kule hamsemi hayo mazuri.

Ndugu zangu sisi ni Watanzania tukitoka hapo nje tunakunywa chai pamoja, tunapanda magari pamoja tusiitenganishe nchi yetu kwa itikadi zetu. Tutajenga mzizi ambao siku tukija kusema usifanyike gharama yake itakuwa kubwa sana. Tapingane kwa hoja, tushauriane kwa hoja na siku ya mwisho tuwe wamoja kama Watanzania wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja, nakushukuru sana. (*Makof*)

NAIBU SPIKA: Ahsante, Mheshimiwa Suleiman Saddiq Murad atafuatiwa na Mheshimiwa Upendo Furaha Peneza na Mheshimiwa Savelina Mwijage ajiandae.

MHE. SULEIMAN A. SADDIQ: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi asubuhi hii ya leo na mimi naomba nianze kutoa pongezi nyingi na za dhati kabisa kwa Mawaziri wetu, Mheshimiwa Angellah, Mheshimiwa Jafo na Mheshimiwa Simbachawene kwa kazi kubwa na nzuri wanayofanya kulitumikia Taifa letu. Ni Mawaziri wasikivu, wachapakazi na mara nyingi ukipeleka shida zako wanakusikiliza na wanakuelewa. Hongereni na chapeni kazi. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimpongeze sana Mheshimiwa Rais wetu kwa kazi kubwa anayofanya. Mheshimiwa Rais amefanya mambo mengi makubwa, amerejesha nidhamu ya kutumia fedha na nidhamu kwenye ofisi za umma. Mheshimiwa Rais amethubutu kufanya mambo mazito kwenye reli, anga na barabara. Mheshimiwa Rais amethubutu kulipa madeni ya nje na leo Serikali yetu inaanza kuaminika. Tuendelee kumuombea nmwenyezi Mungu ampe afya njema na mwenyezi mungu amuongezee ujasili aweze kulitumikia Taifa letu. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie suala la Mvomero kwa upande wa elimu. Mvomero tuna upungufu wa walimu zaidi ya 200 kwenye shule zetu za msingi. Kabla suaendelea naomba niseme kwamba walimu wa Mvomero walikuwa wanaida Serikali shilingi 137,000,000. Naomba nipongeze Serikali kwa kuleta fedha hizi na sasa hivi walimu wa Mvomero hawadai tena. Hongereni sana Mawaziri, hongera sana Mheshimiwa Rais fedha zimekuja shilingi 137,000,000 na walimu wote wamelipwa. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna upungufu wa walimu kama 200 tunaomba Serikali ituangalie kwa jicho la huruma. Jiografia ya Mvomero imekaa vibaya, ukitoka Mvomero unakwenda mpaka Handeni unapakana na Mkoa wa Tanga na Kiliindi, unarudi mpaka kwenye mbuga za wanyama za Mikumi, unakwenda mpaka na Chuo Kikuu cha Mzumbe na unapanda mpaka kwenye milima ya Mgeta unapakana tena na tarafa nyingine za Morogoro Vijijiini. Jiografia ya Mvomero imekaa vibaya, naomba Waheshimiwa Mawaziri tuangalie ni jinsi gani Mvomero tunaweza kuigawa aidha katika Halmashauri mbili au katika majimbo mawili. Mvomero imekaa vibaya tunatumia muda mwingi sana kutembea kupeleka huduma, naomba Serikali iliangularie hilo. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia katika Wilaya ya Mvomero tuna tarafa nne lakini tuna sekondari mbili za *A-level*. Tunaomba Serikali itusaidie fedha ambazo tumeombia zile tarafa mbili zilizobaki tuweze kupata sekondari za *A-level*. Tarafa za Turiani na Mvomero zinazo shule hizo, lakini tarafa

ya Mgeta haina sekondari za *A-level*, kwa hiyo, naomba viongozi mtusikie katika hili. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie suala la *TASAF* kwa ufupi kabisa. Fedha za *TASAF* zinazokuja katika zoezi la kusaidia kaya maskini zinakwenda muda mbaya. Wataalam wetu wanatoka na fedha benki jioni saa kumi, wanatembea kwa zaidi ya saa mbili/tatu wanafika usiku, wananchi wengine wanakuwa wameshapata vinywaji wamechangamka kunakuwa na vurugu. Naomba Waziri, dada yangu Mheshimiwa Angella uliangalie hilo na utoe maelekezo na waraka kwamba fedha zipelekwe muda wa mchana na muda mzuri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie suala la zahanati na afya. Mheshimiwa Waziri Wilaya ya Mvomero tuna upungufu mkubwa sana wa huduma ya afya. Tumejenga Hospitali ya Wilaya, jengo limekamilika lakini bado umeme. Bajeti ambayo wataalamu wetu waliandaa tunahitaji shilingi 100,000,000 tuweze kuifungua hospitali ile ya Wilaya na fedha hizi tayari tumeziomba. Naomba Mawaziri mnaohusika muweza kutuidhinishia fedha hizo tuweze kufungua Hospitali ya Wilaya ya Mvomero. Nawaombeni sana fedha zilizotumika ni nyingi, idadi ya fedha iliyobakia ni ndogo, tunaomba bajeti ile idhinishwe. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini tuna Hospitali Teule inaitwa Turiani Hospitali. Hospitali ile wananchi ambao wanakwenda kupata huduma pale wanapata huduma kwa gharama kubwa. Hospitali ile haitusaidii chochote wananchi wa Mvomero. Fedha ambazo zinapelekwa bado hazisaidii, wananchi wanatozwa gharama mbalimbali na taratibu hazifuatwi. Huduma wanazopata mama na mtoto bado wanatozwa na sera ya Serikali inasema huduma ya mama na mtoto ni bure. Mheshimiwa Jafo uliniahidhi kwamba tutakwenda pamoja Mvomero, naomba tekeleza ahadi yako, tukimaliza Bunge hili au Jumamosi moja chapa kazi twende zetu ukaone matatizo yaliyopo na uweze kutushauri na kutusaidia. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo naomba niliseme, Wilaya ya Mvomero imebarikiwa ina mito mingi, maji mengi na ardhi nzuri sana. Tuna *green land* kubwa sana Mvomero. Wabunge karibuni, chukueni mashamba mlime. Tatizo letu tunahitaji tusaidiwe na Serikali ili kilimo kile kiwe kilimo cha kisasa tuweze kupata fedha za kutusaidia baadhi ya maeneo tuweze kumwagia zaidi tuweze kuyatumia yale maji vizuri. Fursa kubwa ipo tatizo ni fedha tunazoomba haziletwi kwa wakati na zinakuja fedha ndogo. Naomba sana fedha hizo zije kwa wakati ziweze kutusaidia.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini la mwisho kabisa na naona muda unakwenda, tunaomba sana Idara ya Ujenzi Mvomero inayoshughulikia barabara haina gari kufuatilia miradi ya barabara. Mheshimiwa Jafo tuliongea jambo hili ukaniambia tutakaa chini tutazungumza. Naomba kuitia bajeti ya Wizara yenu, Mvomero jiografia yake imekaa vibaya, tunaomba gari Idara ya Ujenzi tuweze kufuatilia barabara zetu tuweze kuleta maendeleo kwa Mvomero yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsanteni na naunga mkono hoja mia kwa mia. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Upendo Furaha Peneza atafuatiwa na Mheshimiwa Savelina Mwijage na Mheshimiwa Peter Simon Msigwa ajiandae.

MHE. UPENDO F. PENEZA: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kunipatia nafasi hii na namshukuru Mungu ambaye ameniwezesha kufika katika Bunge hili la Bajeti.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijajielekeza moja kwa moja kwenye mambo ya msingi ya kuchangia napenda niongelee suala moja. Hapa kuna miongozo kadhaa iliombwa na uliitolea ufanuzi lakini utaratibu ambao umesema ufuatwe wa watu kwenda kwenye hizo taasisi za ajira nadhani ni vizuri tukatambua kwamba hili suala sana sana linaelekea kwenye mambo ya *human trafficking* ambapo watu hawa wanasafrishwa kwa njia ambazo sio

nzuri. Kwa hiyo, ni vizuri Serikali ikaangalia ni namna gani inawalinda watoto wetu kutokana na hiyo biashara haramu ili pia wasiweze kupatwa na matatizo. Kwa hiyo, suala hili naomba liangaliwe katika muktadha wa *human trafficking*. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Iakini suala lingine ni la mama yangu hapa Mama Mollel ambapo Baba yangu ninayemheshimu amelizungumzia lakini niseme tu mama alijunga na CHADEMA katikati ya uchaguzi. Kwa hiyo, si vizuri kuwadhalilisha viongozi wetu ambao tunawaheshimu katika Bunge letu hili. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa najielekeza katika suala ambalo lipo mbele yetu hapa. Tunafahamu kwamba nchi yetu na viongozi wetu ambao wako hapa wameweza kutueleza kiundani kuhusu masuala ya utawala bora. Hata hivyo, katika masuala ya utawala bora, uwazi na uwajibikaji ni vitu vya msingi sana vya kuweza kuzingatiwa ili kuweza kuupata huo utawala bora.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha nyuma wananchi kwa kiasi kikubwa sana wameshiriki kikamilifu kushirikiana na Wabunge kwa ajili ya kuiwajibisha Serikali. Naongea hivi kwa maana moja kwamba kipindi cha nyuma tulikuwa na *Bunge live* ambapo wananchi wamekuwa wakifuatilia matangazo ya moja kwa moja ya Bunge wakiweza kusikiliza vipindi vinavyoendelea ndani ya Bunge ambapo imewasaidia wao kwanza kuelewa hata sheria zinazopitishwa ndani ya Bunge, kuelewa bajeti ambayo inawagusa moja kwa moja lakini pia kuna mambo mengine ambayo yameweza kuwagusa wananchi moja kwa moja. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Bunge hili upande wa Chama cha Mapinduzi waliunga mkono sana suala la *Bunge live* kuondolewa, Iakini kuna watu ambao ni wanawake ambao ndiyo waathirika wakubwa kwa kuliondola hili suala la *Bunge live*. Jana tumesikiliza jinsi ambavyo idadi ya wanawake imepungua katika Baraza la

Mawaziri, Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya na nafasi mbalimbali za Kiserikali. Kwa hiyo, sisi kama wanawake tuna nafasi ya kwenda kugombea katika majimbo na katika jamii zetu zilizojaa mfumo dume, *Bunge live* limeweza kubadilisha umma na kuona kwamba wanawake wanaweza. Pia kuna mambo ya msingi mengi ambayo wanawake tumeweza kuyainua ndani ya Bunge hili, kuna masuala ya ndoa za utotoni uelewa watu umeweza kubadilika, kuna masuala mbalimbali yanayowagusa mabinti zetu kule nyumbani wananchi wameweza kubadilika taratibu kutokana na kwamba wanasiliza Bunge. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Iakini vilevile kuna ripoti ya TWaweza ya mwaka 2012 inayoonesha kwamba masuala ya ukeketaji yamepungua kwa asilimia 21 na inatokana na mchango wa Bunge. Kwa hiyo, wananchi waliokuwa wakifuatilia Bunge wameweza kubadilika na kuona kwamba kuna haja ya kuweza kupunguza masuala ya ukeketaji na hii inatokana na mchango wa Bunge ndani ya Bunge hili letu Tukufu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, niseme tu kwamba yavezekana ni maagizo tunasingizia kupunguza matumizi ya Serikali kwa masuala ambayo yanaathiri masuala ya kijamii na kijinsia. Kwa hiyo, kama wanawake sasa kuna haja kubwa ya kusimama na kudai hili suala la *Bunge live* kwa sababu linatuathiri. Hata kama hamuwezi kuteuliwa kwenye Baraza la Mawaziri basi tukapata nafasi za uwakilishi kule chini na nina imani wanawake kwa pamoja hebu tufanye mambo ya msingi kwa ajili ya maisha yetu na watoto wetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna suala lingine ambalo napenda kuzungumzia katika masuala ya Serikali za Mtaa na niseme tu namshukuru Naibu Waziri Mheshimiwa Jafo kwa kuweza kufika Geita na kwa kujibu swalilangu ambalo lilikuwa ni kuhusu masuala ya maji na bwawa. Napenda tu pia uje utuambie ni lini sasa hiyo Tume ambayo ulisema itaundwa itaenda kuchunguza ubadhirifu ambao umefanywa katika eneo hilo hapo Geita.

Mheshimiwa Naibu Spika, Iakini kuna suala lingine Waheshimiwa Mawaziri wa TAMISEMI ambalo napenda kulitolea ushauri na pia nimeshalitolea ushauri ndani ya Halmashauri yangu ambayo ninatoka. Geita ni kati ya Halmashauri nydingi ambazo zinapokea *service levy* ya 0.3% kutoka Mgodi wa *Geita Gold Mine* kutoka kwenye *gross revenue*, pesa hizi zinavyotumika nydingi zinatumika kwa ajili ya matumizi ya kawaida ya kuendesha shughuli mbalimbali za Halmashauri. Niiombe Serikali, tumetoa mwongozo hatujatunga sheria kuhusu utaratibu wa 5% kwa wanawake na 5% kwa ajili ya wanaume. Hebu tuweke utaratibu sasa kwamba walau 70% ya pesa zote zinazotokana na *service levy* ziweze kwenda kwenye shughuli za maendeleo na 30% ziingizwe katika matumizi ya kawaida. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, suala hili litatusaidia, hapa tunasema kwamba wananchi bado wana wajibu wa kuchangia huduma mbalimbali za kihuduma katika maeneo yetu, Iakini kuna hela ambazo zinatoka katika maeneo ya mgodi, kwa hiyo naiomba sasa Serikali iweze kutoa mwongozo huo ili pesa hiyo iweze kusaidia shule za maana zipatikane. Kwa sababu hizo hela hazina mwendelezo miaka si mingi pesa hizo zitakata kwani mgodi utamaliza shughuli zake. Kwa hiyo, ni afadhali sasa hizo pesa ziwe zimeshaingizwa kwenye shughuli za maendeleo za wananchi ili hata miaka ijayo watoto wetu watuone tuna maana, tulizitumia hizi hela kwa ajili ya faida yao, wamekuta huduma nzuri za afya na shule kutokana na kutumia hizi pesa vizuri. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ni kwamba tuna tatizo kubwa sana nchi hii. Mheshimiwa Rais alipokuwa anaingia madarakani alikataza mambo ya semina elekezi suala ambalo limezungumzwa pia katika hotuba ya Kambi ya Upinzani kwamba mafunzo elekezi ni suala nyeti sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi kwetu kule tuna shida, Mkuu wa Wilaya anawafukuza Wenye viti wa Serikali za Mitaa wakati sheria iko wazi, Mwenyekiti wa Serikali za Mtaa anaondolewa na wananchi. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kama hiyo haitoshi Mheshimiwa Rais ye ye mwenyewe alikiri akasema kwamba ye ye huu urais amepata tu, simu alipiga ikaitika. Kwa hiyo, kwa lugha nyingine ye ye mwenyewe alikuwa anastahili elekezi fulani, namheshimu sana Mheshimiwa Rais. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaangalia suala la watumishi wetu Serikalini tumekuwa na watu tunaowalipa mara mbili mbili. Hapa tunajifunza kwamba *scheme of service* inasema mtu anakawa *promoted* baada ya miaka mitatu kutokana na ripoti ya utendaji wake mzuri, lakini suala hilo halifanyiki ni kwa sababu Serikali hamna pesa, fedha nyingi mnalipa Wakurugenzi wawili, ma-*DED* wawili, ma-*DAS* wawili tutafika wapi kwa namna hiyo? Kwa hiyo, watumishi wa Serikali wanakosa morali kazi hazifanyika vizuri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, watumishi wa Serikali wanavunjika moyo na zaidi ya hapo bado tunawatumbua kiholela bila kuheshimu hata nafasi wala mamlaka walizonazo. Hata ndugu zangu hapo Waheshimiwa Mawaziri nyie pia mnakumbwa na hilo, heshima ya kuthamini utendaji wa mtu inakuwa haipo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba Serikali iangalie hili suala kama hawa watu wanapangiwa maeneo wapangiwe wawe *productive* kuliko kukaa nyumbani. Serikali mnalipa watu mishahara ambao hawana kazi ya maana ambayo wanaifanya katika Serikali. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini vilevile haya masuala kwamba hatuna hela, Serikali ifanye mkakati itafute pesa watu tuwapandishe vyeo kutokana na ripoti na ufanyaji kazi wao mzuri ili tuweze kuwa na wafanya kazi wazuri ndani ya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kipindi cha nyuma pamoja na kwamba Rais wa sasa alimbeza sana Rais aliyepita lakini alikuwa anatafuta viongozi au watu mpaka kutoka nchi za nje, watu wenye uelewa na wenye taalum fulani...

KUHUSU UTARATIBU

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Naibu Spika, Kuhusu Utaratibu.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Peneza naomba ukae, Mheshimiwa Simbachawene endelea.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Naibu Spika, Kanuni ni zile zile tulizozizoea Kanuni ya 68...

MBUNGE FULANI: Soma.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Naljua sana tu, naweza hata nikafundisha. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba niseme tu anachangia vizuri Mheshimiwa Peneza na halafu amependeza ...

MHE. HALIMA J. MDEE: Kuhusu Utaratibu Mheshimiwa.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Halima naomba ukae tafadhalii.

MHE. HALIMA J. MDEE: Utaratibu unataka ataje Kanuni iliyovunjwa...

MBUNGE FULANI: Kaa.

MHE. HALIMA J. MDEE: Sasa lazima ataje Kanuni iliyovunjwa.

NAIBU SPIKA: Naomba ukae Mheshimiwa Halima.

MHE. HALIMA J. MDEE: Nachosema utaratibu...

MBUNGE FULANI: Kaa chini.

NAIBU SPIKA: Nimekuelewa naomba ukae Mheshimiwa Halima. Mheshimiwa Simbachawene.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Naibu Spika, siku moja naomba unipe nafasi nitoe semina kidogo kama ukipata nafasi. (*Makofii*)

MHE. HALIMA J. MDEE: Wewe umesoma elimu ya kuungaunga, wengine...

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Halima naomba uzime *mic.*

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Naibu Spika, nachotaka kusema ni kwamba Mheshimiwa Mbunge anayechangia anachangia vizuri, lakini kuingiza maneno yanayomtaja Rais kwenye mchango wake kwamba anabeza Rais aliyepita, Rais aliyepita ni wa CCM na huyu Rais ni wa CCM na huu ni mwendelezo. Sijui ni lini mmeanza kuwa wazuri kwa Rais aliyepita kwa sababu hapa hapa ndipo yaliposemwa maneno kwamba Serikali ya Awamu ya Nne ni semina elekezi tu leo hii zinahitajika tena semina elekezi. Sisi tunadhani tumeteua watu ambao wana sifa na wanajua na tuna utaratibu wa kuelekezana na sheria zinazotuelekeza zipo.

MHE. HALIMA J. MDEE: Kuhusu Utaratibu Mheshimiwa.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, niseme tu kwamba mchangiaji anayechangia asiingize maneno kwa viongozi wakubwa wa nchi...

MHE. HALIMA J. MDEE: Kuhusu Utaratibu.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Kwa ajili ya kujenga hoja ya ku-*justify* anachokisema.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Halima naomba utulie kidogo na Mheshimiwa Upendo Peneza naomba ukae.

Waheshimiwa Wabunge, kwa sababu mjadala huu utaendelea na kama Mheshimiwa Spika anavyotukumbusha kila wakati kwamba utakuwa ni wa muda mrefu, Kanuni ya 68(1) inataka Mbunge akisimama kusema Kuhusu Utaratibu nimpe nafasi ataje Kanuni iliyovunjwa. Kwa hiyo, Kanuni ya 68(1) inataka Mbunge anayeomba Kuhusu Utaratibu aitumie hiyo, lakini Kanuni ya 64 ndiyo yenye mambo yasiyoruhusiwa Bungeni kwa ujumla. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, sasa kwa sababu tunajifunza tukiwa humu humu ndani ni vizuri hizi Kanuni wote tuwe nazo, tunaposhughulika na Kanuni fulani wakati mwengine ukitokea kila mtu ajue namna ya kufanya. Kanuni ya 64 inayo pale makatazo ya jumla ambayo hayaruhusiwi humu ndani, yako na mengine mengi lakini makatazo ya jumla yako hiyo. Binafsi nimemsikiliza Mheshimiwa Upendo Peneza kutaja tu majina ya Rais aliyepita na aliyepo si tatizo, tatizo ni pale ambapo umesema Rais wa sasa alikuwa akimbeza Rais aliyepita. Sasa hiyo habari maana yake tutataka kwenda tena mbele na nyuma, maneno hayo Mheshimiwa Peneza naomba uyaweke sawasawa ili tuweze kumaliza mjadala wetu vizuri. (*Makofi*)

MHE. UPENDO F. PENEZA: Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nadhani hata pamoja na kwamba tuna roho ya kuwatetea viongozi au mabosi wetu, lakini hebu tuwe wakweli, kama haya masuala hayakuandikwa hata kwenye vyombo vyta habari mseme kwa sababu ni vitu ambavyo vimeandikwa na vimesikika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, mimi niseme tu na hata nilivyzungumzia masuala ya semina elekezi hata kwa Mheshimiwa Rais mwenyewe si kawaida. Mheshimiwa Rais kweli, kuna kuteua Wabunge hapa si imeleta shida mpaka imebidi mtu tena mwenye ulemavu atolewe ni masuala ya shida hayo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ni kijana, naomba niseme kwamba naipenda nchi yetu hii, lakini pia namheshimu sana Mheshimiwa Rais, ni jirani yangu, ni baba yangu...

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Peneza jambo moja tu, kwa sababu nimesema ili tusianze kwenda mbele na nyuma, Rais wa sasa kuhusu kumbeza Rais aliyejita. Naomba hilo uliweke sawa ili tuweze kusonga maana hiyo sentensi ndiyo yenye kuleta taabu hapa.

MHE. UPENDO F. PENEZA: Mheshimiwa Naibu Spika, labda sijui kama ni neno kubeza niseme basi alikuwa akizungumzia upungufu kwenye utawala wake na yeze hawezikuyafanya kama yeze alivyofanywa, labda niseme kwa mfumo huo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, labda nimalizie kwa kusema neno moja kwamba naipenda nchi hii, lakini nathamini pia viongozi. Pia niseme kwamba tunahitaji...

(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MHE. UPENDO F. PENEZA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana.

MBUNGE FULANI: Endelea muda wako bado.

NAIBU SPIKA: Naambiwa walishaongeza muda tayari, hiyo ilikuwa kengele ya pili. Sasa namwita Mheshimiwa Savelina Mwijage.

MHE. SAVELINA S. MWIJAGE: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Na mimi napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kuweza kuchangia Wizara hii ya TAMISEMI.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijaanza kuchangia, napenda kupongeza Shirika la UN walioweza kuwajengea watu wa Bukoba walipata tetemeko. Wale wasiojiweza

wamewajengea mabanda ya kujihifadhi wazee na maskini, napenda kuwapongeza sana. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nianzie kwenye pesa za mchango wa tetemeko Bukoba. Hiso pesa walisema zinakwenda kujenga miundombinu ya shule za lyungo na Nyakato. Ni jambo la kusikitisha pesa ipo na majengo hayajajengwa, wamevuruga tu wakaacha hivyo hivyo, hao wanafunzi wataweza kurudi kusoma au ndiyo mwisho? (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, watu wanashangaa sana kwa sababu hizo pesa zilichangwa kwa ajili ya kuwasaidia watu waliopata madhara, lakini ikaamuliwa kwenda kwenye miundombinu. Mimi sijawahi kuona watu wanatumiwa pesa za kuwasaidia katika matatizo yao zinapelekwa sehemu nyingine. Je, tetemeko lisingetokea miundombinu isingejengwa? Naomba kama pesa hizo zimeshapelekwa kwenye miundombinu basi shule zijengwe tuweze kujua hiyo pesa imefanya kazi. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, niende kwa Wakuu wa Wilaya na Wakuu wa Mikoa. Watu wengi wameongea kwamba Wakuu wa Wilaya na Wakuu wa Mikoa wamekuwa Miungu watu katika Wilaya na Mikoa yetu. Wafanyakazi wanafanya kazi katika mazingira magumu kwa sababu ya kutishwa kuondolewa kazini. Kwa hiyo, tunaposema semina baadaye wanabadilisha kwamba tunabeza, wanapaswa wapewe semina, wasiwe Miungu watu kuwatisha wafanyakazi. Wafanyakazi tunawategemea na wanafanya kazi katika mazingira magumu, unakuta Mkuu wa Wilaya ndiye analeta migogoro ya ardhi ndani ya Halmashauri. Nilishawahî kumletea Mheshimiwa Waziri Lukuvi tatizo la Mkurugenzi wa Bukoba Vijijiini anavyovuruga Halmashauri, wapewe semina wajue mipaka yao, wasipende kuwavuruga wananchi. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, niende kwenye malipo ya wafanyakazi na walimu. Hatujabeza elimu bure ila tunazungumzia mazingira ya walimu, mazingira yaliyoko

katika shule, ukienda kwenye shule nyingi watoto hawana vyoo watapata akili gani ya elimu bure na kuendelea kupata elimu nzuri. Hawana mahali pa kujihifadhi, hawana maji, unakuta wasichana na wavulana matundu ya vyoo yamepakana na magonjwa kuambukizana inakuwa ni rahisi. Hatubezi, bali tunaongelea mazingira yalivyo na walimu wanadai pesa zao na wewe Naibu Spika, sisi tukikosa posho yetu hapa tunalalamika, niambie mwalimu anayekwenda kumfundisha mtoto hajui chochote anakosa pesa yake atakuwa na akili gani ya kuweza kumfundisha yule mtoto? Naomba sana pesa za walimu zikalipwe ili waweze kuwa na nguvu za kuweza kufundisha watoto. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, niende kwenye Hospitali za Wilaya. Bukoba Mjini tumepata Hospitali ya Wilaya iko mbali kabisa na mji, haina miundombinu, njia yenye shida. Tuliomba Serikali kwamba Hospitali ya Wilaya waboreshe yale majengo ya Zamzam ili mgonjwa akitoka kwenye Hospitali ya Mkoa iwe rahisi kuingia kwenye Hospitali ya Wilaya. Hivi sasa watu wanateseka imebaki kuwa hospitali ya majanga kwa sababu juzi ndiyo imesaidia kipindi cha tetemeko. Naomba sana hata yakiwa majengo mawili, matatu lakini yako karibu na wananchi siyo hospitali iko kijijini kabisa kule, miundombinu ya shida, watu hawaijui iko wapi. Wakifika mkoani pale wakakuta wodi zimejaa, wanaambiwa nenda kwenye Hospitali ya Wilaya kufika shida na dawa shida. Juzi wakati wa mafuriko haya watu wamehanganya, kuna daraja limepelekwa na yale maji wanavuka kwenda kwenye Hospitali ya Wilaya wanashindwa kwenda mtu anakaa pale pale anakosa hata mahali pa kwenda kutibiwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, niende kwenye tunaosema utawala bora. Tunasomesha wanafunzi wetu, vijana wanapata elimu wanakwenda kwenye vyuo lakini inafika wakati wa kupata ajira wanakosa ajira, unakuta vijana wana yeti vyao vizuri tu lakini wanaendesa bodaboda, ni aibu. Juzi umeona wametangaza kuwapeleka Kenya madaktari wengi walijitokeza na sisi hatuna madaktari katika nchi yetu inakuwa ni shida ni kwa sababu ya kukosa ajira. Kwanza tuwape ajira watu tuliosomesha kwa pesa za Serikali ili

waweze kulitumikia Taifa lao na sisi tufaidike na watoto wetu tunaowapeleka shule. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuongelea suala la Madiwani. Madiwani wanapata shida kwa sababu sasa hivi mapato ya Halmashauri zetu ni madogo sana. Unakuta barabara za kuunganisha Wilaya kutoka Bukoba Mjini kwenda Bukoba Vijijiini na kutoka Misenyi kwenda Karagwe barabara ni mbovu hawana, hata pesa zile za maendeleo. Serikali inatenga pesa lakini hazifiki kwa wakati. Tumekagua miradi mingi tumekuta pesa zinazoahidiwa na Serikali hazifiki kwa wakati kwa hiyo miradi inakuwa viporo. Sasa tunaiomba Serikali pesa zinazotengwa wakati huu zikipatikana wamalize viporo ndiyo waweze kuanza miradi mipy. Tukiendelea kuongeza miradi mipy na viporo ni vingi hatutaweza kwenda mbele. Ndiyo maana unakuta wengine tukisimama hapa tunasema Serikali imeshindwa ni kwa sababu ya kupanga mipango mipy ya zamani tunaiacha ilivyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mpaka leo hii Madiwani wanakopwa na Serikali kwa vikao wanavyokaa. Diwani anatoka zaidi ya kilometra 30 anakwenda Halmashauri kwa mfano kama Bukoba Vijijiini. Wilaya ya Bukoba Vijijiini iko Bukoba Mjini na tayari walishatenga viwanja vya kujenga Wilaya lakini mpaka leo hii hakuna mipango mikakati inayokwenda, anatembea kilometra zaidi ya 30, 40 anakuja Bukoba Mjini kwenye vikao, hapati posho zake, hana hata nauli ya kurudi kule, unamkuta amepanda ule usafiri wa mtaji wa maskini nguvu zake mwenyewe (baiskeli) kutoka kule ni mbali sana. Naomba Bukoba Vijijiini Halmashauri ijengwe katikati ya Wilaya, wametenga kiwanja kikubwa tu Mgaza. Diwani kukopwa na Serikali ni aibu, wapate posho zao, kile wanachokipata ni kidogo sana. Wangekuwa na pesa za maendeleo, wanapesa wanakusanya vizuri katika makusanyo yao ya Halmashauri ingekuwa ni nafuu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, niende kwenye Hospitali ya Mkao. Hospitali yangu ya Mkao pale, namshukuru Mheshimiwa Jafo anajitahidi sana akifika Bukoba

anazunguka sana, nampongeza sana na ukimletea tatizo lako anaweza kukusikiliza. Tatizo letu mpaka hivi sasa Bukoba Mjini hatuna mahali pa kuhifadhi maiti, kachumba ni kadogo, vijokofu hamna mpaka tunasafirisha maiti kupeleka Bugando. Ni aibu Hospitali ya Mkoa kukosa chumba cha kuhifadhi maiti. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hatuna wodi ya wazazi pale, ni ndogo sana, ina vitanda sita, wewe Naibu Spika ni mwanamke unakuja unaumwa uchungu unamsubiri mwenzako ajifungue ndio na wewe uingie, itawezekana, si utajifungulia kwenye simenti pale. Serikali ilishajiandaa kujenga lakini leo hii wamekaa kimya na hivi sasa nitaomba msaada kwa watu wa *MSD* waweze kutusaidia hata vitanda viwili angalau viwe nane waweze kupata mahali pa kujifungulia au hata ipanuliwe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, niende kwa wanafunzi ambao wamemaliza chuo na wanafunzi wengine, nikimaliza kuchangia hapa nitakwenda kwa Mheshimiwa Waziri wa Elimu, wanafunzi wanazuiwa kufanya mitihani kwa kuwa wanadaiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Mheshiniwa Waziri yuko pale napenda nimueleze kwamba mpaka sasa hivi Chuo cha Mwalimu Nyerere watoto wameshindwa kufanya mitihani kwa sababu wanadaiwa. Wameomba wakaambiwa jazeni fomu mtafanya mitihani mpaka sasa hivi wako nje hawajafanya mitihani kwa *semesterya kwanza* na ya pili. Tunaposema elimu bure basi tuwajali na wanafunzi wetu na wale watoto pesa wanapewa na wazazi kwenda kulipia karo, wawavumilie wafanye mitihani ikifika wakati wa kupata vyeti wawanyime vyeti mpaka walipie ile pesa yao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, niende kwenye matatizo yanayotokea Mkoa wa Kagera, nimalizie na hili. Watu wakimuongelea Rais mnasema kwamba tunamuongelea, hatumuongelei yeye bali yale matamshi. Vitabu vyta dini vinasema mdomo unaumba. (*Makofi*)

NAKALA YA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania nampenda sana, ni jirani yangu, amefika katika maafa anawaambia watu wa Kagera mimi sikuleta tetemeko, kweli mdomo unaumba. Kwa hiyo, naomba afute kauli yake ndipo watu wa Bukoba watakuwa na heshima na Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Naomba afute kauli ya kuwaambia mwafa, hilo jambo limekuwa kero kwa Watanzania na kwa wananchi wa Kagera. Kwa kweli wanaumia sana na jambo hilo. Hata Waziri Mkuu akisimama hapa afute hiyo kauli ili wananchi wa Mkoa wa Kagera waweze kuwa na imani na Rais.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.
(Makofi)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Savelina. Kabla ya Mheshimiwa Msigwa hajasimama, Mheshimiwa Waziri nadhani utatusaidia kwa sababu kuna taarifa zilitolewa kuhusu vitanda kupelekwa Halmashauri zote nchi hii. Zile taarifa zilikuwa ni za kutoka Serikalini ama hapana maana Mheshimiwa Savelina hapa anaongelea vitanda viwili tu kuongezeka. Sasa kama vinapelekwa vitanda 25 kila Halmashauri ni vizuri hilo jambo liwe wazi ili asiendelee kufikiria vitanda viwili, lakini ajue vinaenda zaidi ya hapo. Tujibu tu hilo sasa hivi ili twende vizuri. *(Makofi)*

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba tuna utaratibu wa kugawa vitanda karibu 25 kwa kila Halmashauri na zoezi hili linaendelea. Nafikiri tutafikia mpaka huko kwenye hiyo hospitali kwa hiyo asiwe na mashaka. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Kwa upungufu alioutaja hapa nadhani mtampelekea huko Bukoba mapema zaidi.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea, Mheshimiwa Peter Msigwa atafuatiwa na Mheshimiwa Dua Nkurua na Mheshimiwa Felister Bura ajiandae.

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, takwimu zinaonyesha kwamba toka mwaka 1980 mpaka 2010 Afrika pamoja na resources tulizonazo tumepoteza kiasi cha dola trilioni 1.4. Takwimu hizi zinaonyesha hii yote imesababishwa na uongozi mbovu katika Bara la Afrika. Mojawapo ya sababu ni kutokuwepo mwendelezo wa viongozi wanapobadilishana madaraka. Nchi yetu katika Serikali hii ya Awamu ya Tano kumekuwa na changamoto kubwa sana ambazo takwimu hizi zina-cement kwamba na sisi kama Taifa tunaweza tukaendelea tena kupoteza mali tulizonazo kwa sababu ya tatizo la uongozi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna Mtawa mmoja wa Kikatoliki alishi miaka 1953 kule Marekani anaitwa *Bishop Sheen*, aliwahi kusema; “*Civilization is always in danger when those who have given the right to command have never learned how to obey.*” (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi yetu iko kwenye kiza kinene kwa sababu kuna watu wengi sana ambaao wamepewa mamlaka ya kuamrisha lakini wao wenyewe hawajawahi kujifunza namna ya utii. Nazungumza haya kwa masikitiko makubwa sana kwamba tatizo kubwa tulilonalo katika Serikali ya Awamu ya Tano ni *poor leadership skills* ambayo hii inaweza ikatupelekea tukaingia kwenye matatizo makubwa sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri amezungumzia sana masuala ya Chuo cha Uongozi, lakini nina wasiwasi sana kama hiki chuo kina mtaala wa namna ya kuwa-train hawa watu. Kwa bahati mbaya katika nchi yetu uongozi unakuwa *defined* kwa *title* au *status* badala ya *function*. Uongozi wa sasa hivi tulionao wa Awamu ya Tano ni uongozi ambaao ni *bully*, ni uongozi ambaao ni *una-scream*, ni uongozi ambaao *una-shout*, ni uongozi unaо*-intimidate* badala ya kuonyesha njia. Kwa sababu ya uongozi huu ume-paralyze *civil service* na tuki-paralyze *civil service* maana yake

itashindwa ku-produce. Watu wako *intimidated* na uongozi huu hauko *based* kwenye *merit* kwa sababu watu hawajawa *trained*.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa ukiweza kutusaidia kwa kutumia lugha moja tutakuelewa wote vizuri zaidi maana kila neno moja linafuatiwa na lingine wengine lugha kidogo inaleta taabu. (*Makofii/Kicheko*)

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Mheshimiwa Naibu Spika, unanipotezea muda, Bunge si linaruhusiwa kuongea Kiingereza na Kiswahili unanitoa kwenye... (*Kicheko*)

NAIBU SPIKA: Tukienda kikanuni *actually*...

MBUNGE FULANI: *Actually.*

NAIBU SPIKA: Tukienda kikanuni, tusome hiyo kanuni...

WABUNGE FULANI: *Actually.*

NAIBU SPIKA: Sikilizeni Waheshimiwa Wabunge twende vizuri ili *Hansard* yetu ikae sawasawa, Mheshimiwa Msigwa.

MBUNGE FULANI: *Actually.*

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Mheshimiwa Naibu Spika, naamini utanitunzia muda wangu lakini na wewe mwenyewe umechanganya *actually*, sasa sijui hapo umesemaje, sijui ni Kiswahili hicho? (*Makofii/Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika *society* ambayo ni-*meritocracy*, *the blind cannot lead the sighted, uninformed cannot lead the wise and the unskilled cannot direct the skilled*. Katika uteuzi wa Mheshimiwa Rais, amechukua makada wengi wa Chama cha Mapinduzi amewaingiza kwenye *civil servant* ambayo hiyo ina-*cripple* utendaji wa kazi. Haya mambo hatuwezi kuyanyamazia kwa sababu hili Taifa ni la wote na ni kinyume kabisa na utaratibu. Ndugu

zangu wote tukumbuke hapa tunapokwenda kwenye uchaguzi watu wote sisi tunakuwaga hatuna madaraka sisi wanasiasa, huwa wanabaki *civil service*, *ukii-cripple civil service* maana yake unaua utendaji kazi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nimshauri tu Mheshimiwa Rais ambapo wenzangu wengi wanaogopa sana hata kumshauri, maana yake Mheshimiwa Rais akisema mkikamata watu wanavunja sheria ng'oa matairi kuna watu wanapiga makofi kinyume cha taratibu. Mheshimiwa Rais akisema mimi sikuleta matetemeko wanapiga makofi. Mheshimiwa Rais akisema mkikutana na jambazi huko hata kabla hajapelekwa mahakamani kinyume cha sheria watu wanapiga makofi, wanadhani kumsifu Mheshimiwa Rais kwa kile anachokifanya ni uzalendo. Tunatengeneza Taifa la waoga ambapo tuna *cripple national* kama hatuwezi ku-*criticise* viongozi wetu. Tuko hapa kuwafanya viongozi wetu wawe *accountable* na ndio wajibu wetu, (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Thomas Jefferson, Rais wa Marekani aliwahi kusema ukiona wananchi wanaiogopa Serikali jua Serikali hiyo ni ya kidikteta. Ukiona Serikali inawaogopa wananchi jua Serikali hiyo ni ya kidemokrasia kwa sababu Serikali lazima iwe *accountable* kwa wananchi. Sisi hapa kama Wabunge tuko hapa kuawakilisha wananchi, *the government must fear us*. Serikali lazima ituheshimu sisi kwa sababu lazima iwe *accountable* kwetu. Leo tunafika Bungeni tunanyamazishwa eti tusiikemee Serikali, *why are we here?* (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi kama kiongozi, wewe kama kiongozi *you are accountable to us*, Serikali mko *accountable* kwa Bunge hili. Sasa kila kitu mna-*protect*, chochote mnachofanya mna-*protect*, Serikali ya Awamu ya Tano imekuwa ni ku-*scream, shouting*. Huwezi kujua leo ni msiba au leo ni harusi, huwezi kujua leo wako kwenye matatizo, *leadership is about inspiring people, putting people to work is not about screaming and shouting*. Tuna uongozi wa Awamu ya Tano ambao una-*shout*, una-*scream* una-*intimidate everybody* kwa hiyo ume-*paralyze* watu kufanya

kazi. Halafu wengine wasomi hapa na ninyi mnakaa kimya mnapiga makofi mambo ambayo ni kinyume na utaratibu wa sheria ya nchi yetu, *where we heading? (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, *the unskilled cannot direct the skilled*. Tumekubali kuweka akili zetu mfukoni tunaongozwa na wale ambaao ni *unskilled*. Leo tuna watu kama akina Bashite amesema Sheen hapa, *those who have never learned how to obey they have given the right to command*, mtu kama Bashite anachokijua ni kuvaa shati la kijani na kumtukana Lowassa, ndicho alichoweza. Leo anakuwa Mkuu wa Mkoa anatoa amri kubwa halafu tunampigia makofi. Wale ambaao ni *incompetent wanawaongoza competent*, kwa hiyo, utendaji kazi unashuka wanaona sasa hata maana ya kusoma haipo. Kwa hiyo, mtoto ye yeyote anachoona ili niwe kiongozi ni kujua kumtukana mtu mmoja wa chama kingine, wapi tunakwenda jamani?

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna wanasheria kwa mfano Mwanasheria Mkuu hapa, wajibu wake mkubwa yeye ni kuhakikisha Serikali inafanya kazi lakini na yeye amegeuka amekuwa Mbunge anatetea Serikali. Badala ya yeye kunyoosha akiona Serikali inakosea anasema *Chief Whip* hebu ili jambo tu-withdraw tukajipange vizuri kwa sababu yeye ni kuweka mambo vizuri mwisho wa siku huu ni mtumbwi wa sisi wote lakini kilichotokea ni katil ya upinzani na sisi. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna mtaalamu mmoja anasema Taifa ambalo linazalisha *soft minded people* linanunua kifo kwa *installment* cha Taifa lenyewe. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu mna-discourage criticism katika Bunge, mna-discourage dialogue mnataka tuwe tunapiga makofi, *why are we here?* Kama mngetaka tusije hapa mngetuzuia kule kule Iringa wakati wa uchaguzi, *the fact kwamba watu wa Iringa wamenileta hapa I will speak, I will talk.* (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, leo tuna *TISS* (Usalama wa Taifa) ambapo kazi yake kubwa ni ku-*protect* Chama cha Mapinduzi badala ya ku-*protect*nchi. Ukija kwenye Mkuano Mkuu wa Chama cha Mapinduzi robo tatu utawakuta watu wa *TISS* wamevaa nguo za kijani, *they are busy* na Chama cha Mapinduzi. Tunazungumza hapa kuna mauaji, utekaji lakini ni kwa sababu wameacha mambo ya msingi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, *in this country* kila mtu anaweza akafanya jambo lolote. Jeshi linawenza likakusanya kodi na bunduki, leo tunakusanya kodi na bunduki (*with guns*). Hujui nani anafanya nini na kwa ajili ya nini ni kwa sababu nchi haina *priority, poor leadership.* (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, niwaombe ndugu zangu hebu tujipange Serikali ni ya kwenu, tuji-reorg, tujipange vizuri kwa sababu ni kama ubongo ambaao uko *scattered, you are every where, there is no priority.* Mara tunaenda Dodoma, mara leo Bashite anakamata sijui watu gani, mara huyu ametumwa nini na kwa sababu hatuna *priorities* hatujui tunataka kufanya nini. Ni kama vile wataalamu hawapo katika nchi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunatoa mawazo yetu lengo ni kuifanya Serikali yetu iwe nzuri. Tume-*discourage* fikra ambazo zina *criticize* kwa sababu hakuna mtu ambaye hawezni kuwa *challenged* katika ulimwengu huu. Kuwa *challenged* ni sehemu ya uongozi ili ujipime, sisi ni *mirroryaani* sisi ni kioo chenu huwezi kwenda kwenye kioo nywele hujachana unakipiga ngumi kioo sasa utajionaje, mnatupiga sisi sasa mtajionaje?

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi ni kioo chenu tunawaona hivyo mnavyofanya, wote mmekuwa waoga (*terrified*). Mawaziri wote mko-*terrified* hapo, Wabunge mko-*terrified* tukitoka huko nje ndiyo mnatiambia ee bwana lakini hapa mnasema kweli na wengine nikitoka nje mtaniambia lakini humu ndani hamsemi. (*Makofi/Kicheko*)

NAKALA YA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Naibu Spika, niombe Usalama wa Taifa wafanye kazi yao vizuri. Tumezungumza mauaji hapa sina muda wa kusema, baada ya Wabunge kusema kuna watu wako-*tortured* sana kule Mpingo wanafungiwa kwenye kachumba kadogo, wanakojoa humo humo, wanajisaidia kwenye rambo wanateswa halafu wakionekana hawana hatia wanawadampo kwenye kituo cha mabasi pale wengine wako kwenye Jimbo langu toka Iringa wanaachwa na nauli tu. Hatuna muda wa kusema tu lakini haya mambo yapo watu wanakuwa *totured* tukisema hamtaki kusikia

NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO

YA MAKAZI: Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa
Mzungumzaji)*

NAIBU SPIKA: Muda wako umekwisha Mheshimiwa Msigwa, Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO

YA MAKAZI: Mheshimwia Naibu Spika, ahsante. Nasimamia kwenye Kanuni ya 68(8). Mheshimiwa mchangiaji aliyekuwa anaendelea na bado anaendelea kwa sababu umemsimamisha, anazungumzia suala la Mawaziri wote wako *terrified* na hawawezi kufanya kazi zao kwa kujiamini.

Naomba nimpe taarifa tu kwamba katika timu ya Mawaziri wote na watendaji wao hakuna hata mmoja anayetenda kazi kwa kuogopa, hakuna mwenye hofu na kila mmoja anatekeleza majukumu yake kadri taratibu zinavyomuongoza. Kwa hiyo, nilitaka kumpa taarifa hiyo kwamba hakuna aliye-*terrified* kwa uongozi uliopo. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante.

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Mheshimiwa Naibu Spika, sijaipokea taarifa hiyo.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Msigwa ulikuwa umeshamaliza kwa hiyo hujapewa hiyo taarifa wewe.

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Mheshimiwa Naibu Spika, sijaipokea hiyo taarifa.

NAIBU SPIKA: Naomba ukae tafadhalii.

Waheshimiwa Wabunge, ni hivi, mimi nilikuwa nimeshamsimamisha Mheshimiwa Msigwa kwa kuwa alikuwa ameshamaliza kuzungumza na muda wake umekwisha.

(Hapa baadhi ya Wabunge walikuwa walizungumza bila mpangilio)

NAIBU SPIKA: Tusikilizane, mkiuliza jambo ni kwamba mnataka kujibiwa kama hamjui majibu msiulize basi. Ukitaka kujua jambo sikiliza basi unachojibiwa.

Ni hivi kwa kuwa yeye ametoa taarifa wakati mzungumzaji amekwishakukaa maana yake ni kwamba mimi simpi nafasi huyo mtu kwa sababu kanuni zinataka taarifa mtu atoe wakati anazungumza. Sasa ninyi mnataka kung'ang'ania jambo ambalo halipo.

(Hapa baadhi ya Wabunge walikuwa walizungumza bila mpangilio)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tusikilizane, tutaeendelea na wachangiaji wanaofuata. Nilimtaja Mheshimiwa Dua Nkurua atafuatiwa na Mheshimiwa Felister Bura na Mheshimiwa Atashasta Nditiye ajiandae.

MHE. DUA W. NKURUA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia katika Wizara yetu ya TAMISEMI. Awali ya yote namshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kunipa uhai na afya njema nikaweza kuchangia muda huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumekutana hapa kuviangalia vipaumbele vya Taifa hasa katika matumizi ya pesa yetu kwa muda wa mwaka wa fedha 2017/2018. Kwa hiyo, vipaumbele vya Taifa vipo na mimi kama Mbunge nitajaribu kuviongezea vile ambavyo Wizara labda hamkuviona.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa niishukuru Wizara kwa kuruhusu baadhi ya Halmashauri kutumia asilimia 60 kwa ajili ya kuendesha Halmashauri na asilimia 40 kwa miradi ya maendeleo. Suala hili kwa mtu ambaye hajadumu sana Halmashauri anaweza akalliona ni dogo, lakini Halmashauri nyingine hazina uwezo wa kuendesha Halmashauri zao.

Kwa hiyo, unapowaambia watumie asilimia 60 kwa maendeleo kinachotokea ni kwamba wanakwenda kuathiri pesa zingine na cha kwanza kinachokwenda kuathiriwa ni pesa za mikopo ya akina mama na vijana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kwa kuziruhusu baadhi ya Halmashauri kutumia asilimia 40 kwenye maendeleo na asilimia 60 kuendeshea Halmashauri yao itasaidia kufuata kanuni ambazo Serikali imeweka kuliko pale mwanzo ambapo mlikuwa mnalazimisha asilimia 60 ambazo zilikuwa hazifanyi kazi. Mkumbuke hapo mwanzo ilikuwa asilimia 60 inakwenda kwenye maendeleo, asilimia 20 inakwenda kwenye vijiji na asilimia 10 ilikuwa mikopo ya vijana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, utakuta asilimia 90 imekwenda kwenye mpango ambao Serikali imeelekeza lakini matokeo yake yalikuwa hayaendi vizuri. Kwa hiyo, hilo nalipongeza sana kwa mtazamo huo na nafikiri Halmashauri ya Nanyumbu itakuwa ni mojawapo ambayo itawekwa katika asilimia 40 ili waweze kuendesha vizuri Halmashauri yao na waweze kusimamia pesa nyingi ambazo Serikali inapeleka kule Halmashauri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wangu wa kwanza naenda kujikita kwenye elimu. Nafahamu kwamba Taifa lolote ambalo elimu haijaka vizuri, basi tutakuwa na matatizo mengi kwa sababu elimu ndiyo kama taa, ndiyo kama mwongozo wetu wa kuweza kupambana na maisha haya ya dunia. Sasa Serikali yetu imewe ka vipaumbele vingi katika elimu, imetuonesha katika Bajeti yake mambo gani ya msingi yatakwenda kuzingatiwa ili tuweze kuisimamia vizuri elimu. Sasa nayaunga mkono yote hayo na nataka nisisituze baadhi ya machache.

Mheshimiwa Naibu Spika, la kwanza, Serikali iweke utaratibu wa wazi wa kuweza kuboresha miundombinu ya shule. Tuna matatizo ya madarasa, nyumba za Walimu na Walimu. Maeneo haya matatu yanatusumbua sana katika Serikali yetu. Naiomba sana Serikali isaidie Halmashauri katika ujenzi wa shule, nyumba za Walimu na vyoo katika shule zetu zote za nchi nzima. Katika eneo hili itatusaidia kuwa na shule zenye ubora, lakini pia kuwa na Walimu wenyewe moyo wa kufanya kazi. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ambalo nataka Serikali itilie mkazo ni malipo ya Walimu. Nimeona mkakati amba Serikali imeuweka, naupongeza, lakini naomba sana Serikali isisituze kuhakikisha kwamba Walimu wetu wanapata malipo yatakayowasaidia.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine katika elimu ambalo naomba sana Serikali iliangalie ni uhaba wa Walimu. Wilaya ya Nanyumbu, kwa matokeo ya Darasa la Saba mwaka jana tulifanya vibaya sana katika Mkoa wa Mtwara, lakini pia hata Kitaifa hatukwenda vizuri. Sisi kama Wilaya tulikaa tukayaangalia matatizo yetu ya ndani tujue ni kwa nini tumefika hapo? Tukayabainisha na tumejipanga kukabiliana nayo. Tunayo timu kule ya watu, tunao Madiwani, tunaye Mkuu wetu wa Wilaya, anafanya kazi vizuri sana. Tunahakikisha yale matatizo ya ndani tutakabiliana nayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, yapo matatizo ya nje ambayo lazima Serikali itusaidie. La kwanza, tuna uhaba

mkubwa wa Walimu. Wilaya ya Nanyumbu inahitaji Walimu zaidi ya 1,100 lakini ina Walimu kama 600 hivi. Kwa hiyo, tuna upungufu wa Walimu zaidi ya 450. Kwa hiyo, unakuta kwamba uhaba huo wa Walimu ambao umekithiri, huwezi kuwa na wanafunzi watakaofanya vizuri. Ni sawa na timu isiyo ya kocha, haita-*perform* vizuri. Kwa hiyo, naomba sana Serikali katika mgao wa Walimu awamu hii ihakikishe kwamba Nanyumbu inapata Walimu wa kutosha ili tuweze kuwa na elimu bora ambayo Serikali inalenga kuifikia.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ambalo nataka nilichangie ni afya. Nafahamu Wizara hii ina kazi kubwa, inasimamia afya zetu na za wananchi wetu pia. Afya inafanana na elimu. Tuna uchache wa Zahanati na Vituo vya Afya. Sera ya chama chetu ambayo ndiyo inaongoza nchi hii, tulikubaliana kwamba tutajenga Zahanati katika kila kijiji, lakini nafahamu kwamba safari hii ni ndefu, hatuwezi kujenga leo wala kesho tukamaliza vijiji vyote.

Mheshimiwa Naibu Spika, Halmashauri zitaweka vipaumbele wapi ikajengwe; lakini naomba sana, Serikali iweke mpango maalum utakao-*support* Halmashauri kukamilisha lengo hili. Halmashauri zetu nyingi hazina uwezo wa kukamilisha hili. Kwa hiyo, Serikali iweke mpango ambao utaruhusu pesa nyingi kwenda Halmashauri ili kujenga hizo Zahanati. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ujenzi huo hautatusumbua sana. Wananchi wamejiandaa kujenga zahanati, tusifikiri kwamba Serikali itakwenda kujenga *complete* hii zahanati. Wananchi wamejitoa sasa, kwa hiyo, cha msingi ni Serikali kupeleka pesa na wananchi watajenga, pale ambapo Serikali itahitaji isaidie, tutamalizia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba sana Serikali tupeleke pesa ambazo zita-*support* jitihada za wananchi katika ujenzi wa zahanati katika vijiji vyetu. Tuliahidi wenyewe; nina uhakika kwa kasi ambayo tunayo ya ukusanyaji wa mapato na *seriousness* ya Serikali yetu na Rais wetu, suala hili tutalikamilisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, najua kuna watu wanafikiri ni ndoto, lakini nina uhakika kwamba kwa kasi ya Serikali yetu na kwa kasi ya Rais wetu, suala hili litafanikiwa na wanaobisha tutakutana 2020; watahakikisha! Tutafikia pakubwa, kwa sababu pesa ndiyo itakayofanya haya na wananchi wetu tumeweza kuwaandaa vya kutosha. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nitahukumiwa na wananchi wangu wa Nanyumbu kwa jinsi nitakavyohamasisha na Serikali itakavyoniletea pesa ya kumalizia majengo hayo. Kwa hiyo, naiomba Serikali tutenge pesa maalum kwa ajili ya ujenzi wa Zahanati na Vituo vya Afya. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ni watumishi. Tuna uhaba mkubwa wa watumishi wa zahanati zetu. Naomba sana Serikali ijipange kuhakikisha kwamba tunaweza kumudu kuwatuma watumishi katika zahanati zetu kwa sababu tuna uhaba mkubwa sana wa watumishi katika zahanati zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ambalo nataka nilichangie ni posho ya Waheshimiwa Madiwani. Madiwani wetu wana kazi kubwa sana na wengi hapa wamegusia namna ambavyo Madiwani wanasimamia pesa ambazo Serikali inapeleka kule. Sasa huwezi kumtuma mtu akasimamie pesa, mwenyewe amechanganyikiwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, posho ya Madiwani ni ndogo, sisi tulikuwa huko, tumeiona ni ndogo sana kiasi kwamba wanakosa moyo wa kuweza kusimamia vizuri pesa ya Serikali ambayo ni nyingi inayokwenda kule kwenye Halmashauri. Kwa hiyo, naiomba sana Serikali ihakikishe kwamba posho ya Madiwani inapanda. Imepanda siku nyingi sana; tuliomba mwaka 2016 na mwaka huu sijaona kama imeendelea vizuri. Kwa hiyo naomba sana posho ya Madiwani izingatiwe ili tuwape motisha Madiwani hawa waweeze kusimamia vizuri pesa ya Serikali ambayo inakwenda kule katika Halmashauri zetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine la mwisho, ni posho pia au niite mshahara wa viongozi wetu wa vijiji. Ni eneo lingine ambalo tumelisahau. Tuna vijiji vingi nafahamu, mzigo ni mkubwa lakini twende tuanze tuwaoneshe njia. Tuna Wenyeviti wa Vijihi na Wenyeviti wa Vitongoji. Hao wote wanafanya kazi katika Serikali yetu kuhakikisha kwamba wananchi wanakuwa na amani na wanakuwa na maendeleo, wanasimamia maendeleo kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba Serikali katika mipango yake ituambie namna gani inafikiria kuhakikisha kwamba wananchi hasa Viongozi wa Vijihi na Wenyeviti wa Vijihi na Watendaji wanapata posho au mshahara ili wawe na moyo wa kuweza kutumikia vizuri Serikali yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja. Ahsante sana. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Felister Bura, atafuatiwa na Mheshimiwa Atashasta Nditiye na Mheshimiwa Mbaraka Dau ajiandae.

MHE. FELISTER A. BURA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Pia namshukuru Mwenyezi Mungu kwa afya njema na kwa kutupa nafasi tena ya uhai katika maisha haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimesimama kuipongeza Serikali ya Awamu ya Tano kwamba sasa imetekeleza yale yaliyoamriwa tangu mwaka 1973 ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano kuhamia Dodoma. Nimeona kwa vitendo. Mheshimiwa Rais alisema tarehe 25 mwezi wa Saba mwaka 2016, kwamba Waziri Mkuu atahamia Dodoma na Mawaziri na Makatibu Wakuu pamoja na Watendaji wengine. Jana katika uwanja wa mashujaa, Serikali ilisema mpaka sasa waliohamia Dodoma ni watumishi zaidi ya 2,000. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naipongeza sana Serikali ya Awamu ya Tano kwa uamuzi huo. Tatizo nililonalo

ni hili; wakati Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu anajibu hoja za Wabunge katika Bajeti ya Waziri Mkuu alisema kwamba Muswada wa Sheria ya Serikali kuhamia Dodoma utaletwa Bungeni hivi karibuni, lakini hakusema muda. Utaletwa Bunge hili; Bunge ijalo au Muswada huo utaletwa mwaka 2020? Hakusema.

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wa Dodoma wanataka *time frame* kwamba ni lini Muswada wa Sheria wa Serikali kuifanya Dodoma kuwa Makao Makuu utaletwa Bungeni na kujadiliwa na Bunge hili? Jambo hilo ni muhimu sana kwa sababu hata ilipoamuliwa mwaka 1973, hakuna Sheria iliyotungwa na Bunge hili mwaka 1973 na kuifanya Dodoma kuwa Makao Makuu ya nchi. Kwa sababu hatua imechukuliwa na Serikali ya Awamu ya Tano, sasa ni muhimu kupata *time frame* ya Muswada kuletwa Bungeni na kujadiliwa na Bunge hili na sasa iwe sheria kwamba Makao Makuu ya Serikali ni Dodoma. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeomba Mji wa Dodoma kuwa Jiji. Hatua zote tumeshafanya, tumeshapitisha kwenye Baraza la Madiwani, tumeshapitisha *DCC* na vikao vya *RCC*, lakini mpaka leo agizo hilo au ombi letu halijatekelezwa. Naiomba Serikali, vigezo vyote tumezingatia, kanuni zote tumezipitia, Serikali ione namna sasa ya kuifanya Dodoma kuwa Jiji na hasa ukizingatia ujio wa watu wengi na vigezo vyote vimetekelezwu kama agizo la Serikali liliwyosema. Sasa tunaisubiri Serikali itupe Jiji la Dodoma. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, watu wengi wanahamia Dodoma na wengi wangependa kujenga na wawekezaji wengi wangependa kujenga katika Mji huu na hata viunga vya Dodoma kwa mfano Bahi, Chamwino na maeneo mengine, lakini bado tuna changamoto ya miundombinu. *CDA* ambao wamepewa kazi ya kuhakikisha kwamba wanapanga Mji, hawana fedha za kutosha kupanga mji huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nadhani Serikali sasa iangalie Mji wa Dodoma kwa macho ya huruma na kwa kuzingatia kwamba wengi wanahamia na wengi

wangependa kujenga, lakini *CDA* ambao wamepewa mamlaka ya kupanga Mji, hawana fedha za kutosha. Kwa hiyo, *CDA* wapate fedha za kutosha, washirikiane na Manispaa ya Dodoma kupanga mji huu tusiwe na *squatter* kama miji mingine ilivyo. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nimesoma katika Bajeti ya Waziri wa TAMISEMI, mdogo wangu Mheshimiwa Simbachawene. Nimeona jinsi alivyoonesha maabara yaliyojengwa nchi nzima na akasema kwamba katika ukurasa ule wa 27 na akaonesha kwamba mpaka sasa tumekamilisha asilimia 27% tu ya majengo ya maabara. Katika Mkoa wangu kuna maeneo mengi ambayo majengo ya maabara hayajakamilika. Naomba Serikali yangu sikivu kwamba majengo yale sasa, Serikali ione namna ya kuyakamilisha na Walimu wa Sayansi ambao wameajiriwa kwa sasa wapate kuwafundisha watoto kwa vitendo. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naamini kwamba hata mikoa mingine maabara hazijakamilika kwa asilimia mia moja. Kwa hiyo, katika Wilaya na Halmashauri zetu kama hakuna vifaa vya maabara vya kutosha, hakika wanafunzi hawatajifunza kwa vitendo. Tunatamani wanafunzi wanaosoma sayansi wajifunze kwa vitendo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna shida katika Wilaya yetu ya Bahi. Mimi ni Mbunge wa Mkoa, kwa hiyo, Wilaya zote za Dodoma ni zangu. Tuna shida kubwa katika Wilaya ya Bahi na Wilaya ya Bahi tunategemea kwamba hata wawekezaji na hata ofisi nyingine za Serikali zinaweza kujengwa katika maeneo ya Bahi, lakini pale hatuna Hospitali ya Wilaya. Kituo cha Afya kilichopo kinalaza wagonjwa nane tu. Tulileta maombi maalum kwa Serikali kwamba hospitali ile tena iko njiani, Kituo cha Afya kile kipewe huduma zinazostahili, tupewe *theatre* ndogo. Wanawake wanaotaka kujifungua, kama wana matatizo wanaletwa Dodoma Mjini, kilometra 65. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeleta maombi maalum kwa Serikali yetu. Naomba sasa kwa ajili ya wananchi wa

Bahi; ni miaka kumi sasa tangu Wilaya ile itengwe lakini mpaka leo hawana hospitali ya Wilaya, lakini hata Kituo cha Afya kilichopo basi kiimarishe ili kiweze kuwahudumia wananchi wa Wilaya ya Bahi. Afya ya Mtanzania ni muhimu, afya ya mwanamke na mtoto ni muhimu, lakini hatuna hata *theatre* ndogo pale. Naiomba Serikali ilifikirie sana jambo hilo. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna shida pale Bahi ya maji. Tumeleta maombi maalum kwa Serikali kwamba itusaidie maji. Maji ya pale Bahi hayastahili kwa matumizi ya mwanadamu. Naomba sana Serikali ikawasaidie wananchi wa Bahi, maji ya pale yana chumvi mno na Bahi kuna madini ya *uranium*. Kwa hiyo, naiomba Serikali iwasaidie wananchi wa Bahi kwa kuwaangalia kwa jicho la huruma. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nimesoma kitabu cha bajeti ya Waziri wa Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, ukurasa wa 39. Nimeona ajira ambazo zimetolewa kwa mwaka huu unaokwisha, ajira 9,721. Siyo mbaya, kwa sababu wamepewa Maaskari Polisi, Uhamiaji na kadhalika; lakini tuna shida kubwa ya wahudumu wa afya katika maeneo yetu. Wahudumu katika Vituo vya Afya na Zahanati zetu. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Dodoma pamoja na wafanyakazi kuhamia kwa wingi, hospitali ya Ben Mkapa inapunguza, wagonjwa wanakwenda Hospitali ya Mkao, lakini pale kuna wahudumu 51, kati ya wahudumu 751. Kuna upungufu mkubwa sana. Nilitegemea kwamba Waziri wa utumishi angeliangalia hili kwa macho ya huruma. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna upungufu wa Watendaji wa Mitaa. Tuliambiwa kwamba kada hii tunaweza kuwaajiri, lakini tunawaajiri vipi kama hatuna bajeti? Naisihi tena, Serikali yangu sikuvi iweze kuwapa mamlaka Halmashauri zetu pamoja na fedha. Kuwapa mamlaka siyo neno, lakini fedha za kuwalipa hawa Watendaji wa Mitaa na Watendaji wa Kata watazitoa wapi? Naomba hili litazamwe. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, posho ya Madiwani imezungumzwa sana na Waheshimiwa Wabunge. Linatuhusu kwa sababu na sisi ni Madiwani. Madiwani ndio wasimamizi wa miradi ya maendeleo katika maeneo yetu. Posho yao ni ndogo mno. Madiwani wakumbukwe. Wao ndio wasaidizi wetu, wao ndio wanaosimamia miradi yote ya maendeleo; tukiwasahau hatuwatendei haki. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, nichangie kuhusu Zahanati ya Hamai. Tuliomba fedha kwa ajili ya kituo hicho...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha
kwa muda wa mzungumzaji)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa muda wako umekwisha.

MHE. FEELISTER A. BURA: Mheshimiwa Naibu Spika, naunga hoja mkono. (*Makof*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Atashasta Nditiye, atafuatiwa na Mheshimiwa Mbaraka Dau, tutamaliza na Mheshimiwa Angelina Malembeka.

MHE. ENG. ATASHASTA J. NDITIYE: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Awali ya yote nianze kumshukuru Mungu kwa nafasi hii, lakini vile vile niendelee kuwashukuru sana wananchi wangu wa Jimbo la Muhammadi kwa kunituma kuja kuwatumikia kama Mbunge wao. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nilitamani sana nizungumze kwenye bajeti ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Pamoja na mambo mazuri yaliyoongeleta kwenye hotuba yake, lakini nina ushauri mdogo sana ambao ningependa niutoe.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna hili suala la *Private Public Partnership (PPP)*; nitaongelea hasa kwa Jiji la Dar es Salaam kama ushauri. Naamini Serikali yangu ya Chama cha Mapinduzi itaupokea. Kuna suala la ujenzi wa kipande cha barabara kutoka Dar es Salaam mpaka Chalinze, sina tatizo

na hiyo; na kuna kipande cha barabara kutoka *Oysterbay* ambacho kitakwenda mpaka *Ocean Road*. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nina ushauri mdogo tu kwa Serikali yangu kuhusu kipande cha barabara ya kutoka *Oysterbay* mpaka *Ocean Road*. Ni kweli kwamba kile kipande kinajengwa kwa ajili ya kusaidia kupunguza foleni katika Jiji la Dar es Salaam, lakini kwa maamuzi ya Serikali ya kuhamisha Makao Makuu kuja Dodoma, naona uwezekano wa foleni hasa kipande cha kutoka maeneo ya Bunju mpaka Mjini ikiwa inapungua. Nilikuwa Dar es Salaam juzi nimeona kabisa kwamba foleni inapungua na hapa wamehama wafanyakazi wachache sana. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naamini watakapohama kabisa, kile kipande cha barabara kutoka *Oysterbay* ambacho kikimalizika itatakiwa watu wawe wanalipia ili kufika mjini, kinaweza kukosa pesa ya kurudisha kwa ajili ya kuwalipa wale *private* na hivyo tukaiingiza Serikali kwenye gharama ya kulipia.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri kwamba kama kuna uwezekano, kama hatujafika mbali sana kwenye hatua hiyo, basi Serikali iangalie namna ya kuzitoa himo pesa zije huku Dodoma zijenge miundombinu tutanue mji wetu ambao hakika sasa hivi tunaanza kuiona foleni hapa Dodoma. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya ushauri huo, niingie kwenye hotuba ya TAMISEMI na Ofisi ya Rais, Utawala Bora. Kwanza nawashukuru sana Ofisi ya TAMISEMI; Mheshimiwa Waziri Simbachawene na Msaidizi wake Mheshimiwa Jaffo kwa kazi nzuri sana wanayoifanya. Wamekwishatemebelea sana sehemu mbalimbali za nchi yetu na kwangu Wilaya ya Kibondo wameshafika. Nashukuru sana kwa shughuli mbalimbali wanazozifanya. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nitaongelea sana Kituo cha Afya cha Kifura katika Wilaya yangu ya Kibondo. Kituo hiki cha Afya kimesahauliwa sana kwa muda mrefu.

Miundombinu yake imekuwa chakavu, lakini hicho kituo kimezidiwa kiasi ambacho kinasababisha hata Hospitali ya Wilaya nayo izidiwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, tukumbuke tu hii hospitali ya Wilaya ya Kibondo inatumika kama Hospitali ya Rufaa kwa Hospitali ya Kakonko kwa jirani yangu Mheshimiwa Bilago. Wale pale hawajawa na Hospitali ya Wilaya inayoitwa Hospitali ya Wilaya. Kwa hiyo, rufaa zao zote wanazileta Kibondo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya yangu ya Kibondo pale, kwa takwimu za mwaka 2012 ina watu 290,000. Kwa sasa hivi lazima watakuwa wameshazidi, lakini tuna Kambi ya Wakimbizi ya Nduta ambayo Hospitali yao ya Rufaa na wao ni Hospitali ya Wilaya ya Kibondo, ambayo miundombinu yake bado ni ya mwaka 1969. Naomba sana Serikali langalie hilo iweze kupanua miundombinu katika hospitali hiyo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile miundombinu ya maji katika Wilaya yetu ya Kibondo ambayo ni ya toka mwaka 1973, bado inaendelea kutumika mpaka sasa hivi. Kumbuka mwaka 1973 tulikuwa na wakazi wasiozidi 64,000, sasa hivi tuna watu zaidi ya 290,000 ukiondoa watumishi wanaokuja kuhudumia wakimbizi ambao tunao wengi sana; kwa hiyo, huduma ya maji ni ya kiwango cha chini sana katika Wilaya yetu ya Kibondo. Tunaomba sana Serikali iliangalie hilo tuweze kupata miundombinu ya maji ya kuweza kutosheleza watu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tulijaribu kuongea hata na Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani asaidie kuhusu suala la kuwabana *UNHCR* ambao ndio wameleta wakimbizi pale wasaidie katika suala hilo. Naamini Waziri wa Mambo ya Ndani bado analishughulikia suala hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitoe shukrani ya dhati kwa Wizara ya Afya kwa kutuletea gari moja ya kuhudumia

wagonjwa (*ambulance*). Gari hiyo imekuwa ni ya msaada mkubwa sana kwa akinamama na watoto ambao walikuwa wanapata shida sana. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, niingie kwenye suala la ahadi za Mheshimiwa Rais. Mheshimiwa Rais wakati anafanya kampeni zake, mwaka juzi, 2015 alipita pale Wilayani Kibondo akaahidi ujenzi wa kipande cha lami cha kilometra sita. Kila nikienda kule, huwa nadaiwa. Naomba sana, TAMISEMI waangalie namna ya kuweka kwenye mahesabu yao, hicho kipande cha barabara kiweze kujengwa, kwa sababu ni ahadi ya Mheshimiwa Rais ambayo aliwaahidi wananchi wa Wilaya ya Kibondo na Wilaya ya jirani ya Kakonko, nakumbuka. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine aliloliahidhi Mheshimiwa Rais ambalo natamani sana lifanyiwe kazi ni suala la pensheni kwa wazee. Mheshimiwa Rais akiwa jukwaani aliahidi wazee wote ambao hata kama siyo wafanyakazi, wafugaji, wakulima, anapotimiza miaka 60 watapewa pensheni ya kila mwezi. Naomba sana hilo suala lifuatiliwe na lienze kutekelezwa. Japo nimeangalia katika bajeti sioni utaratibu wowote ambao umesababisha hili suala liweze kuwa la kutekelezeka. Naomba sana Serikali iliangalie hili suala ili tusipate shida sana na wananchi wetu. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna suala la *TASAF*. Mpaka sasa hivi, katika Wilaya yangu ya Kibondo kijumla bado naona lina utata mkubwa sana. Ni kweli kwamba kuna baadhi ya watu walipewa hizo fedha, lakini hawakuwa wanastahili; nashukuru kwamba kuna baadhi wameondolewa; lakini utekelezaji wa suala hilo umewagusa hata wale ambao walikuwa wanahuksika katika kupewa hiyo pesa ya *TASAF*. Wameondolewa bila utaratibu maalum. Sijajua utaratibu uliotumika kuwaondoa baadhi ya watu ambao wanastahili kabisa kuwemo katika utaratibu wa *TASAF*. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sana, Serikali iangalie tena upya wale ambao wanastahili kuwemo kwenye

utaratibu wa kulipwa na *TASAF*, waendelee kulipwa bila kubaguliwa na wale ambao hawastahili waondolewe kweli. Natamani sana watumike viongozi wa Serikali za Vijiji, lakini huu utaratibu naona *TASAF* kwenye Ofisi za Wilaya kule wanaamua wenyewe wanavyotaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichangie kidogo kuhusu suala la usambazaji umeme kwenye taasisi za umma. Tunashukuru sana Serikali kwamba imekuja na *REA* awamu ya tatu, tunaamini watasambaza umeme katika vijiji vyote. Utaratibu wa *REA*, wanapitia kwenye barabara kuu na kwamba watakwenda kushoto na kulia kilometra isiyozidi moja na nusu kusambaza umeme.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa muktadha huo, umeme unapita karibu na shule au zahanati, sijaona kama Wilaya zile ambazo kipato chake ni kidogo, zimesaidiwa je kuhakikisha kwamba shule za sekondari, msingi na zahanati zinaingiziwa umeme kwenye Taasisi hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sana Serikali ihakikishe kwamba shule za sekondari hasa zile za kata zinaingiziwa umeme ili kutupunguzia mzigo sisi Wawakilishi kwa kuwa tunadaiwa kila tunapokwenda, tuingize umeme na kufanya *wiring* moja kwa moja. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile tuna upungufu wa Walimu katika sekondari zetu; hilo najua limeshapigwa kelele sana na Waheshimiwa Wabunge, naamini Serikali italifanyia kazí, mimi nitaongelea sana kuhusu suala la wahudumu wa afya. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna changamoto kubwa sana. Nalipigia sana kelele hili kwa sababu katika Wilaya ya Kibondo kuna ongezeko la watu zaidi ya 200,000 ambao tunalazimika kuahudumia katika suala la...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha
kwa muda wa mzungumzaji)*

NAIBU SPIKA: Muda wako umekwisha Mheshimiwa.

MHE. ENG. ATASHASTA J. NDITIYE: Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge, nilikuwa nimemtaja Mheshimiwa Mbaraka Dau na Mheshimiwa Angelina Malembeka, lakini naona muda wetu utaruhusu Mbunge mmoja tu kuchangia. Mheshimiwa Angelina Malembeka; mchana tutaanza na Mheshimiwa Dau.

MHE. ANGELINA A. MALEMBEKA: Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kuingia katika kikao hiki cha bajeti kwa awamu hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naunga mkono hoja za Mawaziri wote wawili kwa asilimia mia moja. Nachukua pia nafasi hii kuwapongeza Mawaziri wote wawili pamoja na Naibu na *team zao* zote wanazofanya nazo kazi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, michango yangu itakuwa michache na nitajaribu kuitoa kwa ufupi sana. Nianzie na mpango wa MKURABITA. Nachukua nafasi hii kuipongeza Serikali yangu ya Chama cha Mapinduzi kwa kazi nzuri sana wanayoifanya. Nimepita miradi mbalimbali ya MKURABITA na nimeona jinsi gani wananchi walivyohamasika na jinsi walivyokubaliana na shughuli ya MKURABITA na hivyo kuweza kumiliki ardhi na kuwa na hati ambazo zinawezesha kupata mikopo katika taasisi za fedha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naishauri Serikali yangu kwa kuwa wananchi wameridhia ni vyema kabisa kwamba kwa sasa hivi shughuli hii iende moja kwa moja nchi nzima kwa kuangalia Majimbo ili kila Jimbo angalau tuwe na mfano mmojawapo wa kufanyia hii kazi. Nimeona akinamama jinsi

walivyopata hati za kumiliki ardhi pamoja na vijana, kwa hiyo, nashukuru na naiomba iendelee kufanya kazi vizuri. (Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye suala la TASAF, nimepita katika miradi mbalimbali nimeangalia, nimeona TASAF jinsi ilivyofanya kazi vizuri na kuwezesha watu wenyewe kipato kidogo kuweza kujenga nyumba, kupeleka watoto wao shule na kuwanunulia *uniform*, lakini pia na kubuni miradi mbalimbali ambayo imewawezesha kuongeza kipato.

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme tu kwamba, kwa wale Watendaji wachache ambao hawakuwa wema, wakaamua kuvuruga utaratibu huu, nafahamu kwamba wamechukuliwa hatua, lakini ni vyema Mheshimiwa Waziri atakapokuja hapa, atuambie wale watendaji ambao kwa makusudi wameamua kuvuruga utaratibu huu wamechukuliwa hatua gani? Badala ya kuwalazimisha wananchi walipe pesa ambazo hawakuziomba. Wale waliowajazia ndio walikuwa na matatizo. Kwa hiyo, tuwanusuru wale ambao wanalipishwa fedha ambazo hawana uwezo wa kulipa, tuwashughulikie wale waliowaandikisha. (Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, nije katika Mfuko wa Rais wa Uwezeshaji. Mfuko huu umefanya kazi vizuri sana, nampongeza Mheshimiwa Waziri na *team* yake yote, kwa sababu vikundi vya vijana ambavyo vimewezeshwa na Mfuko huu vimefanya kazi vizuri, lakini fedha zile zinazotolewa zimekuwa chache. Ni vizuri tuangalie uwezekano wa kuwaongeza ili waweze kufanya kazi na kujajiri wenyewe. Kwa sababu katika vikundi nilivyopitia, nimekuja kugundua kwamba siyo wote ambao elimu yao ni ndogo, wapo ambao wana elimu kubwa, wamejiunga na wamewachukua wenyewe elimu ndogo na kufanya mradi wa pamoja hivyo kuweza kuajiriana wenyewe kwa wenyewe. Kwa hiyo, nawapongeza. (Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie pia suala la TAKUKURU. TAKUKURU imefanya kazi nzuri, japo watu

wanabeza. Kwa sasa hivi suala la rushwa limepungua, kwa kiasi kikubwa na kama Mheshimiwa Waziri alivyoelezea, wameweza kuokoa mamilioni kadhaa kutokana na mchakato uliofanywa katika kukagua na kutenda kazi zao. Ninachoshauri, fedha zile mmeeleza zimeenda Serikalini, lakini hatujaambiya zimeenda kufanya nini? Naomba Mheshimiwa Waziri atakapokuja hapa atuambie fedha hizo walizookoa zimeenda kufanya nini? Kwa sababu bado tuna matatizo kwa wananchi, fedha hizo zinaweza zikatumika kwa ajili ya kazi nydingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, nzungumzie kidogo suala la Usalama wa Taifa. Suala la Usalama wa Taifa ni suala nyeti na kama ni suala nyeti, naona kuna watu wanalifanyia uzembe uzembe tu. Mtu anaamka asubuhi, anatuma *message*, nimetekwa nyara. Hivi kutekwa nyara mchezo! Mnatania suala la kutekwa nyara! Yaani mtu anatuma *message*, "nabadilisha nguo, naenda Polisi, nimetekwa nyara. Huko kutekwa nyara, mbona mnaifanyia utani taasisi hii! (*Kicheko/Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mtu ananyanyuka, anasema Wabunge 11 watatekwa nyara; yeye alikaa nao vikao akawajua hao Wabunge 11! Naomba Usalama wa Taifa kwanza wawanyanyue wale waliosema kuna Wabunge 11 humu watatekwa nyara, watutajie ni akina nani? Walikaa wapi? Wanatekwa nyara kwa kosa gani? Kwa sababu Usalama wa Taifa, mimi nategemea mpaka tumekaa hapa, ni kwamba wako kazini na wanafanya kazi vizuri. Ni vizuri basi wakaongezewa fedha katika idara yao, wapate mbinu mpya za kufanya kazi, waongezewe vifaa tuweze kupata usalama zaidi.

Mtu kutwa, anaamka asubuhi anatuma *message* kwa rafiki yake, "nimetekwa nyara." Hebu waulizeni waliotekwa nyara, hiyo simu unaipata wapi ya kutuma hiyo *message*? Kutekwa nyara mchezo! Hebu waulizeni wanaotekwa nyara, watakwambieni ukweli. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, huu mchezo wale wanaojifanya usalama *fake*, naomba Mheshimiwa Waziri unayehusika washughulikie. Kwa sababu sasa hivi mtu akishakata panki lake, akavaa kaunda suti yake, anatoa kitambulisho; mimi Usalama wa Taifa. Usalama wa Taifa mchezo! Mtu amejizungusha zungusha tu huko, anawatisha watu mtaani, anasema Usalama wa Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa wale ambao wanajifanya Usalama wa Taifa na kuwahenyesha watu mtaani, washughulikiwe. Wale wanaojifanya Usalama wa Taifa, kutoa *data za uongo*, washughulikiwe; sambamba na *data za uongo za kwenye mitandao*. Tumechoka! Nchi iko juu juu; watu tuko juu juu tunahangaika! Usalama wa Taifa wapo, mnawanyanyapaa; hebu fanyeni kweli; na tuanzie humu humu ndani. (*Kicheko/Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mtu anasema hapa ushahidi ninao, usalama wa Taifa upo, hamjamchukua mpaka leo kuja kukwambieni Mbunge gani aliyetekwa nyara; mnawachaka tu, kwa nini?

Mheshimiwa Naibu Spika, nichangie suala la utawala bora nikienda sambamba na maadili ya viongozi. Tumekaa muda mrefu tukizungumzia Ma-DC, Ma-RC tunajisahau sisi humu ndani. Maadili tuanze nayo sisi wenyewe na uongozi tuanze nao sisi wenyewe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kukaa humu ndani miaka 30 au miaka mitano; kama toka mwanzo wamekuja na mpango wako wa kutukana, utafikiria utaratibu wa huku ni wa kutukana. Naomba semina hizi zianze pia na kwa Wabunge ili tuweze kuwasimamia wenzetu. Kama semina hizi watu watapata, kila mtu atajua wajibu wake ni nini, mamlaka yake na madaraka yake yanaishia wapi? Hatutazozana na DC, RC na wala wao hawatazozana na Wabunge. Isipokuwa kwa sababu semina hizi hazipo, ndio maana kila mtu anajiona yeye kubwa kuliko.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunao Ma-RC, Ma- DC wazuri sana, wanafanya kazi vizuri sana; lakini wale baadhi ambaao wanakosea ni sawasawa na baadhi ya Waheshimiwa Wabunge walioko humu wanaofanya kusudi. Kuna wakati nilisema tupimwe akili, watu wakacheka, lakini tunakoelekeea itafika wakati watu watapimwa akili humu ndani. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu yanayofanyika huku unajiliza kweli huyu kiongozi, wanafikiria kujaza zile *form* za maadili ndiyo maana yake umemaliza maadili ya viongozi...

MHE. HAMIDU H. BOBALI: Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

MHE. ANGELINA A. MALEMBEKA: ...kumbe ni pamoja na matendo tunayoyafanya.

MHE. HAMIDU H. BOBALI: Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Malembeka, kuna taarifa unataka kupewa huko na Mheshimiwa Bobali.

MHE. ANGELINA A. MALEMBEKA: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru, naisubiri.

TAARIFA

MHE. HAMIDU H. BOBALI: Mheshimiwa Naibu Spika, sisi wengine tulisimama kwenye majukwaa tukaomba kura tuje tuwatumikie wananchi. Hadhi ya Bunge...

MBUNGE FULANI: Kanuni gani? Mbona hasemi?

MHE. HAMIDU H. BOBALI: Wewe mwenyewe unayeongea, mbona hujaruhusiwa na Naibu Spika?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Bobali, umeomba kutoa taarifa, kwa hiyo toa taarifa.

MHE. HAMIDU H. BOBALI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Mbunge anayechangia amesema kwamba Usalama wa Taifa waanze na Wabunge waliopo humu ndani waliota taarifa kwamba wako hatarini kutekwa. Nafikiri ni kulishusha hadhi Bunge. Maongezi yanayoongelewa Bungeni kwa mujibu wa Katiba ya nchi, hayahojiwi popote. Labda leo Mheshimiwa Naibu Spika ukubali kwamba Bunge lako sasa hoja za humu ndani zote tuwape mamlaka Usalama wa Taifa, Polisi au ye yote aweze kuhoji hoja za Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, hiyo...

MBUNGE FULANI: Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Deo Sanga, naomba ukae tafadhali. Mheshimiwa Malembeka unaipokea taarifa hiyo?

MHE. ANGELINA A. MALEMBEKA: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naomba unitunzie muda wangu. Pili nataka kumwambia anayeongea, hiyo taarifa yake siipokei. Kwanza naona kazuka tu! Kwa sababu suala la Usalama wa Taifa, imeitwa Taifa; haijaambiwa wa chama wala wa idara fulani. Ina maana hapa tulipo wenyewe wapo na wanafanya hiyo kazi. Kama ye ye anafikiria kwamba anaweza akafanya mambo yake halafu asijadiliwe, ndiyo maana mnaitwa mnahojiwa. Ingekuwa hivi hivi, humu ndani kusingekuwa salama. Iko siku humu ndani mtu angetoka vichwa vingebaki humu; lakini kwa sababu watu wapo na wanatulinda, ndiyo maana mnaona amani ipo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka niseme kwamba, suala la Usalama wa Taifa wasilichukulie mchezo, mchezo. Watu wana-*support* tu; wakisikia fulani katekwa nyara, hata kwa *message* wanakubali. Ninachosema ni kwamba, tunaomba amani iwepo na ninaendelea kusisitiza wale Wabunge waliosema wanawajua 11 wapo, watutaje;

inawezekana labda na mimi nimo, njue ni jinsi gani ninavyojilinda. Hawawezi kusema halafu wakaachwa na wamesema wanao ushahidi. Mmeona! (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme kabisa, asubuhi tunaingia hapa tunaomba dua, tunawaombea na viongozi wetu na Rais tunamwombea; baada ya dakika kumi, wanamtukana halafu wanasema hashauriki. Sasa hata ungekuwa wewe, huyo mtu anakudharau, anakutukana, unamwita akushauri nini? Kwa sababu kinachotakiwa hapa Wabunge tumepewa nafasi ya kuishauri Serikali na kuisimamia. Muda tunaopewa kuishauri Serikali na kuisemea, hatufanyi hivyo, tunaikashifu na kuitukana, halafu mkihojiwa mnasema kuna kanuni. Kuna haja ya kuja kubadilisha hizi kanuni ili watu tuheshimiane vizuri humu ndani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema kwamba kama suala la kuheshimiana, tunavyoapa hapa, tunajaza *form*, tuendelee kuheshimiana na tumheshimu kila mtu kwa nafasi yake. Mheshimiwa Rais sio mtu wa kumtukana; asubuhi huwezi ukamwombea dua, mchana unamtukana, wajirekebishe.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilisema siku moja kwamba nyoka wa kijani huwa haumi, siku akiuma hana dawa. Sasa yule nyoka kaanza kufanya kazi; wakiitwa kuhojiwa wanasema wametekwa nyara. Hatuteki nyara mtu! Mnatakiwa mkatoe maelezo kwa nini mnatukana? Ujilize, kwa nini kila siku unahojiwa wewe? Jiulize, kwa nini kila siku unaitwa wewe? Polisi? Ukishapata jibu utanyamaza.

Mheshimiwa Naibu Spika, namalizia kwa kusema kwamba naungana na wenzangu wote wanaotetea Madiwani posho zao ziongezeke.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja, ahsante. (*Kicheko/Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Deo Sanga.

MWONGOZO WA SPIKA

MHE. DEO K. SANGA: Mheshimiwa Naibu Spika, n似mama kwa kanuni ya 68 (7) pamoja na 64(a) (b) na (c).

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu ya muda. hizi zote nilizozitaja siwezi kuzisoma.

MBUNGE FULANI: Soma.

MHE. DEO K. SANGA: Aliyepewa ridhaa akisema n似ome, nitasoma. Kwa hiyo,....

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Deo Sanga, ongea na mimi tafadhali.

MHE. DEO K. SANGA: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, pamoja na kanuni hizi zote nilizozisema, yameongelewa leo mambo hapa yanayohusiana na Mahakama; yameongelewa mambo mengine yanayohusiana na Usalama wa Taifa na kadhalika; yanahusiana juu ya mauaji kutekwa na kadhalika; nadhani kupitia kanuni hizi, naomba mwongozo wako ni nini kazi ya Bunge?

Mheshimiwa Naibu Spika, nimesema kwa sababu nimezipitia kanuni hizi, nimeona tunakwenda kinyume, ndiyo maana nimeomba mwongozo wako. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tumefika mwisho wa uchangiaji kwa asubuhi. Nitawasoma hapa majina watu tutakaoanza nao mchana, baada ya maelezo yafuatayo:-

Nianze na hili la mwisho la Mheshimiwa Deo Sanga kuomba mwongozo kuhusu mambo ambayo yametajwa humu ndani. Mheshimiwa Sanga ameomba mwongozo huo kwa mujibu wa kanuni ya 68(7) ametaja kanuni ya 64(1) (a) (b) na (c).

Waheshimiwa Wabunge, mtakumbuka kwamba jambo hili kwa mara ya kwanza lilizungumziwa humu ndani kwa kutumia kanuni ya 47. Maombi hayo yalikuwa kwamba tujadili hayo ambayo Mheshimiwa Sanga ameyasema.

Mheshimiwa Sanga, kuna mambo mawili katika yale aliyojasema, nianze kwa kuyatoa yale ambayo yalishatolewa kwenye hotuba, kwa hiyo, kama yalitokeza leo kwenye mijadala, pengine hayakuwa yamesikika vizuri kwenye kitili ili yaweze kutolewa maelezo. Suala kuhusu Mahakama lilishatolewa kwenye kumbukumbu za Bunge. Yaani, taarifa iliyokuwa imetolewa kuhusu Mahakama kuingiliwa ilikuwa imeshaondolewa kwenye taarifa za Bunge.

Hili lingine pia kwa mujibu wa kanuni hiyo uliyosema ya 64(c). Waheshimiwa Wabunge, ukiisoma hili kanuni, mambo ambayo yalikwishaletwa hapa Bungeni ili jambo hilo liweze kurudi tena unapaswa uliletwa kwa hoja mahususi. Sasa nadhani pengine Mheshimiwa Sanga amekuwa akifuatilia jambo ambalo likiwishaamriwa na kiti kwamba lifuate utaratibu wa kisheria, Waheshimiwa Wabunge tumekuwa tukienda mbele na nyuma, tunalirudisha kwa namna ambayo mtu analizungumza wakati akichangia. (*Makofii*)

Waheshimiwa Wabunge, jambo hili lilikuja mahususi chini ya kanuni ya 47 na likakataliwa kwa sababu linao uwezo wa kushughulikiwa kwa kutumia sheria na ndivyo kanuni yetu ya 48 inavyosema. Kwa hiyo, tutumie zile sheria; na Bungeni hapa kanuni ya 64 inatutaka tukitaka kurejesha jambo kama hilo, tulete hoja mahususi.

Waheshimiwa Wabunge, Bunge hili la bajeti kwa sababu ambazo wote tunazijua, sina haja ya kuzirudia jambo hili la kuongelea Usalama wa Taifa limekuwa likijirudia sana, lakini huu si utaratibu ambao pengine ulizoeleka huko nyuma, ila Bunge hili limekuja na jambo hili kana kwamba tunaweza kukaa humu ndani tukaanza kujadili mambo kadhaa ambayo huko nyuma hayakupata kujadiliwa.

Sasa kwa kuwa hizo sheria sina hapa, lakini pamoja na kwamba hili ni Bunge, yako mambo ambayo ni kazi yetu kufanya, yako mambo ambayo ni kazi ya vyombo vingine kufanya. Kwa sababu nimesema hizo sheria sina hapa, hata Bunge siyo kwamba lenyewe linaruhusiwa kuongelea kila jambo kwa kuwa ni Bunge, hapana.

Mheshimiwa Naibu Spika, yako mambo ambayo sheria tulizotunga wenyewe, hata sisi wenyewe tumejifunga kuzungumzia mambo hayo. Kwa sababu hiyo, kwa kutumia Kanuni ya (5) ya kanuni zetu za Bunge na Kanuni ya 64 (1)(c) nimeshaisoma, kama mtu ataleta hoja hiyo mahususi anaruhusiwa na kanuni hizi, lakini kwa kuwa hoja hiyo haiko mezani mahususi, kwa kutumia Kanuni ya (5) suala la mjadala kuhusu Usalama wa Taifa, linaishia hapa kwa leo. (*Makofii*)

Kwa hiyo, hilo ni jambo la kwanza alloomba Mheshimiwa Sanga na mwongozo wangu ni huo, kwamba hilo suala la kuongelea Usalama wa Taifa humu ndani kana kwamba ni kitu kidogo sana, linakwisha hapa mpaka mtu mwingine atakapoleta hoja mahususi kuititia kanuni zetu zinavyotuambia. (*Makofii*)

Waheshimiwa Wabunge, lingine nalo ni la kikanuni; Kanuni yetu ya 147, nataka tu nisisitize kwa sababu tunaendelea na mjadala. Kanuni zinatutaka tujitahidi kutumia lugha mojawapo, nyingine ni pale unaponukuu. Ni sawa, mtu anaweza akasema neno moja wakati wa mchango wake, lakini mchango mzima ukijaa mchanganyiko wa lugha mbili ama tatu tofauti, maana zake ni mbili tu. Kwa kuwa mimi nilikuwa Mwalimu kama Mheshimiwa Bilago pale, ni mbili; moja kati ya hizo lugha mbili hakuna hata moja unayoijua, ndio maana yake; au ya pili kwa kuwa mara nyingi tunazungumza Kiswahili humu ndani, maana yake lugha yetu wenyewe haijitoshelezi. (*Makofii*)

Sasa tusifanye hivyo kwa sababu Kiswahili ni lugha yetu ya Taifa. Unapokuwa unaiongezea maneno kila wakati ni kana kwamba hakuna hayo maneno ya hiyo lugha jamani, si tunayo, nasi tunaitetea hii lugha! Sasa hatuwezi kujikuta

mazingira ambayo wenyе lugha zao wakizungumza, wanazungumza lugha zao mwanzo mpaka mwisho. Sisi hatutumii ya kwetu, hata hiyo ya wageni tuliyoruhusiwa na kanuni, hatutumii pia. Kwa hiyo, mchanganyiko wa neno moja, mawili ni sawa, lakini huwezi kuweka mchango wako sentensi moja hatujui unazungumza Kiswahili ama unazungumza Kiingereza. Kwa hiyo, tuzingatie kanuni ya 147. (*Makofi*)

La mwisho Mheshimiwa Halima Mdee ambaye ni Kapteni wa *Bunge Netball Team* anawatangazia Wabunge wote wanawake kwamba tarehe 26 mwezi wa Nne, 2017 kuna Mechi ya *Netball* na Baraza la Wawakilishi. Sasa Mheshimiwa Halima Mdee anasema hivi, ushiriki wenu ni muhimu sana na mwaka huu mlishtangaziwa wakati Bunge likianza kwamba safari hii mashindano ya Afrika Mashariki yanakuja Tanzania, sisi ndlo wenyejи. Kwa sababu hiyo Kapteni yuko katika harakati za kusuka kikosi kazi kwa ajili ya kuchukua kombe la Mabunge ya Afrika Mashariki. Sasa anawatangazia kwamba mazoezi yanaanza rasmi kesho katika viwanja vya Dodoma Sekondari.

Waheshimiwa Wabunge, tangazo hili ni muhimu sana kwa sababu Naibu Spika mwenyewe anamsikiliza Kapteni wake. Sasa ili upate namba ya kucheza, lazima uende kwenye mazoezi, kwa hiyo, Kapteni naamini nimefikisha salama nisije nikaadhibiwa uwanjani. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, nimekumbushwa hapa niwasome watakaoanza mchana. Mheshimiwa Mbaraka Dau, Mheshimiwa Leah Komanya, Mheshimiwa Almas Maige, Mheshimiwa Hassan Masala, Mheshimiwa Edwin Sanda, halafu Mheshimiwa Suzan Limbweni Kiwanga, Mheshimiwa Joshua Samwel Nassari; hao kwa sababu sio wengi niwasome wote.

Wengine ni Mheshimiwa Jesca Davidi Kishoa, Mheshimiwa Paschal Haonga, Mheshimiwa Hamidu Hassan Bobali, Mheshimiwa Halifa Mohamed Issa na Mheshimiwa Salma Mwassa.

Waheshimiwa Wabunge, hawa niliowasoma watachangia mchana, lakini kwa upande wa Chama cha Mapinduzi sijataja Wabunge wote kwa sababu idadi yao itakuwa kubwa kwa kuangalia uwiano. Kwa hiyo, hawa niliowasoma tutaanza nao mchana.

Baada ya kusema hayo, nasitisha shughuli za Bunge mpaka saa kumi na moja jioni leo.

(Saa 7.08 Mchana Bunge lilsitishwa hadi saa 11.00 Jioni)

(Saa 11.00 Jioni Bunge lilirudia)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tukae. Tunaendelea na majadiliano. Tutaanza na Mheshimiwa Mbaraka Dau, atafuatiwa na Mheshimiwa Leah Komanya na Mheshimiwa Almasi Maige ajandae.

Mheshimiwa Dau hayupo; namwita Mheshimiwa Leah Komanya.

MHE. LEAH J. KOMANYA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipatia nafasi hii ili niweze kuchangia hoja ya Wizara ya TAMISEMI pamoja na Utumishi; Utawala Bora.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza napenda kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa kazi nzuri anazozifanya. Wananchi wa Mkoa wa Simiyu wanamuunga mkono Mheshimiwa Rais kwa kazi zote anazozifanya za kupambana na wote wasio na nia nzuri na nchi. Hii yote imejidhihirisha katika ziara yake aliyofanya mapema mwezi wa Kwanza katika Mkoa wa Simiyu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naendelea kumpongeza na kumshukuru Mheshimiwa Rais kwa kutuzindulia Kiwanda cha Chaki kilichopo Maswa Mkoani Simiyu. Katika uzinduzi wake, alitujengea mazingira ya kuona namna ya kuweza kupanua kiwanda hicho na tayari sasa hivi kiwanda hicho kitapanuliwa kwa kushirikiana na Halmashauri pamoja na *TIB*. Naomba niwajulishe tu kwamba chaki za Maswa ni nzuri; na vijana

wako hapa Dodoma kwenye maonesho wanazo hizo chaki. Kwa hiyo, nawaombeni Waheshimiwa Wabunge mfike mzione ili muweze kununua katika Halmashauri zenu na kukuza uchumi wa vijana wa Maswa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naendelea kumshukuru Mheshimiwa Rais kwa kutuzindulia barabara ya lami ya kutoka Lamadi mpaka Bariadi yenyе kilometa 71, kuweka jiwe la msingi katika ujenzi wa barabara ya lami kutoka Mwigumbi mpaka Maswa yenyе kilometa 52. Mheshimiwa Rais alipokuwa Mkoani Simiyu aliahidi sasa utekelezaji wa ujenzi wa lami wa barabara ya Maswa mpaka Bariadi yenyе kilometa 50 uanze. Hivi sasa ninavyoongea, mchakato wa kumpata Mkandarasi unaendelea. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitoe ushauri upande wa Serikali. Nimeshuhudia miradi mingi mikubwa wakati ikitekelezwa, wakandarasi wamekuwa wakija na vijana kufanya kazi ambazo zingeweza kufanywa na vijana ambaao wanatoka pale pale. Wakandarasi wengine wameweza kuthubutu kuja hata mpaka na unga kwenye eneo analoweza kufanyia kazi. Naomba Serikali isaidiane na wakandarasi, kuwatumia vijana wa eneo hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa mradi ule utatekelezwa katika Wilaya ya Bariadi, Itilima na Maswa, wachukue vijana wa kutoka pale kwa sababu nina imani wanazo nguvu na ni waadilifu. Pia wanunue bidhaa zinazotokea katika maeneo yale. Kuna samaki wazuri wanapatikana katika soko la Bariadi ambaao wanavuliwa katika Ziwa Victoria Wilaya ya Busega; kuna nafaka nzuri inatoka Wilaya ya Itilima; na mchele mzuri unaotokea katika Wilaya ya Maswa. Nawakaribisheni sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, niendelee kwa kusema, Mheshimiwa Rais wakati anafanya kampeni zake mwaka 2015, alipokuwa Wilayani Meatu aliawaahidi wananchi kwamba atawawezesha kujenga nyumba bora kwa kupunguza bei ya vifaa vya ujenzi. Hapa ninapoongea, mfuko mmoja wa saruji Wilayani Meatu ulikuwa unauzwa shilingi

20,000/=, lakini kwa sasa hivi unauzwa shilingi 16,000/=; lakini bei hiyo bado iko juu ukilinganisha na wilaya za jirani. Hii inatokana na kwamba simenti inapokuja, ni mpaka ifike Shinyanga halafu ianze kurudi tena kuja Wilaya ya Meatu. Changamoto ya kutatua mzunguko wa usafiri huu ni ukamilishaji wa ujenzi wa Daraja la Mto Sibiti. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nafahamu daraja hilo linatekelezwa na *TANROAD*, Singida, lakini vikao vya Mfuko wa Barabara vya Mkoa wa Simiyu toka mwezi wa Tisa tumekuwa tukiahidiwa kwamba, vifaa viko China vinatengenezwa, leo yapata miezi saba, vifaa vile havijaletwa. Tunaomba basi ujenzi huu uharakishwe, vifaa hivyo viletwe ili daraja hilo liweze kufungua milango ya biashara kwa Mkoa wa Simiyu, hususan Wilaya ya Meatu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara hiyo itakapoanza kazi, itasaidia wananchi. Mwananchi anapoondoka Meatu kwa kupitia Shinyanga, anatumia sh. 95,000/= kwa sababu inabidi aende Shinyanga, alale Shinyanga kesho yake asafiri. Kwa kutumia daraja la Mto Sibiti pale, atatumia sh. 45,000/= kufika Dar es Salaam. Kwa hiyo, ataokoa sh. 50,000/= pamoja na siku moja ambayo angeweza kutumia katika shughuli nytingine. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichangie upande wa maji. Katika hotuba ya Waziri wa TAMISEMI amesema kwamba Serikali imeunda vyombo vya utumiaji maji *COWSO*, vipatavyo 1,800 kwa ajili ya usimamizi na uendelezaji wa vituo vya maji, ili kuhakikisha miradi hiyo inakuwa endelevu. Mimi nikiwa Mjumbe wa Kamati ya *LAAC*, tumekuwa tukitembelea miradi hiyo, tumeona changamoto mbalimbali katika uendeshaji wa hiyo miradi iliyokabidhiwa kwa wananchi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati zile hazijajengewa uwezo namna ya uendeshaji wa miradi hiyo. Kamati hizo hazijui hata namna ya utunzaji wa fedha, namna ya kupokea mapato, hazina hata '*O*' and '*M*' Accounts (*Operation and*

Maintenance Account), kiasi kwamba tatizo likitokea wanapaswa wachukue fedha ili mradi uendelee. Matokeo wamekuwa wakichangishana fedha kienyeji na kusababisha hata ile gharama kwa ndoo kuwa kubwa. Tunaomba vyombo vile viwezeshe ili viweze kuendesha miradi hiyo ya maji. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalizie mchango wangu kwa 5% ya wanawake na vijana. Ni kweli Halmashauri zimekuwa zikitenga fedha kwa ajili ya kuwawezesha akinamama na vijana, lakini Halmashauri zimekuwa zikiishia kutenga tu bila kutoa michango ile kwa akinamama. Kwa kuwa michango hiyo haiko kisheria, ni waraka tu unaotumika, wakati tukiwa mbioni kuandaa sheria, nashauri ili utekelezaji ufanyike vizuri, basi ajenda hii ya mchango iwe ya kudumu kwenye vikao vya RCC ili Mkuu wa Mkoa na Kikao chake aanze ye ye kwanza kufuatilla badala ya kusubiri Kamati ya LAAC ndio ije kwanza ionekane kwamba ule mchango ndio kwanza wameuona. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hayo machache, naunga mkono hoja. (Makofi)

NAIBU SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Almas Maige, atafuatiwa na Mheshimiwa Hassan Masala na Mheshimiwa Edwin Sannda ajiandae.

MHE. ALMAS A. MAIGE: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa muda huu nami niweze kuchangia hotuba ya Mawaziri wa Nchi katika Ofisi ya Rais; Waziri wa Nchi wa TAMISEMI na Waziri wa Nchi, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwanza kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa kazi yake nzuri anayoifanya katika kutekeleza wajibu wake na katika kuendesha nchi yetu ili wananchi tuweze kuwa na amani na tuweze kukuza uchumi wetu. Sisi Wanyamwezi tunapenda

sana kupongeza jambo kwa kushangaa na maneno yetu ya kushangaa ni mawili tu, yaani 'ish!' na 'jamani!' (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Rais ametushangaza sana na tunamwona wa ajabu. Kwa mfano, Mheshimiwa Rais kanunua ndege mbili, sisi tukashangaa, *ish!* Pia, Mheshimiwa Rais amegundua wafanyakazi hewa wengi, tukasema, jamani! Mara tumesikia Mheshimiwa Rais huyu huyu anajenga reli ya *standard gauge*, tukasema, *ish!* Kapata wapi hela? Hatujakaa vizuri, Mheshimiwa Rais huyu huyu akasema tunahamia Dodoma, jamani! Wote tuko Dodoma! (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, upande wa UKAWA kule wamekosa maneno mazuri ya kumpongeza, lakini na wao pia wanashangaa. Wanamshangaa kwa mazuri anayoyafanya katika kutekeleza majukumu, wanabaki kusema Rais wa ajabu, kama ambavyo sisi tunasema Rais wa ajabu kwa mambo mazuri anayoyafanya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ziko fujo zinazolalamikiwa na dawa hiyo ya kulalamikiwa fujo hizo, mimi niliileta katika Mkutano wetu wa Pili wa Bunge hili la Kumi na Moja. Nilileta kwa Mheshimiwa Spika Muswada wa Sheria wa Sekta ya Ulinzi Binafsi. Sheria ile ingeweza sana kutibu mambo ambayo tunayaona sasa. Vikundi mbalimbali vinavyojitokeza sasa ni kwa sababu hakuna sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani alete sheria hiyo haraka ili tuweze kudhibiti vikundi ambavyo vinafanya fujo kwa wananchi, vinapiga na kukaba watu. Serikali na Waziri wa Mambo ya Ndani, kama nilivyosema, ni budi alete sheria hiyo ili tuweze kudhibiti matukio ambayo yanatokea sasa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naomba nichagie ukurasa wa 65 wa hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Nchi katika Ofisi ya Rais, kuhusu TAMISEMI. Katika DCC ya Wilaya ya Uyui pamoja na Halmashauri na Baraza la Ushauri la Mkoa

(RCC) tuliomba jina la Halmashauri ya Uyui libadilishwe kutoka *Tabora District Council* liwe *Uyui District Council*. Jambo hili linachanganya wakati wa maagizo ya kiserikali kutoka Serikali Kuu, lakini pia tumeshuhudia fedha za Wilaya ya Uyui, Halmashauri ya Uyui, zikienda Manispaa ya Tabora. Kwa hiyo, mikutano yote miwili ya Wilaya pamoja na ya mkoa ililetia maombi kwa Waziri anayehusika na TAMISEMI ya kubadilisha jina. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba atakapokuja Mheshimiwa Waziri hapa kujadili kufikia mwisho wa majumuisho yake, asiache kueleza kwa nini Halmashauri ya Uyui isiiitwe Halmashauri ya Uyui badala ya Halmashauri ya Tabora? Kwa sababu hatuhitaji bajeti ya hela. Ni maombi yetu sisi wananchi wa Uyui na yeye ni kutoa kibali tu. Kwa hiyo, sidhani kama itakuwa tatizo kwa Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI kutukubalia ombi letu hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile naomba nichangie kwenye Kifungu cha 33 kuhusu uboreshaji wa huduma za afya. Halmashauri ya Uyui na Wilaya nzima ya Uyui haina Hospitali ya Wilaya. Kwa hiyo, tunategemea kituo kimoja cha afya ambacho hakifanyi kazi vizuri na hakiwezi kufanya upasuaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru Naibu Waziri wa Nishati ambaye amenisaidia kupeleka umeme pale; umeme tunao sasa, lakini hatuwezi kufanya upasuaji kwa sababu ya matatizo makubwa. Hicho ndicho kituo pekee cha afya katika Jimbo langu na katika Wilaya nzima ya Uyui. Kwa hiyo, tunaomba Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI aje na msaada wa kusaidia kituo kile na hatimaye kusaidia majengo yanayojengwa na Halmashauri ambayo yamejengwa kwa hela ya ndani ili tuweze kuyamalizia na tupate Kituo cha Hospitali ya Wilaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza sana Serikali, hasa Wizara ya TAMISEMI kuanzisha Mfuko au kuanzisha Kitengo cha Barabara, Uwakala wa Barabara Vijijini. Wilaya yangu ni mpya na Jimbo langu ni jipya, hatuna barabara za

ndani kabisa. Tuna barabara ambayo ni lazima utoke barabara kubwa uende mjini, huwezi kwenda katika kijiji kingine. Hakuna barabara! Kwa hiyo, tumefurahi sana kusikia kwamba mwezi wa saba Serikali itaanzisha Wakala wa Barabara Vijijini. Tuna imani kwamba wakala huyu atafanya kazi sawasawa na Wakala wa *TANROADS*ambaye anafanya kazi nzuri. Wakiiga hivyo, basi Jimboni kwangu kutakuwa na barabara za kutosha ili kusafirisha mazao na kuweza kuwasiliana. Nina imani kwamba wakala huyu atakuwa ndiye kichocheo. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho niongelee mambo ya utawala bora. Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais kuhusu mambo ya Utawala Bora, watu wengi, Wabunge wengi humu ndani na wananchi kule nje, wanalamika sana kuhusu mpango mzuri ulioanzishwa wa *TASAF*. Kwetu umesaidia sana. Tulipoanza mpango huo ulifanya kazi nzuri sana, lakini baadaye mpango umekuja kuwafuta watu waliokuwa wamepewa hela; wanatakiwa wazirudishe kwa madai kwamba wamekosewa kupewa hizo hela, hawamo tena katika sifa za wanaopokea hela. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo hili limeleta mgongano mkubwa sana. Wengine wameomba Wabunge tuwasaidie, nasi hatuna hizo hela, lakini pia wananchi hawana hizo hela kuzirudisha tena. Kosa lillolofanywa na *TASAF* lisahahihishwe kwa Maafisa wa *TASAF*na siyo kusahihishwa kwa wazee. Wazee wengine wanaotaka kurudisha hela, kwa kweli, ukimwangalia hivi ni maskini na hawana uwezo kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Mheshimiwa Waziri mhusika mwenye jukumu hilo atakapokuja kufanya majumuisho yake, aeleze tutafanyaje kuondoa matatizo ya wazee kuwaomba hela ambayo tuliwapa sisi wenyewe?

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga hoja mkono na nakushukuru sana kwa kuniruhusu kuchangia katika Wizara hizi mbili. (*Makofî*)

NAIBU SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Hassan Masala. Hayupo; Mheshimiwa Edwin Sannda atafuatiwa na Mheshimiwa Ikupa Stella Alex, halafu Mheshimiwa Susan Kiwanga ajandae.

MHE. EDWIN M. SANNDA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipatia fursa hii ya kuchangia kwenye hotuba ya bajeti ya TAMISEMI, Utumishi na Utawala Bora. Kwanza kabisa nawapongeza kwa kuwasilisha hotuba nzuri na kuwasilisha mpango wa bajeti mzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia siyo vibaya na ni muhimu tukaweza kutoa maboresho pale ambapo panaonekana panahitaji kuboreshwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nitaanza na eneo la kujenga uwezo kwa maana ya mafunzo. Nimemsikia kaka yangu Mheshimiwa Simbachawene namna alivyoliweka; tunaelewa mlipotoka, tunaelewa maana yake, lakini nataka niseme, mafunzo ya kujenga uwezo ni jambo muhimu sana. Hata ukiwa umesoma namna gani, una *Ph.D*, umetoka umewiva, una *experience* nzuri kabisa kwenye eneo lako la kazi, lakini kujifunza ni dhana endelevu. Utajifunza mpaka siku ya kwenda kaburini. (*Makofii*)

Sasa tunaposema kwenye baadhi ya maeneo kwamba tumechagua watu au tumeteua watu ambao wamekwishawiva, nafikiri pale kidogo tunahitaji tulitafakari upya. Nashauri, jambo hili la wenzetu Wazungu, wanasema "*learning is a continuous process.*" Mpaka siku ya mwisho utaendelea kujifunza tu, hautafika mahali ukasema wewe umekamilisha, unajua kila kitu, haiwezekani. Ni lazima tuendelee kujifunza. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, napendekeza kwamba Wizara, kwa maana ya Serikali, bajeti ya kujenga uwezo iendelee kuwepo na izingatiwe sana. Taifa ambalo halijifunzi, hili litakuwa ni Taifa la namna gani? Kweli mtu anasema nimeshamaliza kujuu! Haiwezekani. Ndiyo maana

wakati mwingine tunakutana na changamoto za makosa madogo madogo ambayo yangeweza kuepukika kuitia *capacity building*. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nisisitize sana, nimeona kuna bajeti kidogo kwa wale ambao wengine wanawaita maarufu kama wateule kwa maana *DED, DC, DAS* na Wakuu wa Idara wengine, lakini nataka niseme pia hii *capacity building* isiishie kwa hawa wateule peke yake, hata sisi Wabunge, lakini wale Madiwani, Wenyeviti wa Mitaa, Vijiji na Vitongoji ambao toka wameingia, sehemu kubwa mfano kwa Wenyeviti hakuna chochote walichojifunza. Matokeo yake unajikuta wako tu kule hawajui hata wanakwenda vipi pamoja na kwamba waliomba zile nafasi wakiamini wana uwezo na zile nafasi lakini kwa kweli wanahitaji kufanyiwa mafunzo ya kujenga uwezo. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nisisitize kwamba katika bajeti, hili ni jambo la msingi sana na kama tunakwenda na falsafa ya kwamba hakuna tena; kulikuwa na ile dhana ya Semina Elekezi. Naishauri tu Serikali yetu, naamini Serikali yetu ni sikivu, jambo hili tutakuwa tunakwenda kidogo kwa kimakosa. Tujaribu kulitazama upya, tutenge bajeti kwa ajili ya shughuli hiyo. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili ambalo nitapenda nichangie, kumejitokeza kule kwenye Halmashauri zetu ukinzani kati ya maelekezo kutoka Serikali Kuu na vipaumbele kutoka kwa wananchi. Sisi tunaokwenda kwa wananchi tunakutana na changamoto. Tunataka kuzitatua changamoto kutokana na vipaumbele ambavyo tumefikuta kwa wananchi, lakini mkikaa kwenye vikao vile pale Halmashauri wakati mwingine tayari kuna maelekezo, safari hii kipaumbele ni moja, mbili, tatu, huku kwingine hapana. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, najua hata hii Serikali tumeiweka kwa ajili ya kuhudumia wale wananchi. Tunapoweka *one size fits all*/kwamba katika ngazi ya Serikali, sawa. Kulikuwa na jambo ambalo limeonekana safari hii

tufanye operesheni hii twende namna hiyo, lakini vile vipaumbele ambavyo tunakwenda kuviluba kwa wananchi, tusiviache.

Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Waziri, hebu labda kuwe na maelekezo kwamba panapotokea mambo ya vipaumbele na maelekezo kabisa ya labda miongozo, maana yake hii miongozo ndiyo Watendaji wengi wanafanya nayo kazi hiyo, ili kusiwe na migongano sana katika hilo. Mwenyekiti, Mbunge na Madiwani wengine wanapambana na vipaumbele vilivyoibuliwa huko na wananchi; lakini Watendaji wa Halmashauri, wanapambana na melekezo. Mwisho wa siku hatutafika. Naomba sana Mheshimiwa Waziri hilo tuliangalie vizuri. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la tatu, napenda kuongelea kuhusiana na suala zima la huduma kwa wazee kwa maana ya kule hospitali. Niko sasa kwenye mpango wa afya kwa maana ya hospitali. Sera ipo vizuri na mipango ni mizuri. Nataka niwaambie, utekelezaji wake kule hospitali hebu tengenezeni mkakati au *mechanisms* za kuhakikisha unatekelezwa kadri mnavyopanga, kwa sababu utekelezaji kule haupo. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka niwaambie kama kwangu kule Hospitali ya Mji wa Kondo, ukiuliza habari ya Dirisha la Wazee, halipo. Ukiwaliza, sera hii ipo vipi? Wengine hawaelewi. Kwa hiyo, hebu tuhakikishe kuna mikakati mahususi ya kuona hii mipango tunayoiveka katika ngazi ya kitaifa inatekelezwa mpaka kule chini. Tuwe na *mechanisms* za kusimamia utekelezaji ambao utakuwa makini.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la vitambulisho; hao wazee wa kuanzia miaka 60 wapate vitambulisho ili waweze kuhudumiwa. Siyo tena kila wakati wakija wapite kwa Mtendaji wa Kata waandikiwe barua. Hiyo haijaka sawa! Ni usumbufu ambao unapunguza ufanisi. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nikiwa hapo hapo kwenye suala la afya, napenda niongelee suala la dawa. Malalamiko

juu ya dawa ni mengi kweli kweli. Hapa tunasikia kwamba hela zimepelekwa nyingi kwa ajili ya dawa, lakini kule unakuta hakuna dawa. Tatizo liko wapi hapa? Nataka nishauri Serikali tufanye utaratibu wa kuweka *procurement experts* kule kwenye Hospitali zetu ili waweze kujua *supply chain* ya dawa inakwenda vipi? Inapofika wakati mtu anasema matumizi yake ya dawa ni shilingi milioni 15 kwa wiki, huku analetewa hela tofauti, au ana-order kila baada ya *quarter* moja wakati dawa zinakatika katikati hapo ina maana hatuna mpango mzuri wa dawa. Tuweke taratibu ambao kutakuwa na *minimum reorder level*, ikifika kiasi fulani wana *orderten*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, bila kuwa na *experts wa procurement* kule kwenye hospitali zetu, tutaendelea kusumbuka na haya malalamiko yatakuwepo na hela zipo, zimepelekwa. Ukiangalia kwenye upande hela, zipo dawa hakuna. Naomba na hilo nalo liangaliwe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine kwenye upande huo huo wa afya, kuna baadhi ya hospitali zinakutana na changamoto kubwa sana kama ile hospitali ya Mji, Kondoa. Inahudumia Halmashauri tatu Kondoa Mji, Kondoa Wilaya, Chemba, lakini pia na sasa hivi barabara kubwa ya lami imepita na dharura zinaongezeka, lakini fungu kubwa la bajeti linakwenda kwa ajili ya Hospitali ya Mji; haitatosha. Hebu tuangalie kama pale tunawenza kuboresha kufikiria mpaka hao wengine watakapo jenga hospitali zao za wilaya, lakini kwa sasa hivi wote wanahudumiwa kuitia Hospitali ya Mji, Kondoa.

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho, niguse kidogo tu kwenye upande wa *TASAF*. Napongeza mpango huu, ni mzuri na malengo yake yana tija sana, lakini nataka niwaambie, utelezaji wake unahitaji mkakati wa kuusimamia ili ukidhi malengo. Kwa sasa hivi kuna upungufu mkubwa na kunatokea malalamiko mengi... (*Makofi*)

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa, muda wako umekwisha.
(*Kicheko*)

MHE. EDWIN M. SANNDA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. Naunga mkono hoja. (*Kicheko/Makofi*)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, nadhani mlimwona Mheshimiwa Waziri Mkuu alipokuwa amekaa, baada ya kukuta mtu anachangia ambaye angekatiza mbele yake. Tunakumbushana kila siku, Mheshimiwa Waziri Mkuu ameonesha mfano hapa. Kwa hiyo, tukumbuke tusikatize kati ya kiti ya Mheshimiwa Mbunge anapochangia. (*Makofi*)

Sasa namwita Mheshimiwa Ikupa Stella Alex, atafuatiwa na Mheshimiwa Susan Limbweni Kiwanga na Mheshimiwa Hamidu Hassan Bobali ajilande.

MHE. IKUPA S. ALEX: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii nami niweze kuchangia machache katika Wizara hizi mbili. Awali ya yote, naomba niiungane na wenzangu ambao wametangulia kumpongeza sana Mheshimiwa Rais, kwa yale makubwa ambayo ameendelea kuyafanya. Pia tumeona mambo mengi yamefanyika ndani ya kipindi hiki cha mwaka mmoja. Kwa kweli napenda nimpongeze sana. Kwa ajili ya muda sitawezza kuyataja, lakini naomba tu pongezi zangu zimfikie mahali popote alipo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri Simbachawene na Mheshimiwa Waziri Angella Kairuki kwa hizi taarifa zao. Nimezipitia kwa ufupi na uchache, mengi yamefanyika, pongezi zangu ziwafikie.

Mheshimiwa Naibu Spika, moja kwa moja naomba niongelee ile asilimia kumi ya vijana na wanawake. Naishukuru sana Serikali kwa kutenga hii asilimia kumi kwa ajili ya wanawake na vijana katika Halmashauri, lakini nina ushauri kidogo kuhusiana hii asilimia kumi na pia nimekuwa

nikiongea mara kwa mara, naomba niweke msisitizo tena juu ya hii asilimia kumi. Naiomba Serikali na pia Wabunge wenzangu tuungane katika hili, kwamba hii asilimia kumi igawanywe, angalau basi hata asilimia mbili au hata kama ni asilimia moja iwe ni kwa ajili ya watu wenye ulemavu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nini nasema hivyo? Kuna siku niliuliza swalii, nikaambiwa kwamba hii asilimia kumi unaposema kwamba wanawake na vijana, *in-accommodate* na watu wenye ulemavu, lakini kiuhalisia watu wenye ulemavu huwa hawapewi kipaumbele katika hii asilimia kumi. Ni malalamiko ambayo tumekutana nayo hata katika ziara mbalimbali; ukifuatia kwamba je, hii asilimia kumi mnanufanika nayo vipi? Wanasema hapana, tunapofika pale tunaambiwa kwamba ni kwa ajili ya vijana na wanawake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ikumbukwe kwamba kuna watu wenye ulemavu ambao siyo wanawake na wala siyo vijana; nafiki hapo naeleweka. Kwa hiyo, naiomba sana Serikali iliangalie hili; hii asilimia 10 igawanywe *either* iwe asilimia mbili kwa walemovu, halafu asilimia nne ibaki kwa wanawake na asilimia nne ibaki kwa vijana.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia naomba niongelee takwimu za watu wenye ulemavu. Kiukweli Tanzania hatuna takwimu halisi. Yaani tunasemea tu kwamba kwa sababu ndivyo ambavyo inajulikana kwamba katika *population* duniani asilimia kumi inakuwa ni ya watu wenye ulemavu kwa kila nchi, lakini tunatakiwa kuwa tupate uhalsia wa takwimu halisi za watu wenye ulemavu ili tuweze kupanga bajeti *accordingly*; kwa sababu sasa hivi tunabaki tu kama tuna hisia hisia, kwa hiyo hata ile bajeti yenyewe ambayo inatakiwa kwa ajili ya mambo fulani kwa ajili ya watu wenye ulemavu, inakuwa ni ngumu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaweza kufanyaje? Kupata takwimu yake, ni rahisi na ambayo inakuwa haina gharama ya aina yoyote. Kwa kuwatumia hao Wenyevitii wa

Serikali za Mitaa; nirudie tena kusema kwamba mimi mwenyewe binafsi nimeshawahi kufanya hivyo, yaani ile kuona kwamba hili jambo linawezekana? Nilimtumia Mwenyekiti wangu wa Serikali ya Mtaa nikamwambia naomba nifahamu, huu mtaa wako una watu wenye ulemavu wangapi? Ilikuwa ndani ya muda mfupi, yule Mwenyekiti akawasiliana na viongozi wake kwa maana ya Mabalozi, kila Balozi akaja na takwimu kwamba mimi katika nyumba zangu nina watu wenye ulemavu kadhaa. Kwa hiyo, mwisho wa siku yule Mwenyekiti akawa na takwimu sahihi kwamba watu wenye ulemavu nilionao kwenye Mtaa wangu ni watu kadhaa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho wa siku sasa hao Wenyeviti wanaweza wakawa wanakusanya zile takwimu wanapeleka kwa Wakuu wa Wilaya; Wakuu wa Wilaya wanazipandisha mpaka kwenye mikoa, hatimaye tunapata takwimu ya nchi nzima, kwamba watu wenye ulemavu wako wangapi, ambayo haitaigharimu Serikali gharama yoyote ile. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia naomba niongelee suala zima la miundombinu kwenye shule zetu kwa maana kwamba shule za msingi mpaka shule za sekondari. Hapa naongea kwa sababu tunaongelea suala zima la *inclusive education*, tukiongela suala la *inclusive education* miundombinu bado siyo rafiki.

Kwa hiyo, naendelea kuiomba Serikali iendelee kuboresha hii miundombinu. Hapa naomba niipongeze sana Serikali kwa sababu kuna baadhi ya maeneo nimetembelea kwenye hizi shule za msingi na kuna fedha zimepelekwa kwa ajili ya kurekebisha ile miundombinu. Sasa kupelekea tu ile fedha, haitoshi; nafikiri wakati zile fedha zinapelekwa, pia liwe linatolewa agizo kwamba hii miundombinu inakarabatiwa. Pia mnapokuwa mnafanya ukarabati, mzingatia mahitaji ya watoto wenye ulemavu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia katika kila shule itakuwa ni vizuri sana kukiwa kuna choo ambacho kinaweza

kumsaidia mtoto mwenye ulemavu kujisaidia kwa urahisi. Kwa sababu wakati nafanya hizi ziara, nilijaribu pia kuangalia miundombinu ya vyoo. Miundombinu ya vyoo siyo mizuri kabisa ukiangalia kuna ulemavu mwingine mtu anakuwa anatambaa chini, sasa ukimchanganya, kwamba aende kwenye vyoo vya *public* na watoto wenzake, inakuwa ni shida sana. Kwa hiyo, naiomba Serikali izingatie hilo pia kwamba hata kama ule ukarabati wa jumla utakuwa labda unachukua gharama kubwa, lakini pia suala la choo lingeanza, ingekuwa nzuri zaidi kwamba angalau kila shule ipate choo ambacho kitamsaidia mtoto mwenye ulemavu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kumalizia, naomba niongelee suala la *TASAF*. Naipongeza sana Serikali kwa jinsi ambavyo imefanya. Kweli katikati wakati niko kwenye ziara zangu, watu wenyе ulemavu walizungumzia sana suala la *TASAF* kwamba wao wamekuwa wakiachwa na badala yake wanakuwa wakiwekwa watu ambaо wana uwezo wao kabisa. Kwa hiyo, naipongeza Serikali, lakini pia naomba katika zile *qualifications* za kuingizwa kwenye huu mfumo wa *TASAF*, pia suala la ulemavu liangaliwe kwa maana kwamba ule ulemavu ambaо mtu anakuwa hajiwezi kabisa, anakuwa ni maskini. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna mmoja amekuwa akinisumbua sana hata sasa hivi, anasema kwamba yeye hana uwezo; nikajaribu kumwambia kwamba hebu basi awasiliane hata na Mwenyekiti Serikali za Mitaa, anaweza akamsaidia kwamba aanzie wapi au jinsi gani anaweza akaorodheshwa kwenye huu mpango; anasema hapana, hawa watu wanapeana, unakuta sisi ambaо tunakuwa tuna shida, tunaachwa, wanapeana watu ambaо hawana shida. Kwa hiyo, pia naomba Serikali iliangalie sana hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa nafasi, naomba kuunga mkono hoja. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Ikupa. Mheshimiwa Susan Limbweni Kiwanga, atafuatiwa na

Mheshimiwa Hamidu Hassan Bobali na Mheshimiwa Joshua Samwel Nassari ajiandae.

MHE. SUSAN L. KIWANGA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipatia hii nafasi nami nipate kuchangia kwenye hii Wizara yetu ya TAMISEMI. Ni Wizara ambayo ni pana, kubwa na inahangaika sana na makundi mengi ya kijamii yaliyoko kijiji, lakini ni Wizara ambayo haina uwezo, yaani kifedha imekuwa hoi, lakini inashughulika na watu moja kwa moja kwenye vijiji. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ninayeongea hapa natokea kwenye vijiji; tena vijiji hasa kule kusikokuwa na barabara, kusikokuwa na maji, wala huduma ya afya, wala kilimo bora wala na kilimo cha umwangilaji. Ndiyo huko ninakotoka. Kwa hiyo, hata kwenye hivi vitabu wakiandika, wanaenda kuboresha barabara vijiji kwa kuweka zege na nini, mimi nashangaa, wanaboresha wapi? Mijini au vijijini? Kwa hiyo, ni muhimu watakapokua hapa kuleta majibu ya kila eneo waeleze ni namna gani wataenda kuboresha haya maeneo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kibaya zaidi sasa, huko nilikotoka kwenye Halmashauri ya Wilaya ya Kilombero, mpaka tunakuja hapa kwenye hili Bunge, ni asilimia 25 tu ya pesa za maendeleo zimepelekwa huko. Sasa nashangaa, tunakuja kupitisha tena, hiyo asilimia 75 mtapeleka lini? Labda mtuambie, kabla hatujamaliza mwaka huu wa fedha mnapeleka lini hizo hela ili tupate maendeleo? (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wamejenga maboma, lakini Serikali haijamalizia. Mnasema mnaboresha *OND*, lakini wananchi wameshafanya; Serikali mna mpango gani wa kumalizia hayo maeneo ambayo wananchi wameshafanya kazi ya kutosha? Matokeo yake mvua zinakuja zinaharibu majengo, kwa hiyo, nguvu za wananchi zinapotea bure. Sasa ni vema kila bajeti mkija, hapo muwe na majibu ya uhakika mlifanya nini na kila Jimbo mtuambie mmefanya nini? Hiyo jumla jumla wakati wengine tunaumia huko, haiwezekani. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, migogoro ya mipaka katika vijiji ipo. Kwa mfano, Ofisi ya Waziri Mkuu inajua, TAMISEMI mnajua. Halmashauri ya Wilaya ya Kilombero; Kijiji cha Ngombo kiko Halmashauri ya Wilaya ya Kilombero, lakini mpaka leo Serikali haijaleta majibu Ngombo inaitika wapi? Matokeo yake mnatuachia ugomvi; Malinyi wanagombana na Kilombero. Naomba mniipe majibu, Ngombo iko wapi ili tupate maendeleo kwa wananchi wa Ngombo? (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu sasa vijiji, tangu mwaka 2014 tulivyoingia kwenye uchaguzi wa vijiji, kuna vijiji viwili havijafanya uchaguzi mpaka leo. Kijiji cha Idandu na Kijiji cha Miomboni. Majibu ya Serikali mnasema kwamba eti kule kuna uwekezaji; mimi nashangaa, hivi mahali kwenye uwekezaji ndiyo watu hawachagui uongozi wao?

Kwa hiyo, wale watu wanataabika, maendeleo yao hawajui wanafanya nini? Naomba majibu ya Serikali, ni lini mtaruhusu katika vile vijiji watu wafanye uchaguzi? Ni aibu, ni Serikali ambayo inasema ina utawala bora, lakini kule katika vile vijiji kwani wanakaa wanyama? Nataka majibu ya Serikali. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Mkoa kuisimamia Halmashauri, sasa nimpe taarifa Waziri wa TAMISEMI kama hajui. Katika Mkoa wa Morogoro, Wilaya ya Kilombero, wananchi wa Wilaya ya Kilombero tumenunua gari la Mkurugenzi, lakini gari hilo nakwambia mpaka sasa ni miezi sita liko kwa Mkuu wa Mkoa. Leo mnasema Mkoa usimamie Halmashauri, utasimamiae wakati wenyewe ndiyo unakwenda kubembeleza unachukua gari kwenye Halmashauri? Hawa watu wataweza wapi kuisimamia Halmashauri. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nini msiboreshe? Kama kweli ninyi ni waungwana, kwa nini mnaishia kununua ndege, hamboreshi Ofisi za Wakuu wa Mikoa ili waende wakasimamie hizo Halmashauri? Matokeo yake Mkuu wa Mkoa wa Morogoro hana gari, amechukua gari la Kilombero, moyo unaniuma na wananchi wa Kilombero tumenunua lile

gari kwa pesa zetu? Pelekeni gari la Mkuu wa Mkoa pale Morogoro ili gari letu lirudi Kilombero likafanye kazi. Miundombinu yetu ni mibovu, tunahitaji gari, acheni ubabaishaji. (*Kicheko/Makofi*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Susan, ulisema unatoa taarifa, hunipi nafasi nimwulize kama anapokea hiyo taarifa au unataka kumaliza?

MHE. SUSAN L. KIWANGA: Dakika zangu unitunzie. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ndiyo namwambia hivi, ajue nataka majibu ya Serikali apige simu kule atajua mwenyewe.

NAIBU SPIKA: Basi nadhani atakuwa amesikia. (*Kicheko*)

MHE. SUSAN L. KIWANGA: Mheshimiwa Naibu Spika, elimu ya awali. (*Kicheko*)

Usicheke hayo ndiyo mambo, mnatuumiza sana ninyi, haki ya Mungu! Yapo maneno mengi kwenye vitabu, lakini utekelezaji huko chini hamna. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, elimu ya awali na msingi; sawa mnasema elimu bure, lakini nendeni *field* mkaone. Haki ya Mungu, watoto 400 wa chekechea na darasa la kwanza wapo nje, Walimu hakuna. Hii nini? Kwa nini hamwajiri Walimu? Tatizo liko wapi? Leo nimeona kwenye vyombo vya habari eti Mheshimiwa Rais, wale Madaktari wa Kenya Wamekataliwa, ninyi ndiyo mnasema mnaajiri. Ninyi mna matatizo gani? Kwani ninyi hamna mpango wa kuajiri mpaka wakataliwe Kenya ndiyo mwajiri? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, leo mnasema mnapeleka Walimu wa Sayansi katika shule zetu, lakini mkae mkijua, Walimu wengi hata wa masomo ya kawaida, wamepungua

katika maeneo ya Vijijini, labda wamejaa Mjini. Tunataka ajira kwa Walimu, tunataka ajiwa kwa Madaktari, tunataka ajira kwa Manesi. Mtahakiki mpaka lini? Hii ni Serikali ya kuhakikil! Haiwezekani! Leteni ajira. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, uendeshaji wa Miji na Vijiji. Nilimwomba Mheshimiwa Jafo, hebu tembelea Jimbo la Mlimba. Kwa nini hamtembelei? Ninyi mkifika Ifakara, ndiyo mnaona mmefika Wilaya ya Kilombelo, lakini mjue kuna kilometra 265 kutoka ifakara mpaka kufikia Jimbo la Mlimba. Kwa nini hamji? Mnaogopa nini? Mnaogopa barabara kwa sababu mbaya! Njooni, tena vizuri mje wakati wa masika mwone kama hamkulala njiani siku tano na magari yenu hayo. Fikeni kule, nendeni mkahudumie wananchi. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Jimbo la Mlimba lina miji kama sikosei miwili au mitatu. Mlimba yenyewe, Ngeta na Chita, lakini mpaka leo hakuna mwendelezo, hakuna upimaji watu wako hovyo hovyo, hamtusaidi. Yaani Mlimba inastahili kuwa Halmashauri, Kilombelo na Ulanga na Malinyi inastahili kuwa na Mkoa, lakini leo mnatuchakaza. Sisi watoto wa wakulima hamtupi mkoa, hamtupi halmashauri, hamtupi miji, mna matatizo gani? Tunahitaji Halmashauri ya Mji wa Mlimba, tunahitaji Mkoa wa Morogoro ugawanywe mara mbili uwe Mkoa wa Kilombero. Tumeshatese sana, sasa tunasema basi. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, utawala bora uko wapi? Mkuu wa Mkoa kuteremka kwenye Kijiji, kuna mkutano mkubwa wa wananchi kutoka Kata mbalimbali, halafu anatangaza: "nimevunja Serikali ya Kijiji." Huo ndiyo utawala bora? Wapeni Semina Elekezi, wanaenda kutuvuruga vijijini. Hiyo imetokea kwenye Kijiji cha Ikule; Kata ya Mngeta Mkuu wa Mkoa alienda akiwepo na Mheshimiwa Waziri Mwinyi huyu hapa. Hivi alivyofanya vile Mkuu wa Mkoa pale ni sahihi; kwenda kuvunja Serikali ya Kijiji kwenye Mkutano wa wananchi Kata yote? Ni aibu! Waambie, wapeni elimu; wanatutesa wananchi. Wapeni Semina Elekezi, kuna umuhimu. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema hivi, kwenye hiyo hotuba ya Kambi ya Upinzani naiunga mkono. Huyu Mheshimiwa Mama Mollel wallyempiga hapa, alistaafu kazi miaka mitatu iliyopita, mtu asiyekuwa na takwimu, yaani usipofanya utafiti huna *right* ya kusema wewe. Leo anampiga Mheshimiwa Mama Mollel, eti amestaafu siku tano; achana na hizo habari wewe! Mengine kuna watu wamekuwekea kiporo, watakuja kumalizana na wewe. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hali ya vijjini kwetu ni mbaya; mnapoenda kuzuru maeneo na Waziri Mkuu anajuba, kwenye kile kijiji mnasema kuna uwekezaji wa sukari, lakini mpaka leo wananchi wanahangaika. Vijiji havijafanya uchaguzi. Nendeni sasa mkalete hao wawekezaji, wananchi wapo tayari kuwa wakulima wa nje illi wapate maendeleo yao.

Mheshimiwa Simbachawenye naongea na wewe kila siku; tunahitaji, ingawa unasema sasa hivi huyu jamaa hataki utawala mpya. Sisi tumeshaumia sana watu wa huku; hivi wewe Jimbo moja lina kilometa karibu 300, leo linakwenda ku-report Makao Makuu ya Wilaya kilometa 265, hamwoni kama mnawatesa wananchi wale?

Mheshimiwa Naibu Spika, tunahitaji utawala, tunahitaji Halmashauri ya Mji wa Wilaya ya Mlimba; tunahitaji Mji midogo ikaendelezwe; na hizo bajeti mnazosema, tunahitaji tuzipate; Vituo vya Afya ndiyo usiseme, balaa. Juzi juzi hapa tumepata shilingi milioni 500 kuendeleza Kituo cha Afya cha Mlimba lakini hakitoshi, kwa sababu Jimbo lina kilometa zisizopungua... (*Makofi*)

(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Susan, umetoa amri nydingi hapo, hata sijui ni ipi inayotakiwa kutekelezwa. (*Kicheko/Makofi*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Hamidu Hassan Bobali, atafuatiwa na Mheshimiwa Joshua Samwel Nassari na Mheshimiwa Mbaraka Dau ajilandae.

MHE. HAMIDU H. BOBALI: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia afya niweze kusimama leo kuchangia kwenye Bajeti ya Ofisi ya Rais.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwa na mkanganyiko kwamba watu wana sema tusimtaje Mheshimiwa Rais. Mheshimiwa Naibu Spika, Ofisi ya TAMISEMI iko chini ya Rais, Ofisi ya Utawala Bora iko chini ya Rais. Wizara tunazozijadili leo zinafanya kazi chini ya Rais. Kwa hiyo, kutomtaja Rais maana yake hatujadili kabisa hizi Wizara. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kutuzuia tuiseme, tuishie kwenye kusifia, mimi Mbunge wa Jimbo la Mchinga wananchi hawakunituma nije kusifia hapa. Wananchi wamenituma nije kueleza kero zinazowakabili. Katiba yetu ya nchi imetoa mamlaka ya kazi za Bunge, sasa nashangaa kama kuna mtu anakuja anasema nyie mnaponda tu. Tusifie! Aah, sisi tuliochaguliwa bwana hatusifii, tunakuja kueleza kero za wananchi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze suala la utawala wa sheria. Nchi yetu inafuata utaratibu; tuna Serikali Kuu na Serikali za Mitaa. Mheshimiwa Waziri Simbachawene, kuna Mamlaka za Serikali za Mitaa Halmashauri ya Wilaya, Vijiji; hizi Serikali nasi tuliamua kutumia mfumo wa *D by D*, lakini leo vyanzo vya mapato kwenye Halmashauri zetu tumevihamisha tumepeleka Serikali Kuu. *Property Tax* ambayo kwenye taarifa yako mwenyewe umeeleza kwamba haijakusanywa.

Mheshimiwa Naibu Spika, makadirio ilikuwa zikusanywe shilingi bilioni 29, zimekusanywa shilingi bilioni nne; nami naamini itakuwa sjui Kinondoni tu. Haijakusanywa kwa sababu hizi shughuli zinahitaji zifanywe na Halmashauri

wenyewe. Tunapoteza mapato mengi, mmejilimbikizia kila kitu mmepeleka *TRA*, mwisho wa siku Halmashauri zetu zitashindwa kufanya kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri kwa kuwa tumeamua kufuata mfumo huu wa *D by D*, hizi Serikali ni Serikali zilizopo kwa mujibu wa Katiba, tuzipe mamlaka zikusanye mapato zenyewe, hii *Property Tax* ni muhimu sana. Jana nilikuwa nafuatilia, nilikuwa najaribu kuangalia kusoma mifumo ya nchi mbalimbali. Nimeangalia India, Thailand na nchi nyingine ambazo tunafanana nazo. Hakuna nchi ambayo imechukua *Property tax* kwenye Halmashauri inapeleka kwenye *Central Government*, ni sisi tu na sijui kwa malengo gani? (*Makof!*)

Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri, naomba sana hili mliangalle. Isiwe kila mpango unaoletwa na Waziri wa Fedha iwe unau-copy na kuu-paste na kuuchukua, mwisho wa siku wewe ndio utalaumiwa. Halmashauri zikifa, wewe ndio utabeba huu msala. Mheshimiwa Mpango ataendelea na kazi yake ya kukusanya mapato *TRA*. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo nataka niliunganishie hapo hapo, kumekuwa na tabia isiyoridhisha ya Wakuu wa Wilaya kuziondoa Madarakani Serikali za Vijiiji. Imefikia hatua leo Serikali za Vijiiji wale Wenyeviti wakisikia Mkuu wa Wilaya anakuja, hawaendi kwenye Mkutano, kwa sababu wanajua wakienda, wanatumbuliwa. Sasa tunataka tujue ni sheria ipi inampa Mamlaka Mkuu wa Wilaya kuondoa Serikali halali ya Kijiji iliyochaguliwa na wananchi? (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tunayo mifano mizuri mingine hapa Dodoma. Mkuu wa Wilaya Dodoma katangaza tu, Mwenyekiti hapa ondoka! Kwa hiyo, tunahitaji ufanuzi; haya ni maagizo ya Mheshimiwa Rais? Kwa sababu hizi Wizara ziko chini ya Rais. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nzungumzie suala la kuajiri Watumishi wa Idara ya Afya. Kwenye Jimbo langu zipo

zahanati nne, zimejengwa, zimekamilika. Hazijafunguliwa kwa sababu hazina wahudumu wa afya. Kwa bahati nzuri, Mheshimiwa Rais alikuja mwezi wa Tatu Lindi, alisimama Mchinga, akaelezwa na wananchi kwamba kero yetu kubwa hapa ni wahudumu wa afya. Mheshimiwa Rais akamwachia lile suala Mganga Mkuu wa Mkoa, akamwambia shughulikia hilo. Mganga Mkuu wa Mkoa anawatoa wapi? Kila tukiangalia kwenye Halmashauri yetu, hakuna mtu ambaye anaweza kutoka kituo kimoja kwenda kwenye kituo kingine, kwa sababu hata hivyo vituo vyenyewe vina uhaba mkubwa wa watumishi hao. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba sana Mheshimiwa Waziri, hili alichukulie kwa uzito wake. Tunahitaji Watumishi wa Idara wa Afya waende wakahudumie wananchi. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ni suala la *TASAF*. Nashukuru Mheshimiwa Waziri ameeleza kwamba upo mpango wa wa kuongeza vijiji vingine. Jambo hili litatusaidia sana. *TASAF* sasa hivi imekuwa hata kwetu wanasiasa siasa yetu imekuwa ngumu. Kwa mfano, mimi Jimbo langu lina Tarafa nne. Katika Jimbo lenye Tarafa nne, Tarafa mbili zinanufaika, Tarafa mbili hazinufaiki, inatuwia shida na wananchi hawajui; wanachofikiri wao ni kwamba wewe ndio Mbunge, unaamua kwamba hapa wapate hapa wasipate. (*Makof*)

Kwa hiyo, naomba sana mtusaidie, vile vijiji ambavyo havijapata hii miradi ya *TASAF* pelekeni na kama inashindikana, basi bora tuondoke wote tukose wote, kwa sababu haileti maana kwamba wengine wanapata; wana sifa zile zile na wengine wanakosa. Nashauri sana Mheshimiwa Waziri hili alichukulie *very seriously* kwa sababu ni suala la kisiasi na linatuharibia siasa huko na sisi wote ni wanasiasa hapa. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo ni muhimu nataka nilizungumzie ni suala la utendaji mbovu usioridhisha wa Wakurugenzi. Watu wamesema hapa, lakini

inaonekana kama masihara. Jamani sisi wenzenu, nafikiri hata mwenzangu Mheshimiwa Nape wa Halmashauri moja naye anawezakuja kusema hapa. Wenzenu tuna shida. Tulikuwa tunavumilia lakini sasa tunasema, wenzenu tuna shida. Yaani unamtoa mtu, sijui alikuwepo Afisa nani sijui kwenye Kata huko unakuja kumfanya Mkurugenzi katika Halmashauri kubwa kama ilivyo Halmashauri yetu. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Halmashauri yetu ni kubwa kuliko Halmashauri zote za Mkoa wa Lindi, zina eneo kubwa! Unatuletea mtu ambaye ukisoma hivi vitabu, katika Mkoa mzima wa *Lindi, internal collection* iliyo chini kuliko zote ni Halmashauri yetu ya Wilaya ya Lindi. Ndiyo Halmashauri yenye *population* kubwa na Halmashauri ambayo ni kubwa. Tatizo ni utendaji usioridhisha wa hao watu mliowateua mkatuletea. Kwa hiyo, tunaomba sana, kama kuna haja ya kubadilisha, tubadilishieni, lakini kama hamna haja ya kufanya hivyo, tunaomba basi muwape mafunzo, kwa sababu wanatuletea umaskini; badala ya kwenda mbele sasa, tunarudi nyuma. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la mwisho, nilimwandikia jana Mheshimiwa Simbachawene, nami namwamini kwamba hilo, nililomwandikia atalifanyia kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala la Walimu, nilipoona taarifa kwamba kumeajiriwa Walimu nilipata faraja sana hususan Walimu wa sayansi. Katika Jimbo langu kuna shule za sekondari saba, nimepata Walimu katika shule za sekondari mbili; Shule ya Mvuleni na Shule ya Rutamu; shule ambazo zina matatizo makubwa zimekosa Walimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, siyo tu shule yangu au Halmashauri yetu, Mkoa wa Lindi mnajua matokeo ya mtihani uliopita yalikuwa mabaya; tumekuwa kwenye tatu bora na hatupendi kuwa hivyo. Katika jambo ambalo linatuma ni sisi kuwa wa mwisho na ni Mkoa uliota Waziri Mkuu; lakini moja ya sababu ambayo imepelekea Mkoa wetu kuwa katika kiwango cha mwisho cha ufaulu ni kwa sababu ya idadi ndogo ya Walimu.

Waheshimiwa Mawaziri wanajua historia ya Lindi, hili halifichiki. Zamani watu walikuwa wanagoma kuja kule. Siku hizi wanakuja kwa sababu kuna mambo mazuri; kuna miradi ya gesi, korosho ziko juu, kila kitu kipo. Kwa hiyo, waleteni, hawagomi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nilipoona kwamba mmetangaza ajira, nikajua mtatufanyia *affirmative action* kwa sababu mkoaa wetu uko chini, tunahitaji mtusaidie. Kama mtaajiri tena, naomba sana, shule zilizopo katika eneo langu la Jimbo la Mchinga zina uhaba mkubwa wa Walimu. Shule ya Sekondari Mchinga ambayo ni kubwa, inafaulisha kidogo wastani, lakini ina uhaba wa Walimu wa Sayansi; Shule ya Sekondari ya Mvuleni nimepelekewa mmoja, mahitaji ilikuwa ni Walimu watano; Milola na shule nyingine zote zina uhaba mkubwa wa Walimu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Bobali. Mheshimiwa Joshua Samwel Nassari atafuatiwa na Mheshimiwa Mbaraka Dau na Mheshimiwa Mendrad Kigola ajiandae.

MHE. JOSHUA S. NASSARI: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana. Kipekee, kwanza kabisa kabla ya kuzungumza, nawashukuru sana wananchi wangu wa Jimbo la Arumeru ambaao wamenivumila kwa kipindi chote ambacho nilikuwa masomoni nchini Uingereza mpaka sasa ambapo nimerejea kuja kuendelea na kazi hii. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, dunia inazunguka kwa kasi sana. Kwa nini nasema hivyo? Leo kwenye Bunge hili, Mawaziri wanatuambia tusizungumze habari ya kugusa wala kujadili habari ya Usalama wa Taifa letu. Kwenye mkono huu, ninayo barua hapa yenye kurasa saba iliyoandikwa na aliyekuwa Naibu Waziri wa Ujenzi, leo hii ni Waziri wa Habari, Mheshimiwa Dkt. Harrison George Mwakyembe. Barua hii imeandikwa tarehe 9 Februari, 2011. Kwenye barua hii Mheshimiwa Dkt. Mwakyembe alikuwa anatuhumu baadhi

ya watu wakiwemo watu wa Utumishi wa Usalama wa Taifa kutaka kuchukua maisha yake; kutaka kumteka ama vitendo ambavyo vimekuwa vikiendelea kwenye Taifa hili. Usipoguswa, huyasikii maumivu; ukiguswa unayasikia maumivu. Barua hiyo aliyoandika Mheshimiwa Dkt. Mwakyembe, Mwalimu wangu wa Sheria huyu... (*Kicheko*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Nassari, ili Bunge liweze kwenda sawasawa, hiyo barua alikuandikia wewe? Nani aliyeandikiwa? Ili wote tuje cha kufanya humu ndani. Wewe tuongoze, barua aliandikiwa nani?

MHE. JOSHUA S. NASSARI: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Baada ya maongezi yangu ya dakika moja ijayo, nitai-table hii barua Mezani kwako, kwa hiyo, utafahamu *details* zote, lakini...

NAIBU SPIKA: Sasa ukiniambia hivyo, nitakwambia hivi, jambo hilo nimekataza tayari. Ndiyo maana nakuuliza ili njue twende wote pamoja. Kwa hiyo, wewe nieleze, maana unayo hapo mkononi.

MHE. JOSHUA S. NASSARI: Mheshimiwa Naibu Spika, *my sister in Christ, let me finish.* Nina barua nimekwambia ninayo mkononi, nitaileta Mezani kwako *in a minute.*

NAIBU SPIKA: Naomba ukae Mheshimiwa Nassari.

Waheshimiwa Wabunge, leo kabla hatujaahirisha shughuli za Bunge, mwongozo umeombwa na Mheshimiwa Deo Sanga; nimetao hapa maelekezo wote tulikuwepo kuhusu jambo hilo. Sasa Mheshimiwa Nassari nikushauri, Kanuni ya tano inakupa wewe uwezo wa kuuliza kuhusu maamuzi ya kiti, kwa sababu jambo hili nililiamua leo hapa ndani. Wewe huwezi kulizungumzia kwa kuwa mimi ndio nililamua leo hapa.

Kwa hiyo, kama unataka kuleta hoja yakutokukubaliana ya kile nilichokiamua, tumia uwezo wako ambao umepewa kikanuni na Kanuni ya (5) ili uweze

kuzungumzia jambo hilo. Kwa hiyo, Mheshimiwa Nassari naomba uendelee na mchango, lakini usichangie kuhusu jambo ambalo nimelikataza leo.

MHE. JOSHUA S. NASSARI: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba unilindie muda wangu, kwa sababu umechukua dakika zangu takribani mbili; lakini kwa sababu naheshimu sana kiti, barua hii imeandikwa tarehe 9 Februari, 2011 na ikaandikwa kwa *IGP* Saidi Mwema.

NAIBU SPIKA: Hilo tumeshalimaliza Mheshimiwa Nassari. Nimekuuliza mara mbili umekataa kusoma. Kwa hiyo, naomba uliache utumie Kanuni ya (5) kama nilivyokushauri ili uweze kuuliza maamuzi ya kiti; peleka suala lako kwa Spika ili Kamati ya Kanuni iweze kuamua juu ya maamuzi nillyoyafanya.

MHE. JOSHUA S. NASSARI: Mheshimiwa Naibu Spika, nitaitleta kwako kama ulivyonagiza...

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu utaratibu.

NAIBU SPIKA: Naomba ukae Mheshimiwa Msigwa. Mheshimiwa Nassari.

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Kuhusu utaratibu.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Msigwa naomba ukae.

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Mimi ndio *Chief Whip* wa huku Mheshimiwa! Si na kule unamsimamisha! (*Kicheko*)

NAIBU SPIKA: Naomba ukae Mheshimiwa Msigwa.

NAIBU SPIKA: Naomba ukae Mheshimiwa Msigwa ili nikueleze kanuni ya kuhusu utaratibu inasemaje. Yaani tuwe tunaelewana vizuri Waheshimiwa Wabunge, Kanuni ya kuhusu utaratibu unampa Mbunge mwenzio anayezungumza si Spika wala si Kiti cha Spika, si utaratibu. Kwa hiyo, ninapokwambia ukae ni kwa sababu kanuni hizi tumetunga wenyewe. (*Makof*)

Mheshimiwa Nassari naomba uendelee na mchango.

MHE. JOSHUA S. NASSARI: Mheshimiwa Naibu Spika, nina *stop watch* kwangu nimeweka kabisa nimeongea kwa sekunde 38, naomba utunze muda wangu kwasababu umetumia dakika zangu mbili, habari ya Dkt. Mwakyembe...

NAIBU SPIKA: Makatibu wanansaidia kutunza muda, kwa hiyo usitie shaka.

MHE. JOSHUA S. NASSARI: ...nitaiacha sitaizingumza tena, lakini naomba Makatibu waliopo mezani waje kuchukua hii nyaraka wakuletee wewe na wewe uipitie wakati naizungumza ili ujue nazungumza kitu gani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu umesema tusizungumzie habari ya Usalama wa Taifa nitaiacha ila nitaendelea kujadili hotuba hii nikizingatia utaratibu uliofanywa na watu ambao ni wakubwa kwenye Serikali yetu akiwepo mwalimu wangu Mheshimiwa Dkt. Harison Mwakyembe. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, habari ya usalama naiweka pemberi, lakini kuonesha namna gani dunia inakwenda kwa kasi, ni Mheshimiwa Dkt. Harisson Mwakyembe huyu huyu Waziri wa leo; mwaka 2008 aliongoza Kamati Teule ya Bunge hili Tukufu ambayo ilijadili suala la *Richmond*. Katika suala lile hakusikiliza upande wa pili kwa maana ya aliyekuwa Waziri Mkuu Mheshimiwa Edward Lowassa, akasikiliza upande mmoja akatoa ripoti kwenye Bunge hili ambayo ilipelekea Mheshimiwa Lowassa kuachia ngazi. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mwakyembe huyu leo amepokea ripoti ya aliyejikuwa Waziri kwenye Wizara yake Mheshimiwa Nape yupo hapa; upande wa pili kwa maana ya Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam aliyejataa kuhojiwa, akakimbia kwa mlango wa mbele wakati amewatumwa watu kwa mlango wa nyuma. Leo Mwakyembe anasema ripoti hii hajja-*balance* storu kwa hiyo siwezi kuifanya kazi. Mwakyembe hiyo *balancing of the story* ya Mheshimiwa Lowassa na kuachia ngazi uliitoa wapi? Hukumsikiliza Lowassa alikuwa Waziri Mkuu hapa... (*Makofii*)

WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO: Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

MHE. JOSHUA S. NASSARI: Taarifa unanilettea ya nini, wote tulikuwa tunaangalia Bunge?

T A A R I F A

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Nassari, sikiliza taarifa; Mheshimiwa Mwakyembe.

WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO: Mheshimiwa Naibu Spika, nimesimama kuomba taarifa chini ya kanuni ya 68 ili nimsaidie Mheshimiwa Nassari asipotoshe umma kuhusu masuala ya kisheria na mimi ninayeongea hapa kama ananiita mwalimu ni mwalimu wake anisikilize vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la *Richmond* lilipokuwa linachunguzwa liliifanywa na *Select Committee* ya Bunge ambalo kazi yake ilikuwa ni ku-*investigate. Investigation* hailazimishi umwite mtu kumsikiliza.

(Hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge walizomea)

WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO: Mimi nashindwa kuelewa kama polisi hajakuhoji unaenda kulalamika kwamba sijahojiwa na polisi? Ni kukosa uelewa tu, mambo ya weledi haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, unapokuwa na Kamati Teule inapochunguza ikimpata mtu wa...

MHE. HALIMA J. MDEE: Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Halima muache amalize kutoa taarifa halafu...

(Hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge waliongea bila mpangilio kuashiria kutokubaliana na Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge tufuate utaratibu wa kikanuni kwa sababu huyu anampa taarifa Mheshimiwa Nassari. Kwa hiyo, lazima Nassari aulizwe kwanza, Mheshimiwa Halima naomba ukae...

MHE. HALIMA J. MDEE: Mheshimiwa Naibu Spika, nampa taarifa hapa kwamba...

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Halima, naomba ukae tafadhalii; Mheshimiwa Mwakyembe endelea.

WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANA NA MICHEZO: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana; mimi nashindwa kuelewa wanasheria tulionao hapa. Halima unasi mama wala huelewi nasema nini, subiri nimalize kuongea.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninachosema ni kwamba, unapokuwa kwenye Kamati Teule kazi yako kubwa ni kuchunguza wale watu ambao unaona hakuna ushahidi unawahoji, lakini wale watu ambao una ushahidi kamilifu huitaji kuwahoji; unawaleta Bungeni na Bunge ndilo linakuja kuwahoji. (*Makofi*)

(Hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge waliendelea kuongea bila mpangilio kuashiria kutokubaliana na Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo)

WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO: Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naomba nimweleze tu Nassari suala la *Richmond* kama kuna watu hawajariidhika, kwa sababu wamejawa na mahaba walileté tena Bungeni tuone kama huyo mwenzao wenye mahaba hatutamnyoa hapa kwa vipande vya chupa. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Mwakyembe, malizia taarifa yako.

WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO: Mheshimiwa Naibu Spika, nimalizie kumpa taarifa Nassari...

(Hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge waliendelea kuongea bila mpangilio kuashiria kutokubaliana na Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo)

NAIBU SPIKA: Ongea na Kiti Mheshimiwa Mwakyembe.

WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana. Tatizo hapa ni kwamba... Bunge letu watu ndiyo tunalilia /ive wakati tunafanya mambo ya kitoto hapa; nisikilize najenga hoja.

(Hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge waliendelea kuongea bila mpangilio kuashiria kutokubaliana na Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo)

WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO: Mheshimiwa Naibu Spika, ninachosema tu ni kwamba tulichokifanya kwenye Kamati Teule ya Bunge kilikuwa sahihi, sisi hatukuhitaji kumhoji mtu ambaye tulimkuta na evidence ambayo ni *incriminating*. Hata leo wakitaka... (*Makofi*)

MHE. HALIMA J. MDEE: Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Mwakyembe nadhani ameshaipata hiyo taarifa.

WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANA'A NA MICHEZO: Na hata leo wakitaka kanuni za Bunge zinaturuhusu tuweze kulipitia tena suala la *Richmond* na nawahakikishia...

MHE. HALIMA J. MDEE: Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Mwakyembe naomba ukae. Mheshimiwa Nassari... Mheshimiwa Silinde naomba ukae, Mheshimiwa Halima!

Mheshimiwa Nassari, Mheshimiwa Mwakyembe ametoa taarifa unaipokea hiyo taarifa ama unaikataa?

MHE. HALIMA J. MDEE: Sasa wewe si ukae nae, mshamba.

MHE. JOSHUA S. NASSARI: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru, naomba ulinde muda wangu. Namheshimu sana mwalimu wangu Dkt. Mwakyembe lakini naomba nimkumbushe pia kwamba taarifa yake siipokei kwa sababu zifuatazo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ya kwanza; ni Profesa ama Dkt. wa kwanza wa *PhD* kwenye nchi hii ambae aliandika *thesis* yake ya *PhD* iliyoonesha ili taifa hili liende mbele lazima kuwe na Serikali tatu na tena wakati wa Bunge la Katiba alikataa *thesis* yake mwenye hapa ndani ya Bunge hili; mimi nilikuwa Mbunge hapa, huyo hapo. (*Makofii/Vigelegele*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa...

WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANA'A NA MICHEZO: Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge... Mheshimiwa Jenista Mhagama.

MBUNGE FULANI: Unapendelea!

(Hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge waliongea bila mpangilio kuashiria kutokubaliana na Naibu Spika)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tusikilizane. Mheshimiwa Nassari naomba uzime *mic* Mheshimiwa *Chief Whip*.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WATU WENYE ULEMAVU): Mheshimiwa Naibu Spika...

NAIBU SPIKA: Huwezi kusimama na mwiningine kasimama, subiri uwe *recognized*; akimaliza! Sasa mtaongea wote wawili Msigwa? Ndio kaa sasa, kaa chini amalize mwenzako upewe nafasi, Mheshimiwa *Chief Whip*.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WATU WENYE ULEMAVU): Mheshimiwa Naibu Spika, kanuni zetu, kanuni ya 68(1) inazungumzia utaratibu ndani ya shughuli zinazoendelea Bungeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, mjadala huu unaokwenda hapa Bungeni sasa huko tunapokwenda unakwenda kuvunja kanuni zifuatazo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kanuni ya kwanza; tunakwenda kuvunja kanuni ambayo inawakataza Waheshimiwa Wabunge kuchelewesa shughuli za Bunge kwa hoja ambazo haziko katika ratiba ya Bunge. Kwa hiyo, hiyo ni kanuni ya kwanza inavunjwa na ni lazima tuone kwamba kanuni hii inalindwa na wachangiaji wajikite katika hoja ambayo iko kwenye meza yako na si hoja nyingine. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini...

MHE. HALIMA J. MDEE: Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Halima, naomba ukae.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WATU WENYE ULEMAVU): Mheshimiwa Naibu Spika, kanuni nyingine ambayo inavunjwa; tunapozungumzia suala la utawala bora tunazungumzia utawala bora si kwa kumu-*attack* mtu *in person*. Kwa hiyo, tunachokifanya hapa ni kama vile tunahamisha hoja hii na kumzungumza Mheshimiwa Dkt. Mwakyembe; Waziri wa Habari...

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WATU WENYE ULEMAVU): Kama Dkt. Mwakyembe na sio hoja ambayo ipo ya utawala bora kwa ujumla wake...

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WATU WENYE ULEMAVU): Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba kiti chako kituongoze tufanye mjadala huu na kama mtu ana hoja inayohusu Wizara ya Habari asubiri...

MHE. HALIMA J. MDEE: Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu utaratibu.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WATU WENYE ULEMAVU): ...asubiri asiwhahishe shughuli kanuni pia inakataza kuwashisha shughuli...

MHE. HALIMA J. MDEE: Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu utaratibu.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WATU WENYE ULEMAVU): ...asubiri hotuba ya Wizara inayohusika itakapofika ajenge hizo hoja kwa kuzingatia utaratibu uliowekwa. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Msigwa

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Mheshimiwa Naibu Spika, kanuni ya 64(1) inasema bila ya kuathiri masharti ya ibara ya 100 ya Katiba yanayolinda na kuhifadhi uhuru wa mawazo na majadiliano katika Bunge. Ibara yetu ya 100 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inatutaka na inalitaka Bunge liwe na uhuru wa mawazo (*freedom of speech*)ndani ya Bunge. Kitendo anachokifanya Mheshimiwa Nassari ana-*cite*; Bunge hili tumekuwa tuki-*cite* kwa kusoma magazeti, kwa kusoma barua na kwa kutoa nukuu kwa kuwa kanuni zinaturuhusu; hicho ndicho kitendo anachokifanya Mheshimiwa Nassari. Zaidi ya yote anayemzungumzia yumo humu ndani ya Bunge, ana uwezo wa kujitetea, hayupo nje ya Bunge. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Nassari ana-*cite*; anatoa *reference*, anajenga hoja yake katika kuzungumzia suala la utawala bora na jinsi watu ambavyo wapo *double standard*. Sasa kila anachozungumza watu wanajaa presha ya nini?

Mheshimiwa Naibu Spika, nikuombe, tunazungumzia utawala bora, tumuache Mheshimiwa azungumze hoja yake, atoe uhuru wake wa mawazo. Tunachokifanya sasa hivi tunakanyaga Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; tupo hapa kutoa uhuru wa mawazo na wananchi wametupa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ningeomba *Chief Whip* aache kulipotosha Bunge na nakuomba usimame katika haki; watu tutoe uhuru wetu wa mawazo. Hapa ni mahali pa ku-

dialogue, hapa kama huwezi kuongea ukakae sehemu nyingine; this is the place to speak, tunaongea kwa niaba ya wananchi. (Makof)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali naomba ukae.

Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Nassari alikuwa anachangia mambo mawili kwa haraka. Mheshimiwa Mwakyembe aliomba kutoa taarifa kulingana na yale yaliyokuwa yanachangiwa na Mheshimiwa Nassari. Kanuni zetu zinamruhusu anayepewa taarifa kuikubali ama kuikataa taarifa hiyo na Mheshimiwa Nassari ameikataa taarifa akatoa sababu zake na ameendelea sasa kuchangia. Katika kuendelea kuchangia kwake amerudi tena kwa Mheshimiwa Mwakyembe na uandishi wake...

(Hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge waliongea bila mpangilio)

NAIBU SPIKA: Tusikilizane Waheshimiwa. Amerudi kuchangia tena kuhusu andiko la *degree* ya uzamivu ya Mheshimiwa Mwakyembe, kwamba maoni yake yalikuwa ni kwamba Serikali tatu na sasa akasema mbili kwenye Bunge la Katiba. Sasa Mheshimiwa Mwakyembe akawa anasimama anataka tena kuomba taarifa, Wabunge wengi wakasimama.

Waheshimiwa Wabunge, ili tuweze kusonga mbele tuzifuate kanuni tulizojiwekea sisi wenyewe. Hawezi mtu mmoja akawa anatoa taarifa, mwininge anasimama anataka kutoa taarifa; tutakuwa hatuendi sawasawa. Kwa sababu la sivyo maana yake hii nyumba hakuna mtu atakaa azungumze amalize kwa kuwa kila mtu anakatizwa kila wakati.

Sasa nimesimama hapa ili kuweka utulivu huu; tafadhali naomba tufuate utaratibu wa kikanuni. Mbunge anayechangia ndiye anayepewa taarifa. Sasa ikiwa kila mtu

anataka kupeana taarifa, hizi kanuni tutakuwa tunazikosea lakini pia nani atayekuwa anaulizwa na yupi? Kwa sababu kanuni zetu zinazungumzia Mbunge anayechangia.

Naomba sana Waheshimiwa Wabunge tutunze muda wetu vizuri ili tuweze kumaliza jambo lililo mbele yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Nassari.

MHE. JOSHUA S. NASSARI: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru lakini naomba tu niweke upepo sawa; sina shida na mwalimu wangu Dkt. Harrison Mwakyembe napenda sana amenitoa kwenye ujinga; lakini ukweli ni kwamba nilikuwa naikataa taarifa ya Dkt. Harrison Mkwakyembe kwa kutumia *reference and the kind of reference I used was his own thesis*. Sasa kama mimi natumia *reference* ya andiko ambalo ameliandika ye ye mwenyewe kwa miaka; ninyi mnataka mtu atumie *reference* gani jamani, mnataka nitumie Mwanahalisi ya Kubenea, Mwananchi au Tanzania Daima? Natumia *reference* ya alichokiandika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mnapeleka wapi Bunge ninyi watu? Muda wangu tafadhalii.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nimepata nafasi ya kusoma ya kwenye nchi za Magharibi, nchi za Amerika, Ulaya na nchi za Asia, zilizoendelea. Katika kipindi cha miezi tisa iliyopita nimekaa nje ya siasa za Kitanzania, siasa za Kibunge kwa hiyo nimezitazama nikiwa niko nje ya siasa za nchi hii. Nimeona siasa zinatia kichefu chefu; ukiongea ukweli kama huu unakandamizwa. Leo wewe asubuhi ameongea Mzee Bulembo hapa, kwenye mchango wake hapa amemsema Mbunge wa Siha Dkt. Mollel wa CHADEMA mbona hamjamzuia? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nimepewa taarifa nakataa taarifa *with a reference* wewe ni mwalimu wa sheria unajua huyu ni mwalimu mwenzako wa sheria kwa nini unaikataa taarifa yangu kukataa taarifa yake?

NAIBU SPIKA: Nassari, mimi sijakukataza; nimekuuliza kikanuni unaikubali au unaikataa? Sasa ukianza tena kuonesha kana kwamba hatukufuata utaratibu unamaanisha nini? Tuendelee jamani, Mheshimiwa Nassari naomba uchangie usianze tena kuki-*accuse* kit; Mheshimiwa Spika aliwaeleza jana na mfuate huo utaratibu tafadhalii.

MHE. JOSHUA S. NASSARI: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nikuthibitishie kwamba nilipoziangalia siasa za nchi yetu kutoka nje niliona ujinga ufuataao:-

Mheshimiwa Naibu Spika, la kwanza; ni mara ya kwanza kwenye historia ya siasa za dunia unamuona mtu mwenye cheo kama cha Ukuu wa Mkoa anavamia kwenye *media house* tena si *media house* anaingia kwenye *production room* akiwa yupo *full armed*. Mahali pekee kwenye dunia unaona kiongozi mkubwa wa ngazi hiyo anaingia kwenye *media house* tena *production room* akiwa na watu wapo *full armed* na silaha. Kuna mambo mawili; la kwanza ni jaribio la Mapinduzi na la pili ni Mapinduzi yenye. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Taifa liko kimya, watu wamezungumza hapa; ni mara ya kwanza tunakuta maiti zipo Mto Ruvu watu saba wameuawa zimefungwa kwenye viroba halafu mnasema Bunge lisijadili, mnatetea akina nani kwenye nchi hii? (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ni mara ya kwanza kwenye nchi Mbunge anawekwa ndani miezi minne mfululizo. Mimi nimeondoka Arusha nimemuacha Lema yupo magereza; mwezi wa Kumi na Moja nimekuja kumtembelea. Nimeondoka nimerudi, nimemaliza *masters* yangu; nimemaliza *semester* mbili namkuta Mbunge bado yupo ndani kwa sababu Hakimu amefungwa mikono ya kutoa masharti ya dhamana, si dhamana. *And you want us to stay quiet?* (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ni Tanzania pekee ambayo Mkuu wa Wilaya ya Arumeru Shija Lutoja Alexander Pastory

Mnyeti ameingia, Madiwani wametengeneza Bajeti ya Halmashauri kwa mujibu wa sheria, wameipitisha. Bajeti ya Halmashauri inajadiliwa na Kamati ya Ulinzi na Usalama na inaamua kupeleka bajeti mbadala; mmewahi kuona wapi ninyi? Ni mara ya kwanza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nimempokea Waziri Mkuu; nipo masomoni Uingereza tunatumiana *email* anakuja Mkoani kwetu muungwana, Mheshimiwa Waziri Mkuu Majaliwa huyu. Nimekuja kumpokea nimepanda ndege kwa gharama zangu sijalipiwa na Bunge kuja kumpokea; namwambia *issues* za wananchi ananiuliza tufanye nini Mheshimiwa Nassari? Namwambia ni hili la ardhi na hili na hili; ametoa maelekezo Waziri wa Ardhi aje Jimboni, nikampongeza, mnakumbuka. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Waziri wa Ardhi amekuja tunakwenda kwenye mkutano wa hadhara wenye matatizo ya wananchi; wananchi waje na mabango na makaratasi, Lukuvi ameagiza. Wanakuja Mkuu wa Wilaya anaongea jukwaani baada ya kuongea hatambui uwepo wa Mbunge, anamuita Waziri jukwaani. Namshukuru ndugu yangu Lukuvi alikataa, *he refused*. Alisema hapana, hili Jimbo linaye mwakilishi wa wananchi; azungumze kwanza mimi Serikali nitajibu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, utawala bora uko wapi? Yaani bajeti ya Halmashauri inajadiliwa kwenye Kamati ya Ulinzi na Usalama; wale wanajeshi wanajuaje wanajuaje kwamba wananchi wa kata 25 za Jimbo langu hawana vyoo, *how do they know?* Tunaongea, wanatoa miongozo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mara ya kwanza kwenye nchi, *first time in the history of this country*, Bunge linafanya kazi likiwa limeingiziwa hofu. *First time in the history of this country*, Bunge linatukanwa halafu unataka nikae kimya? Walisema waliotangulia Bunge linapaswa kulindwa kwa vivu wa hali ya juu. Leo unatoa mwongozo hapa kwamba Wabunge wasiguse Usalama wa Taifa; ni kweli sitaugusa.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini naomba nikukumbushe mwalimu wangu wa sheria; ulimfundisha mke wangu sheria. Nchi hii ina mihimili mitatu; mhimili wa Bunge unasi mamia mhimili wa Serikali; Kitengo cha Usalama wa Taifa nchi hii kipo chini ya *executive*, kinasimamiwa na Bunge. Vitu ambavyo hatuwezi kujadili kwenye Bunge hili ni nchi ina mizinga mingapi, ina vifaru vimekaaje na vimeangalia kushoto au kulia, lakini habari ya kujadili Waziri kama Nape anatolewa bastola mbele ya kamera za waandishi wa habari, *we cannot stay quiet, are you kidding us? (Makofi)* (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Taifa linafika hatua vituo vya redio vinavamiwa usiku saa sita na unataka Wabunge tukae kimya? Leo Mfuko wa Jimbo wa Mbunge unaingiliwa na Mkurugenzi na Mkuu wa Wilaya ndiye anayeamua kwamba miradi gani ipewe pesa wakati Sheria ya Mfuko wa Jimbo imesema *an MP keeps records. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, leo asubuhi, nimeumia sana hapa ndani. Kwa historia za Kiafrika mtu mwenye uchungu na watoto, mtu mwenye uchungu na mtu yeyote; kwa sababu kila aliyekaa hapa ndani ni mtoto wa mama, kila aliyekaa hapa ndani ni mtoto wa mwanamke, yeyote, awe na miaka 90 au miaka 80; wenye uchungu na watoto ni akinamama, ni wanawake, bila kujali vyama vyao. Leo asubuhi hapa mama anaongea habari ya watu kutekwa... (*Makofi*)

*(Hapa kengele illia kuashiria kwisha
kwa muda wa mzungumzaji)*

NAIBU SPIKA: Muda wako umekwisha. Mheshimiwa Mbaraka Dau, atafuatiwa na Mheshimiwa Mendrad Kigola. (*Makofi*)

MHE. MBARAKA K. DAU: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipatia fursa hii ili nami nipate kuchangia Hotuba za Bajeti mbili hizi, Wizara ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI na Utumishi na Utawala Bora.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu aliyetujalia uzima na afya njema. Nielekeze pongezi zangu kwa Mheshimiwa Waziri, George Simbachawene pamoja na dada yangu, Mheshimwa Waziri, Angella Kairuki kwa hotuba nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, teknolojia inakuwa kwa kasi sana siku hizi. Leo tumeshuhudia maelezo hapa mtu anamaliza *semester* mbili ndani ya miezi minne, habari kubwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi leo nimefunga, nimefunga kwa maana nina swaumu au nimejizua kula. Nimefanya hivyo kwa makusudi tu ili nimwombe Mwenyezi Mungu aniongoze katika haya nitakayoyazungumza leo niseme iliyo kweli, basi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye kitabu ambacho nakiamini cha *Quran*, Sura ya 33, Aya ya 70 baada ya *audhubillah mina shaitwan rajim*, Mwenyezi Mungu anasema *Bismillah Rahman Rahim; ya ayuha ladhina aamanuh, takkullah wakulu kaulan sadida*. Hii ni Aya ya Mwenyezi Mungu. Tafsiri yake; Enyi mliaoamini mcheni Mwenyezi Mungu, muabuduni Mwenyezi Mungu na semeni kauli zilizo za kweli' " (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba Mwenyezi Mungu aniongeze niseme ile iliyo ya kweli. Wilaya ya Mafia, Hospitali ya Wilaya ya Mafia ambayo mimi ni Mbunge wao haina huduma ya *X-ray* takribani miaka minne sasa. Nilipokuwa najinadi niliwaahidi wananchi wa Mafia kwamba nikipata fursa hii nitajitahidi kushirikiana na watu mbalimbali Hospitali ya Mafia iwe na *X-ray* mpya kabisa. Nimetimiza, *true to my words*, nimetimiza ahadi hiyo, mwezi wa Nne mwaka wa jana.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kwa masikitiko makubwa sana huu ni mwezi wa Nne mwaka 2017. Mwezi wa Nne mwaka 2016, *X-ray machine* ile mpya imefika Mafia

na katika nukta hii kwa namna ya kipekee kabisa ningeomba nitambue msaada mkubwa sana aliyeutoa mama yetu kipenzi, Mheshimiwa Salma Kikwete alipokuja Mafia. Sina uhakika kama kanuni zinaruhusu Mbunge anayeongea ampigie makofi Mbunge aliyekaa, lakini naomba Bunge tumpe makofi makubwa sana Mheshimiwa mama Salma. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya *X-ray* ile kufika Mafia zikaanza figisufigisu. Mtu wa kwanza; na bahati mbaya simwoni hapa; Mheshimiwa Waziri wa Afya; akatuambia kwamba hamruhusiwi kuifunga kwa sababu tuna mkataba na Kampuni inaitwa *Philips* na kampuni hii ndiyo pekee inayoruhusiwa kufanya ukarabati na matengenezo ya ile *X-ray* ya zamani. *X-ray* ya zamani ni chakavu, ni ya teknolojia ya miaka ya 1970, ukiitengeneza inaharibika. Sasa leo wanasema kuna mkataba na *Philips*, mpaka leo umefika sasa mwaka mmoja *X-ray* ile bado ipo kwenye stoo, nawauliza wahusika wanatuambia mkataba.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mafia ni kisiwa, huna namna kusema kwamba labda mgonjwa utamhamishia hospitali ya jirani, sasa wagonjwa wetu sisi *referral hospital* yetu lazima umpandishe kwenye boti kwa masaa tano kwenda, *referral hospital* Temeke.

Mheshimiwa Naibu Spika, juzi nilikuwa huko wakati wa Pasaka, tumepeleka wagonjwa wawili Hospitali ya Temeke, tunafika Temeke na kwenyewe nako tunaambiya *X-ray* ni mbovu kwa zaidi ya mwezi mmoja, haohao *Philips*. Tunawauliza wahusika wanasema mkataba na *Philips* umekwisha toka mwaka wa jana. Mafia tunazuiwa tusifunge kwa sababu kuna mkataba na *Philips*, Temeke wanasema *X-ray* mbovu *Philips* mkataba umekwisha, tushike lipi? Hili la Temeke watalizungumza wenyewe akina Mheshimiwa Mangungu na Mheshimiwa Mariam Kisangi na ndugu yangu Mheshimiwa Mt Olea lakini mimi najikita kwenye Mafia.

Mheshimiwa Naibu Spika...

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAMISEMI:
Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa!

T A A R I F A

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Dau, naomba ucae na Mheshimiwa Waziri pia naomba ucae nitakupa nafasi.

Waheshimiwa Wabunge mtakuwa mashahidi, Mheshimiwa Dau amelizungumza hili jambo sijui hii ni mara ya ngapi! Sasa Mheshimiwa Waziri nafasi bado nakupa, lakini tafadhali utupe majibu yatakayotuondoa kwenye hili tatizo la Mafia kwa sababu sasa ameshazungumza mara nyingi humu ndani mpaka tunaona ni taabu sasa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Naibu Spika, nimesimama kwa msingi huohuo uliousema kumpa Taarifa Mheshimiwa Mbunge. Nataka nimhakikishie kwamba tumekwishafanya uamuzi kwamba *X-rayile itafutiwe chumba kingine ifungwe na tayari chumba kimekwishatafutwa*. Nataka nimhakikishie kwamba Wizara ya TAMISEMI itatoa shilingi millioni hamsini kwa ajili ya kurekebisha hicho chumba na maelekezo tumekwishayatoa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimhakikishie kwamba hatua tumekwishazichukua kwa sababu tangu amelisema na amelisema na mahali pengine na alilisema hata kwenye chama tulimsikia na tumetekeleza, nilikuwa tu bado sijampa *feedback* yeeye na ndiyo maana amelisema kwa uchungu nikadhani ni vizuri nitumie fursa hii kuweza kumjibu Mheshimiwa. Nataka nimpongeze kwa kazi nzuri aliyoifanya na kwa niaba ya Serikali tunampongeza sana...

MHE. LUCY S. MAGERELI: Mheshimiwa Naibu Spika, Kuhusu Utaratibu!

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: ...kutafuta wafadhili ambao wamemsaidia kununua hiyo *X-ray*.

KUHUSU UTARATIBU

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Magereli!

MHE. LUCY S. MAGERELI: Mheshimiwa Naibu Spika, ni wiki moja iliyopita nililiza swali langu ndani ya Bunge hili kuhusu hoja ya muda na *speed* ambayo tunajikuta tunakwenda nayo mpaka wakati mwingine mambo mengine yanashindwa kutekelezeka.

Mheshimiwa Naibu Spika, Siku ya leo wakati nachangia hii Hotuba ya TAMISEMI, Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI amepata fursa nyingi sana ya kujibu hoja nyingine za Wabunge humuhumu ndani, kitu ambacho naamini si utaratibu. Kama Waziri mwenye dhamana wakati huo bajeti yake ikijadiliwa muda wake ulikuwa unakuja angejibu, lakini naamini mengine mnayapa ruhusa yajibiwe kwa sababu mnajua kwa zile dakika 30 atakazopewa kwa hoja ambazo zimeletwa ndani ya TAMISEMI ni nyingi mno, muda hautatosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo tukubaliane kwamba hakuna utaratibu huo wa kila Waziri ikitokea Hoja ikamfurahisha Mwenyekiti basi akasema Mheshimiwa Waziri Taarifa anapewa fursa azungumze, hiyo sio kweli. Tunaomba utaratibu ufuatwe na ikiwezekana kama basi hivyo ndivyo tuongeze muda wa Bunge ili Mawaziri wapate fursa ya kutosha, Wizara kama TAMISEMI ni kubwa mno dakika 30 hazitoshi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Magereli wakati ukikaa hapo kabla sijamruhusu Mheshimiwa Dau, naomba uipitie Kanuni ya 68(1) ili ikuongoze namna ya kusimama Kuhusu Utaratibu.

Mheshimiwa Dau!

MHE. MBARAKA K. DAU: Mheshimiwa Naibu Spika, niseme tu kwamba naipokea Taarifa ya Mheshimiwa Waziri kwa tahadhari kubwa sana. Kwanza hajanipa *time frame*, kwa sababu hili jambo limekuwa likienda kwa danadana kwa muda mrefu sana. Hicho chumba ambacho wamekitoa mwanzo walisema sisi wenyeje tujenge halafu tuhamishie ile mashine mpya kule. Midhalii yeye amesema leo kwamba wametupatia chumba hicho; mimi nafahamu kule hatuna chumba cha ziada; lakini kama atawea kutupatia kingine cha kujenga haraka kwa hizo milioni 50, tutashukuru sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, labda niliache hili suala kwa sababu nilikuwa nilielezee kwa upana zaidi. Niingie kwenye suala la pili. Kwenye ukurasa wa 11 wa Hotuba ya Mheshimiwa Waziri amezungumzia mlgogoro ya mipaka baina ya wilaya, mikoa, vijiji na vitu kama hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi kule Mafia mipaka yetu ni bahari, hakuna namna nyininge ya kupakana na kijji cha karibu, tunaopakana nao karibu ni ndugu yangu Bwege kule upande wa Kilwa. Tungeomba sana mipaka ya bahari ije iwekwe, kwa sababu kule mafia kuna *exploration* za mafuta zinafanyika, kwa kiasi kikubwa sana zimo ndani ya eneo la Mafia lakini kutokana na *logistics* yale makampuni yanafanya wakitokea Kilwa. Sasa matokeo yake chochote kinachopatikana kinaonekana ni sehemu ya Kilwa wakati kimipaka, kihalsia ile ni sehemu ya Mafia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo tunaomba sana wataalam watakapokuja, sijui wanatumia vitu gani vyatya kisayansi ili kutofautisha mipaka kwenye bahari lakini waje watuoneshe. Kuna kisiwa kimoja kinaitwa Kisiwa cha Ukuza, kisiwa hiki ni sehemu ya Mafia, lakini shughuli zote za kijamii zinafanyika kutokea Kilwa, tungeomba sana Mheshimiwa Waziri hilo nalo atusaidie kutupatia ufanuzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, zahanati; tumeomba zahanati...

*(Hapa kengele illia kuashiria kwisha
kwa muda wa mzungumzaji)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Dau, naambiwa muda wako umekwisha.

MHE. MBARAKA K. DAU: Mheshimiwa Naibu Spika, wewe ni mtu mwema sana, mimi naamini utanipa dakika mbili ili nimalizie hili.

NAIBU SPIKA: Wakati mwingine, nitakupa wakati mwingine. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Mendrad Kigola nilikuwa nime...

MHE. MBARAKA K. DAU: Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Mendrad Kigola, atafuatiwa na Mheshimiwa Ester Mahawe, Mheshimiwa Goodluck Mlinga ajande.

MHE. MENDRAD L. KIGOLA: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nashukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili nami niweze kuchangia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa nianze na kuipongeza Serikali. Serikali ya Awamu ya Tano naamini kabisa iko makini sana; na tunaposema utawala bora maana yake ni kutimiza malengo ambayo uliwaahidi wananchi. Nakumbuka katika Mwaka wa Bajeti 2016/2017, naweza nikayakumbuka malengo ya Serikali 14 ambayo yamefanywa na Serikali na yametekelezeka tayari. Kwanza kabisa, lengo la kwanza, katika ununuzi wa ndege, walisema watanunua ndege sita na sasa hivi kuna ndege mbili tayari ziko zinazunguka Tanzania nzima.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika viwanja vya ndege ambavyo vimefanyiwa upanuzi na Serikali; na usafiri wa anga sasa hivi kila kona wenzetu Watanzania wameanza

kusafiri na naomba kutoa ombi kwamba ndege inayotoka Dar es Salaam kuja Dodoma ipite Iringa iende Mbeya ili na sisi watu wa Iringa tukitoka Dodoma tuweze kupata usafiri wa ndege mpaka Iringa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna watu wengine wameanza kubeza hizi ndege; sisi wa Iringa tunahitaji ndege. Hata kwenye Jimbo langu la Mufindi Kusini tuna viwanja vidogo vitatu, wananchi wale wanataka ndege na wenyewe. Ukienda Ngwazi pale pana kiwanja cha ndege, ukienda Luhunga pale kuna kiwanja kidogo cha ndege, ukienda Mgololo pale pana kiwanja kidogo cha ndege, tunahitaji ndege na sisi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili, katika utekelezaji wa Serikali kuhusu elimu bure. Serikali ilisema itatoa elimu bure kwa watoto wa Watanzania wote na imefanya hivyo, hiyo ni hatua kubwa sana. Kama jambo zuri limefanyika lazima tulisifu. Hata kwa Mungu kama unaanza kupiga maombi kwa Mungu wako wewe humsifii Mungu huwezi kupata Baraka hata siku moja, hilo niwaambie kabisa. Kitu kizuri kimefanyika tuseme hiki kizuri kimefanyika, elimu bure tayari.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye hili suala la elimu bure watu wana-*mislead*, elimu bure sio kwamba ni na kujenga madarasa na mambo mengine, elimu bure maana yake ni ile ada. Watoto kuanzia shule ya awali, shule ya msingi na sekondari wanasoma bure.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la tatu, tatizo kubwa la madawati limepungua kwa asilimia kubwa sana, hata kwenye jimbo langu nilikuwa na tatizo kubwa sana lakini sasa hivi madawati tunaweza tukasema kuna sehemu nyingine wana ziada ya madawati. Watoto walikuwa wanakaa chini sasa hivi wanakaa kwenye madawati. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine, ndugu zangu Waheshimiwa Wabunge, tukitaka uchumi wa Tanzania ukue

ni kutengeneza miundombinu ikae vizuri. Nimeifurahia sana mipango ya Serikali. Kwa mfano kuimarishe usafiri wa reli ni suala la msingi sana. Barabara zilikuwa zinaharibika kwa sababu zinabeba mizigo mizito. Kwa mfano watu wanasafirisha mbao kutoka Iringa mpaka Dar es Salaam, kutoka Iringa mpaka hapa Dodoma kwenye barabara hizi za kawaida, za lami, barabara zinaharibika; lakini mpango wa Serikali wa kusema utaimarisha usafiri wa reli ni mpango mzuri mno.

Mheshimiwa Naibu Spika, Pale Mgololo kuna barabara ya reli imepita, namwomba Waziri wa Uchukuzi, akiangalie kile kituo cha Mgololo; mbao zitoke pale Mafinga ziende moja kwa moja kwenye kituo cha reli ili waweze kusafirisha kwa njia ya treni ili tusiharibu hizi barabara za lami, ziweze kukaa muda mrefu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ambalo ni la msingi sana; tumesema Serikali iimarishe vituo vya afya. Bahati nzuri sisi Wabunge tulipewa semina moja ambayo pia nilihudhuria, ilinisikitisha sana. Inasemekana kwa siku moja akinamama 30 wanakufa kwa ajili ya tatizo la uzazi. Sasa ukichukua 30 ukizidisha mara siku 30 maana yake akinamama 900 wanakufa kwa mwezi mmoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika takwimu pia walisema watoto 180 wanakufa kwa siku moja, ambayo ni hatari. Sasa nataka niiombe Wizara ya TAMISEMI, suala ya kuimarishe vituo vya afya ni suala la msingi sana. Tukitaka kuepukana na hili tatizo la uzazi kwa akinamama lazima tuhakikishe vituo vya afya kule vijijini vimekaa vizuri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, bahati nzuri, naishukuru Serikali, nilisikia wanagawa *ambulance*, *ambulance* kama mia ngapi ziliuja lakini bahati mbaya sana kwenye jimbo langu sikupata. Kwenye kile Kituo cha Mgololo kuna takriban kata tano zinazotegemea kituo cha afya kimoja lakini hakuna *ambulance*. Kwenye bajeti yetu ya Halmashauri tulitenga

500,000,000 ili tuweze kununua *ambulance* tatu, matokeo yake mwaka wa fedha unakwisha lakini zile *ambulance* hatujanunua.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika maswali yangu ya nyuma nilikuwa nauliza kuhusiana na *ambulance* ya Mgololo na Serikali ilikuwa inaniahidi kwamba watanunua ile *ambulance*, wataipeleka pale kituo cha Mgololo lakini mpaka leo hawajapeleka. Nitaiomba Serikali kwenye hilo, ili kuepukana na hili tatizo watupelekee *ambulance* pale. Tukifikia kwenye Bajeti ya Wizara ya Afya lazima tuiangalie vizuri, tuiongeze ili ikae vizuri tuepukane na matatizo ya zahanati na vituo vya afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine linahusiana na umeme. Bahati nzuri sana Mheshimwia Waziri alitoa hotuba nzuri sana na wana mpango mzuri sana; lakini tumewaaahidi wananchi kwamba kila Kijiji kitapewa umeme na wananchi kule wamekaa *standby*. Niombe Serikali, kwenye suala la umeme tunesema kila kitongoji, kijiji na kila kaya watapewa umeme. Tunategemea kwenye vijiji, hasa kwenye Jimbo langu, nina vijiji na kata nyingi sana hazijapata umeme; kwamba tutakapomaliza Mwaka wa Fedha wa 2017/2018 vijiji vingi sana vitakuwa vimeshapata umeme.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikianza kutaja vijiji hapa ni vingi. Kuna kata karibu nane hazina umeme kabisa na ukizingatia Jimbo la Mufindi Kusini ndilo Jimbo linaloweza kuchangia kwenye pato la Taifa asilimia kubwa sana, lakini ukiangalia kwenye miundombinu ya umeme ni duni. Kwa hiyo, naiomba Serikali kwenye Jimbo langu la Mufindi Kusini kama Waziri alivyoahidi, kwamba mpango wa REA kwa mwaka huu wa fedha vijiji vyote vya Jimbo la Mufindi Kusini vitaweza kupewa umeme.

Mhesimiwa Naibu Spika, nakuja kwenye upande wa barabara. Kuna barabara Serikali iliifanyia upembuzi yakinifu na ilishamaliza. Barabara kutoka Nyololo, Igowole mpaka

pale Mtwango. Upembuzi yakinifu ulishafanyika miaka miwili iyopita lakini sasa hivi hakuna kitu kinachoendelea na Serikali ilishaahidi kwamba itajenga barabara ya lami.

Mheshimiwa Naibu Spika, maeneo yale kijiografia mvua zinanyesha kila siku, kwa hiyo magari yanashindwa kusafirisha chai kule. Kuna viwanda ambavyo ni viwanda vikubwa katika *East Africa*. Ukipensa Kiwanda cha Chai katika *East Africa* lazima uende pale Mufindi, lakini barabara ile ni tazito na pato kubwa la Taifa linatoka katika kile kiwanda cha Chai Mufindi. Sasa naiomba Serikali, ile barabara ambayo iliahidi kwamba itajengwa kwa kiwango cha lami, basi iweze kutekeleza ahadi yake hiyo. Bahati nzuri sana hata kwenye llani ya Chama cha Mapinduzi iliwekwa nina imani kabisa watamaliza kujenga ile barabara.

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho; niseme kwamba naipongeza Serikali, nasema ikaze mwendo na sisi Waheshimiwa Wabunge tuko nyuma yako ili tuweze kutekeleza ahadi tulizoahidi kwa wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana, Mheshimiwa Esther Mahawe, atafuatiwa na Mheshimiwa Goodluck Mlinga, Mheshimiwa Dkt. Shukuru Kawambwa ajiandae.

MHE. ESTHER A. MAHAWE: Mheshimiwa Naibu Spika ahsante sana. Kwanza kabisa napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa ajili ya kutupa afya sisi wote tulioko ndani ya Jengo hili Tukufu la Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kwanza kabisa nielekeze pongozi zangu za dhati kwa Mheshimiwa Rais Dkt. John Pombe Magufuli kwa kazi yake nzuri sana anayofanya kupitia kwa Mawaziri hawa wawili wa TAMISEMI, Mheshimiwa Simbachawene na Mheshimiwa Jafo, kwa kweli kazi inafanyika. Niseme tu kwa upande wa Mkoa wa Manyara tunashukuru sana Serikali, tayari tumeanza kuona kwamba

kwa kweli kazi inapigwa. Tunategemea kuboreshewa zahanati zetu katika Wilaya nne za Mkoa wa Manyara; Wilaya ya Mbulu Mjini na Jimbo la Mbulu Vijijini, Babati Mjini, Babati Vijijini na Wilaya ya Simanjiro, zahanati ile ya *Urban* Orkesumet inakwenda kuboreshwa sasa kwenda kwenye hadhi ya kituo cha afya; shughuli hii siyo ndogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia naomba nipongeze juhudzi za Serikali. Tumekuwa na kilio cha maji muda mrefu katika Wilaya ya Simanjiro sasa mradi mkubwa wa maji kutoka Mto Ruvu unaelekea katika eneo la Orkesumet Makao Makuu ya Wilaya ya Simanjiro, ni mradi ambaa utaondoa tatizo la maji kwa kiwango kikubwa sana, kwa kweli naipongeza Serikali. Wale wanaosema hakuna kinachofanyika na bajeti iliyoletwa hapa mwaka jana ni hewa siyo kweli.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia niseme kwamba tayari *tender* ya Daraja la Magara ambalo tumekuwa tukilipigia kelele sana watu wa Babati na watu wa Mbulu, imetangazwa. Niiombe Serikali iwahishe kupeleka fedha daraja lile lianzu kutengenezwa ili wananchi wetu waanze kupona.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba njielekeze kwenye *TASAF*. Mfuko huu wa *TASAF* kwa kweli binafsi katika kutembea kwetu tulipokuwa kwenye Kamati katika Mikoa ya Mbeya, Iringa na Njombe ulionesha mafanikio makubwa sana katika kuondoa umaskini wa wananchi wetu. Wananchi hawa wenyewe wametoa ushuhuda jinsi gani Mfuko huu umekuwa wa msaada sana kwao. Watoto wanakwenda shule, watoto wanapelekwa *clinic* kwa idadi kubwa, watu wanapata bima ya afya; huu siyo Mfuko wa kubezwa hata kidogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, niiombe Serikali na yenyewe iweze kuchangia sehemu inayotakiwa kuchangia ili Mfuko huu uendelee kudumu na kuendelea kusaidia kwa sababu wananchi wengi wameshatoka katika hali ya umaskini. Wale

walio-graduate unaona kabisa tayari wana nyumba bora, maisha yao yamebadilika. Ni Mfuko ambao kwa kweli unahitaji kuongezewa nguvu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini hapo hapo pia niseme kwamba kuna changamoto ndogo ndogo zilizojitokeza kwenye zile kaya ambazo zilionekana ziliingizwa kinyume na utaratibu. Ninachoshauri tu ni kwamba, haki itendeke kwa watu wale ikiwa huenda wengine waliondolewa bila kuona kwamba wanastahili ama la maana pia walipaswa kurejesha fedha zile walizokwishapewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri kwamba wale waratibu waliohusika kuingiza watu ambao hawakuhusika wao wawajibike zaidi kuliko mwananchi ambaye hali yake ni duni na alishapewa fedha zile za kujisaidia na bado anapaswa kurudisha. Kama alipewa kwa sababu ni maskini anazitoa wapi leo? Kwa hiyo, nashauri hili lifanyike kwa umakini mkubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna huu MKURABITA. MKURABITA katika maeneo ya Njombe tumeona watu wametoa ushuhuda. Wale ambao ardhi zao zimerasimishwa na tayari wanatumia zile hati zao kuchukua mikopo mikubwa katika Mabenki tofauti. Tulishangaa kuona kwamba mtu ana uwezo wa kukopeshwa kuanzia milioni 100 mpaka 400 kwa kutumia hati hizi za Kimila, kwa kweli ni hatua kubwa mno Serikali imepiga katika hili. Niendelee kuitia moyo Serikali yangu ya kwamba sasa iendelee kupanua wigo wa kusaidia hati hizi za kimila zipatikane katika maeneo mengine ambayo hayajafanyiwa kazi namna hiyo. MKURABITA ushirikiane na Halmashauri zetu mbalimbali nchini ili wananchi wetu waweze kufaidika. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia wakati mwингine kuna changamoto katika upelekwaji wa fedha. Tunafahamu mambo yaliyofanyika ndani ya kipindi cha mwaka mmoja kwenye Serikali yetu kupitia Mheshimiwa Rais ni mambo makubwa na mambo mengi ambayo kiukweli hayapaswi kudhihakiwa, bali tumtie Rais wetu moyo kazi inapigwa sana.

Hata hivyo, niombe, bajeti hii tunayojadili sasa iweze kupelekwa kwa wakati katika Halmashauri zetu. Kuwe na ushirikiano mkubwa na wa kutosha kati ya Serikali Kuu na Halmashauri zetu ili kwamba kazi ziweze kufanyika kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, ilijitokeza pia changamoto kuhusu zile asilimia tano za wanawake na tano za vijana. Kwa sababu ya kucheleweshwa kwa fedha hizi za *OC* kufika kwa wakati katika Halmashauri, imeonekana ile asilimia 10 kuelekezwa katika mambo mengine katika Halmashauri kwa, mfano; suala la madawati, maabara na vitu vya namna hiyo, hatulaumu zote ni kazi, lakini kwa sababu fungu hili lipo kisheria basi Serikali iangalie namna bora zaidi ya kufikisha zile fedha kwa wakati ili akinamama na vijana waweze kujikwamua katika lindi hili la umaskini kupitia kukopeshwa fedha zile za asilimia tano za vijana na tano za wanawake. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, najua tayari tulimaliza changamoto za madawati, sasa hivi maeneo mengi tuna changamoto kubwa ya upungufu wa madarasa, mashimo ya vyoo pamoja na nyumba za Walimu. Ni kweli kwamba elimu bora inahitaji uwekezaji, hakuna muujiza; Walimu hawa watakapokuwa pia wamepata maeneo mazuri kwa maana ya madarasa toshelevu watafundisha watoto wetu vizuri na wanafunzi hawa wataelewa. Pia matundu ya vyoo yaendane sawa sawa na idadi ya wanafunzi walioko kwenye shule husika. Nafahamu Serikali yetu sikivu imejipanga kwa hili kwa mwaka huu wa 2017/2018 ili kuhakikisha tunaondokana na changamoto hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala hili la upungufu nalo linaendelea kwenye maeneo mengine kama zahanati ambapo tuna upungufu mkubwa wa vyumba ama nyumba za wafanyakazi wa kada ya afya. Waganga wetu hawana mahali pa kuishi, wanaishi mbali na maeneo ambayo yanapaswa kutolewa huduma za afya. Tunaomba pia Serikali itazame hilo katika kipindi hiki cha bajeti. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kwa dakika chache zilizobaki niweze kusema machache kuhusu habari ya utumishi na utawala bora. Nasikitika sana kwa bahati mbaya sana niliyoionna kwenye hotuba ya dada yangu Mheshimiwa Ruth; sikuona, hotuba yao haikugusa suala zima la rushwa ambalo Serikali yetu imepambana nalo na sasa inaanza kuwa hadithi. Si hivyo tu, utawala bora ni pamoja na uhakiki mkubwa na mrefu uliofanywa na Serikali ili kuondoa mianya yote iliyokuwa inatumika kupoteza fedha za nchi hii. Kazi hiyo imefanyika kwa umakini mkubwa na fedha nydingi zimeokolewa, lakini hilli hatukuliona pia likizungumzwa. Kwa hiyo, niseme tu, najua kwamba kazi yao siyo kuisifu Serikali yetu, lakini sisi kama Waheshimiwa Wabunge wa Chama Tawala, kwa kweli tunapongeza sana juhudhi hizi ambazo zimefanywa katika awamu hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini niombe tu kwamba juhudhi hizi ziendelee kufanywa na Serikali. Nampongeza sana Mheshimiwa Angella Kairuki.....

MHE. RUTH H. MOLLEL: Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

MHE. ESTHER A. MAHAWE: ...na timu yake nzima, wanafanya kazi nzuri sana kuhakikisha wanaokoa fedha nydingi. TAKUKURU...

T A A R I F A

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Ester Mahawe, kuna taarifa unataka kupewa. Mheshimiwa Ruth Mollel.

MHE. RUTH H. MOLLEL: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Nasimamia kanuni ya 68(8) kumtaarifu Mheshimiwa Mahawe kwamba yeye anaweza kuchangia kuhusu hilo jambo la TAKUKURU si lazima nizungumzie katika taarifa yangu. Kwa hiyo, ajikite ni kitu gani anataka kulitaarifu Bunge. Ahsante. (*Makof!*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Esther Mahawe unaipokea hiyo taarifa ama unaikataa?

MHE. ESTHER A. MAHAWE: Mheshimiwa Naibu Spika siipokei kwa sababu unapojuza kusema mabaya tu ujifunze kusema na mema pia. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, suala zima la uwajibikaji (*accountability*) lilikuwa halipo mahali pale, leo kuna *accountability* ukifika hata kwenye ofisi zetu za Serikali unasikilizwa hakuna tena njoo kesho, njoo kesho kutwa, ni sehemu ya utawala bora. Unaifika hospitali unatibiwa hakuna rushwa ni sehemu ya utawala bora. Hii kazi inafanywa na Serikali hii ya Awamu ya Tano ya Dkt. John Pombe Magufuli.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia ubadhirifu haupo tena, tayari Serikali ipo kazini inapambana na suala zima la ubadhirifu wa mali ya umma; hayo yote tumeyaona, mbona hatukuyaona kwenye hii hotuba? Wamesema hii ni Serikali ya kuhakiki, yes, we are after accountability, lazima kuwe na uhakiki ili kila mmoja awajibike kwa zamu yake. Wakati Serikali haihakiki wanasema Serikali gani hii, leo inahakiki wanasema Serikali ya kuhakiki; wanadamu hawana jema, Mawaziri wetu chapeni kazi tuko nyuma yenu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia nizungumzie suala la *performance based payments*. Kuna zile *on call allowances*, labda kwa Madaktari na Manesi au kwa Walimu wetu. Wakati mwengine baadhi ya Walimu wametuhumiwa labda wanafanya biashara ya bodaboda wakati wa vipindi, kwa hiyo labda madarasa hayafundishwi inavyotakiwa. Ifike mahali ile *performance based payment* ifanye sehemu yake ili kuboresha huduma katika taasisi mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga mkono hoja. Ahsante sana. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Goodluck Asaph Mlinga atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Shukuru Kawambwa, Mheshimiwa Jesca David Kishoa, ajiandae.

MHE. GOODLUCK A. MLINGA: Mheshimiwa Naibu Spika ahsante sana. Kwanza, wiki iliyopita kwa siku mbili mfululizo nimetuhamiwa kuwa nabebwa na kitu chako kuwa natumia nafasi yangu vibaya, kwa hiyo naomba; unapopata tuhuma kama hizi, ninapopata nafasi kama hii inabidi na mimi nijitetee kwa nafasi yangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ulifanyika uchaguzi wa Wabunge la Afrika Mashariki. Wajumbe walioletwa kutoka upande wa CHADEMA walipata kura nyingi za hapana; lakini naomba nifafanue kuititia mkataba wa uanzishwaji wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (*The Treaty For The Establishment of East African Community 1999*) ambao umekuwa Revised mwaka 2006, Article 50; *Election of Member of the Assembly*

MHE. HALIMA J. MDEE: Kuhusu utaratibu

MHE. GOODLUCK A. MLINGA:namba moja, inasema hivi.....

MHE. HALIMA J. MDEE: Kuhusu utaratibu

MHE. GOODLUCK A. MLINGA:*The National Assembly of each Partner State....*

KUHUSU UTARATIBU

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Mlinga naomba ukae. Kuhusu utaratibu Mheshimiwa Halima

MHE. HALIMA J. MDEE: Mheshimiwa Naibu Spika, kanuni ya 64(1) (b) naomba niisome:-

"Bila ya kuathiri masharti ya ibara ya 100 ya Katiba yanayolinda na kuhifadhi uhuru wa mawazo na majadiliano katika Bunge, Mbunge hatazungumzia jambo ambalo haliko kwenye mjadala."

(Hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge waliongea bila mpangilio)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge tusikilizane,

MBUNGE FULANI: Kaa chini, kaa chini!

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Halima ongea na kititafadhalii.

MHE. HALIMA J. MDEE: Mheshimiwa Naibu Spika, mdogo wangu Mlinga anazungumzia suala la uchaguzi wa Bunge la Afrika Mashariki. Kwa maelezo yake, anasema kwa kuwa leo amepata nafasi ya kuzungumza, basi ni nafasi yake ya kujitetee kujibu tuhuma ambazo ziliwuwa *raised* na watu katika mijadala mbalimbali ya Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, mosi, tunajadili Ofisi ya Rais TAMISEMI na masuala ya Utumishi. Masuala ya...

(Hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge waliongea bila mpangilio)

MHE. HALIMA J. MDEE: Tulieni!

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Halima ongea na mimi ndiye ninayekusikiliza, kwa hiyo ongea na mimi hapa.

MHE. HALIMA J. MDEE: Naona ndiyo wanachokonoa sasa sababu wanataka wapate wanachokitaka.

(Hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge waliongea bila mpangilio)

MBUNGE FULANI: Mambo hayooo!

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Halima ukisimama kusikiliza Wabunge wenzio tutakuwa hatumalizi mimi na wewe. Wewe unaniambia Naibu Spika.

MBUNGE FULANI: Ameshakunywa ki.....

NAIBU SPIKA: Nakusikiliza kwa hiyo wewe zungumza.

MHE. HALIMA J. MDEE: Mheshimiwa Naibu Spika ninachokisema ni hiki, kama kitu chako na naamini kwa sababu vilevile wewe ni Mwalimu wangu umenisimamia *Thesis ya Masters*, umenielewa. Kama tunasimamia kanuni hizi, suala la Ubunge ama uchaguzi wa Bunge la *EALA* si ajenda hapa. Kwa hiyo, kama Mheshimiwa Mlinga ana la kusema asizungumze kujibu hoja zilizokuwa *raised* na watu wakati hoja hizo zilitolewa wiki moja iliyopita na kuna utaratibu wa kikanuni kama kuna mtu hajaridhika na mambo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, niombe ili ule mwongozo ulioutoa usimame, tujadili mambo ambayo yapo kwenye hotuba. Sasa ukiruhusu watu waongee wanavyotaka kuzungumza maana yake ni kwamba na sisi huku hatukosi la kusema. Kwa hiyo, naomba kitu chako suala linalohusiana na uchaguzi wa *EALA* si sehemu yake. Uchaguzi ulifanyika, yaliyofanyika yalitokea, tunasubiri utaratibu wa Katibu wa Bunge akiandikie Chama chetu tuweze kuleta utaratibu mwingine kwa kadri ambavyo maelekezo yanasema.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo nakupa hii mwongozo wa kikanuni, kanuni ya 64(1)(b). Ana mengi ya kuzungumza, mengi tu kama anataka kupiga mawe mengi tu lakini...

NAIBU SPIKA: Naomba umalize Mheshimiwa Halima.

Waheshimiwa Wabunge, kanuni zetu hizi zinagusa kila jambo, Mheshimiwa Halima ametupeleka kwenye kanuni ya 64(1) (b) ambayo inasema:

"Mbunge hatazungumzia jambo ambalo haliko kwenye mjadala."

Waheshimiwa Wabunge kanuni hiyo iko wazi na kwa kuwa Mheshimiwa Mlinga alikua bado akizungumza sikujua hoja yake inazungumzia nini, lakini niwakumbushe tu vizuri ili wote twende sawasawa.

Ukurasa wa tano na kwa sababu nimekisoma kifungu hicho cha 50, cha ule Mkataba unaoanzisha Afrika Mashariki, ukurasa wa tano wa mchango ama hotuba ya Kambi Rasmi ya Upinzani, iliyoletwa na Mheshimiwa Ruth Mollel inazungumzia... (*Makofi*)

Waheshimiwa tusikilizane ili twende vizuri. Nimesema hivi, kwa kuwa sisi wote hapa hatukujua anataka kuzungumzia nini katika kujenga hoja yake. Nishauri tuwe tunajitahidi, si mara zote tunaweza lakini tuwe tunajitahidi kadri tunavyoweza kuwa wavumilivu kwenye hii michango. Kwa sababu kama nitakuwa kweli nasimamia kanuni kama Mheshimiwa Halima anavyosema, mambo mengi watu wanajenga hoja; yaani tuseme wanaanza mahali wanajenga wee mpaka ije kufika ndipo anazungumzia kitu cha leo. Tukisema hivyo, hizi kanuni hicho kifungu kinachozungumzia uchaguzi, mlimi sijui hoja yake ilikuwa nini, lakini nimewarudisha hapa ikiwa hoja yake inaelekea huko,

Sasa niwakumbushe jambo moja tu, kanuni ya 64 ina mambo ya jumla yanayokatazwa. Sasa tujaribu sisi wenyewe kupima mambo tunayochangia ili tusipoteze muda katika kusimama kila wakati. Kwa hiyo, tuangalie hayo pande zote na sisi wote tunaosoma kanuni tusikilize mawazo ya pande zote yanavyosema ili yote yanavyovunjwa yaonekane sawasawa. Mheshimiwa Mlinga endelea.

MHE. GOODLUCK A. MLINGA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana naomba muda wangu ulindwe, Mheshimiwa dada yangu Halima Mdee amesahau kumalizia Utawala Bora. Naomba niendelee.

Mheshimiwa Naibu Spika, *Article 50, election member of Assembly* inasema hivi:-

"The National Assembly of each partner state shall elect..."

Mheshimiwa Naibu Spika, wewe ni shahidi kuwa CCM tulikuwa tuna nafasi sita, tulileta watu kumi na mbili.

MHE. JOSHUA S. NASSARI: Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa, kwa mujibu wa kanuni

MHE. GOODLUCK A. MLINGA: Najenga hoja, najenga hoja nimetuhumiwa.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Nassari taarifa kwa kifupi kwa sababu muda wetu unakimbia tunaumaliza kwenye taarifa kwa kifupi tu.

T A A R I F A

MHE. JOSHUA S. NASSARI: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kumpa taarifa Goodluck Mlinga, kwamba anachokisoma kinasema *a partner state and not a political party, a political party* ni CCM, CHADEMA na NCCR ni ACT wote wana vyama huku wana wawakilishi.

MBUNGE FULANI: Amelewa huyo amelewa!

MHE. JOSHUA S. NASSARI: ...wanaokwenda kwenye Jumuiya ya Afrika Mashariki wanakwenda kama...

NAIBU SPIKA: Ahsante Mheshimiwa Nassari, naomba tuendelee. Waheshimiwa Wabunge naomba tusikilizane, unapojenga hoja yako uwe mvumilivu mwenzio pia anapojenga ya kwake, kwa sababu hujamsikiliza bado, mwache ajenge hoja yake amalize. Mheshimiwa Mlinga.

MHE. JOSHUA S. NASSARI: *Partner State* siyo CCM Mheshimiwa....

WABUNGE FULANI: Kelele amelewa, amelewa Nassari!

MHE. GOODLUCK A. MLINGA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Alipokuwa anaelekea Mheshimiwa Nassari ndiyo huko huko ndio nilikuwa naenda. Kifungu namba moja kinasema hivi; *a partner state shall elect assembly*, yaani kwa Kiswahili Bunge la nchi mwanachama litachagua. CHADEMA mlichagua huko hapa mlileta tu-

approve, hapa tofauti ni lugha. Ndiyo maana nasema CHADEMA mna Wanasheria wengi, lakini hao Wanasheria wanashinda mahakamani kuwatetea watu ambao wanamtukana Rais badala ya kuwasaidia nyinyi humu. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la pili ambalo lilipigwa kelele ni suala la *gender*. Katika hicho hicho kifungu namba moja ukiendelea kukisoma mbele kimezungumzia *gender, interest groups*. Nikauliza ninyi mtuambie, mnatulaumu sisi hatujachagua hii kanuni mlisoma? Imezungumzia *gender*, nikawaambia mniambie kati ya Masha na Wenje nani alikuwa anawakilisha hizo gender? Mmekataa kusema, matusi yangu yako wapi?

Mheshimiwa Naibu Spika, ndiyo maana nasema hivi tuwe tunaangalia viongozi tunaowachagua, wakati sisi tunachagua Mwenyekiti wetu wa Chama wa *PhD*, ninyi mlichagua Mwenyekiti wenu wa Chama *form six zero*. (*Makofi*)

MHE. GOODLUCK A. MLINGA: Mheshimiwa Naibu Spika, suala langu la pili, naomba niishukuru Serikali kwa uje...

KUHUSU UTARATIBU

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Mlinga, kuhusu utaratibu.

(Hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge waliongea bila mpangilio)

MBUNGE FULANI: Mheshimiwa Naibu Spika, wanakula muda wa Mheshimiwa Mlinga.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Halima Mdee

MHE. HALIMA MDEE: Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu utaratibu...

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Gekul, Mheshimiwa Halima amesimama, kwa hiyo mnataka kuzungumza wote wawili

kwa wakati mmoja? Nimemtaja Mheshimiwa Halima, sasa ukisimama na wewe unataka nani azungumze. Nimemtaja mtu mmoja Mheshimiwa Halima Mdee zungumza.

MBUNGE FULANI: Nassari ameleta konyagi.

MHE. HALIMA J. MDEE: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza narejea kanuni namba 64 1 (a) na kanuni ya 63 (1), (2), (3) mpaka (9) (10) na vifungu vyake vyote.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, kanuni ya 64 inasema hivi:-

"Bila ya kuathiri ya masharti ya Ibara mia moja ya 100 ya Katiba yanayolinda na kuhifadhi uhuru wa mawazo na majadiliano katika Bunge, Mbunge:-

(a) hatatoa ndani ya Bunge taarifa ambazo hazina ukweli;"

Mheshimiwa Naibu Spika, hiyo ni A, lakini kanuni ya 63 (1) inasema:

Bila kuathiri masharti ya ibara ya 100 ya Katiba yanayolidha na kuhifadhi uhuru wa mawazo na majadiliano katika Bunge, ni marufuku kabisa kusema uongo Bungeni na kwa sababu hiyo, Mbunge ye yeyote napokuwa akisema Bungeni ana wajibu wa kuhakikisha kwamba anatoa kauli au maelezo kuhusu jambo au suala ambalo yeye mwenyewe anaamini kuwa ni la kweli na siyo jambo la kubuni au la kubahatisha tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kanuni ya (2), (3), (4) na (5) inaelelezea Mbunge kutakiwa kuthibitisha kauli anayoisema. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Mlinga amesema Kiongozi wa Kambi ya Upinzani Bungeni, ambaye ni Mwenyekiti wa CHADEMA amepata sifuri...

(Hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge waliongea bila mpangilio)

MBUNGE FULANI: Aseme mmoja!

MHE. HALIMA J. MDEE: Naomba tuheshimiane.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Halima naomba uzungumze na kiti tafadhali

MHE. HALIMA J. MDEE: Mheshimiwa Mlinga, kwa maelezo aliyyoatoa na tukitaka tutaiomba *hansard* hapa ithibitishe, amesema Mwenyekiti wa CHADEMA amepata zero *form six*. Sasa, sisi tunataka kwa kanuni hizi, akilinganisha na Mwenyekiti wa CCM ambaye ana *PhD*; mimi hapa sitaki kuzungumza biashara ya *PhD* ya Magufuli kwa sababu nikitaka kuzungumza tutavyana nguo hapa; sitaki kwenda huko. Ila ninachokitaka hapa ni kiti chako, kwa watu wanapotoa kauli za aina hii ambazo ni za uongo, ambazo zinadhalilisha viongozi wakubwa wa Serikali na Chama athibitishe na akishindwa kuthibitisha kuna utaratibu wa kikanuni wa kuwaadhibu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaendekeza hawa watu, tunaadhibu upande mmoja ndio maana watu wana...

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Halima umeomba kuhusu utaratibu, wewe onesha kanuni iliyovunjwa ongea na mimi, ukianza na wewe tena kumjibu mashambulizi hatutafika mahali. Zungumzia utaratibu ili mimi niweze kutoa maamuzi.

MHE. HALIMA J. MDEE: Nimekusomea kanuni ya 63 yenye kifungu cha kwanza mpaka cha kumi na utaratibu wake. Nimekuelezea kifungu cha kanuni ya 64(1)(a), huyu kijana amesema uongo, alithibitishie Bunge hili, kwa sababu Mheshimiwa tukisema yanayosemwa...

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Halima umesema, alithibitishie Bunge, umemaliza hoja yako, subiri basi mimi niamue juu ya jambo hilo. Umemaliza umeshanirudisha

kwenye kanuni hizo hizo mara mbili unarudia hoja hiyo na mimi nimeshakuelewa, subiri nitoe maamuzi. Tafadhalii naomba ukae.

Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Halima amesimama kwa mujibu wa kanuni ya 64 ambayo fasili ya pili inampa nafasi ya kuomba kuhusu utaratibu akiona kuna kanuni inavunjwa. Mheshimiwa Halima ametoa maelezo ya kuvunjwa kwa kanuni ya 64(a) na kwamba Mbunge hatatoa ndani ya Bunge taarifa ambazo hazina ukweli; na anazungumzia jambo hili kuhusu mchango wa Mheshimiwa Mlinga kumtaja Mwenyekiti wa chama ambae hajafanya vizuri mitihani yake ya *form six*.

Mheshimiwa Halima Mdee ametupeleka kwenye kanuni ya 63 inayozungumzia kutosema uongo Bungeni. Waheshimiwa Wabunge, kanuni ya 63 (3) inasema hivi:-

(3) Mbunge mwingine ye yote anaweza kusimama mahali pake na kutamka "kuhusu utaratibu" na baada ya kuruhusiwa na Spika, kudai kwamba, Mbunge aliyekuwa anasema kabla yake ametoa maelezo ya uongo kuhusu jambo au suala alilokuwa analisema Bungeni.

(4) Mbunge anayetoa madai kwa mujibu wa fasili ya (3) ya Kanuni hii atakuwa na wajibu wa kutoa na kuthibitisha ukweli kuhusu jambo au suala hilo kwa kiwango cha kuliridhisha Bunge.

Waheshimiwa Wabunge Kanuni ya 63(3) na (4) inamzungumzia Mbunge aliyemomba kuhusu utaratibu siyo aliyetoe hoja. Sasa tusikilizane na tuelewane vizuri. Kanuni hizi zina ujuzi au zinayo mambo yote. Sasa hizi fasili mbili nilizosoma zinamhusu mtu aliyemomba kuhusu utaratibu; yeye ndiye anayeanza kuthibitisha kwanza kabla ya mtoe hoja. (*Makofii*)

(Hapa Mheshimiwa Halima James Mdee alisimama)

NAIBU SPIKA: Sasa Mheshimiwa Halima nimesimama usisimame, kanuni ziko wazi nikisimama usisimame.

Sasa baada ya kusema hayo fasili ya (5), Mheshimiwa Halima ametoa maelezo marefu na mimi sitotaka kwenda kwenye hayo. Fasili ya (5) inataka yeye akishathibitisha kwamba yule anaYesema anazungumza uongo na kitikajiridhisha kwamba kweli yule anazungumza uongo kwa uthibitisho uliotolewa na aliyeomba kuhusu utaratibu, kitikitamtaka mtu yule afute kauli yake kwa mujibu wa fasili ya (5) au afute maelezo yake.

Sasa tuzielewe vizuri hizi kanuni, pamoja na kusema...

(Hapa Mheshimiwa Halima James Mdee alisimama)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Halima, tafadhali Mheshimiwa Halima, umeshasema mimi ni mwalimu wako nireshimu hata kwa hilo basi. Nireshimu hata kwa hilo tu. (*Makofii*)

Waheshimiwa Wabunge anayetakiwa kuthibitisha kwenye hili ni Mheshimiwa Halima, kwamba Mlinga anasema uongo. Kwa mujibu wa kanuni hii. Sasa, kwa sababu tunayo kazi mbele yetu, mimi sitataka kwenda kwenye hayo, moja, mbili, tatu. Waheshimiwa Wabunge pamoja na maelezo hayo yote niliyoyatoa, nimetoa hivyo ili Kanuni hizi tuzielewe usimwambie mtu kasema uongo kama wewe hunu uthibitisho wa kuonesha tofauti.

La pili, na ndiyo natoa sasa maelekezo, Mheshimiwa Mlinga kwa sababu nimesema sitaki kwenda mbele, nyuma kuhusu hili, Mheshimiwa Mlinga kwenye hili kama hauna uthibitisho tafadhali kwa kutumia fasili ya (5) futa kauli hiyo, ama maelezo uliyoyatua tuweze kusonga mbele. Mheshimiwa Mlinga. (*Makofii*)

MHE. GOODLUCK A. MLINGA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Naomba muda wangu ulindwe,

nimesema sisi wakati tunachagua Mwenyekiti *PhD holderwao* walichagua *form six zero*, sijasema wao nani.

MBUNGE FULANI: Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa, kuhusu utaratibu.

MBUNGE FULANI: Ukimaliza kuchangia uijie pitcha za mama yako!

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Nassari naomba ukae.

(Hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge walismama na kuongea bila utaratibu)

MBUNGE FULANI: Amelewa huyo Nassari! Amelewa huyo Nassari.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Nassari naomba ukae, nimekusihi mara nyingi naomba ukae, tafadhali naomba ukae. Mheshimiwa Kubenea naomba ukae, naomba ukae Mheshimiwa Kubenea.

Mheshimiwa Mlinga, ukisema sisi na wao humu ndani ye yeyote utakayekuwa unamwambia anajulikana, labla kama utakuwa unazungumzia watu wa nje. Naomba ili tuweze kusonga mbele tafadhali futa kauli yako uendelee na michango yako. (*Makofi*)

MHE. GOODLUCK A. MLINGA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Kwa sababu nilisha-*declare* humu ndani kuwa yule ni baba mkwe wangu naomba niyafute hayo maneno. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niende upande wa Jimbo langu la Ulanga...

MHE. SAED A. KUBENEÀ: Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa!

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Kubenea, naomba ukae tafadhali

MHE. SAED A. KUBNEA: Taarifa.

NAIBU SPIKA: Naomba ukae Mheshimiwa Kubenea, Mheshimiwa Mlinga malizia.

MHE. GOODLUCK A. MLINGA: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nafasi ya pekee niishukuru Serikali kwa ujenzi wa Daraja la Kilombero. Kwa Waheshimiwa Wabunge ambao mmeshatembelea lile Jimbo la Ulanga mliuona ule Mto Kilombero, limetusaidia kwa kiasi kikubwa sana. Watu walikuwa wanakufa upande wa pili huku wakiiona hospitali ipo upande wa pili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kwa namna ya pekee kabisa, shukrani za pekee kutoka kwa wana Ulanga. Naiomba Serikali ijaribu kutusogezea kipande cha lami kutoka Kilombero mpaka Mahenge Mjini, hiyo itakuwa imetusaidia sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mvua zinanyesha, kwenye Jimbo langu la Ulanga tumekumbwa na adha kubwa ya mafuriko, madaraja yamebomoka, hamna mawasiliano kutoka Kata moja kwenda nyingine. Naiomba Serikali kwa jicho la pekee walitazame Jimbo la Ulanga. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la Walimu. Serikali ilisimamisha kupandisha madaraja Walimu kwa muda mrefu kwa ajili ya kupisha uhakiki, maajabu yangu yanayokuja, kuna Walimu wamekaa miaka kumi na mbili hawajapandishwa madaraja. Leo hii Serikali imekuja na uamuzi kuwa Mwalimu hawezi kupandishwa daraja mpaka aende mafunzo. Hao waliokaa miaka kumi na mbili wakisubiria kupandishwa madaraja hajatoa mwongozo watawafanya? Wengine wanakaribia kustaafu na wamefanya kazi muda mrefu.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la tatu, katika Jimbo langu la Ulanga wananchi wamejitlea hasa Kata ya Ilagwa wamejenga shule wameweka watoto wanasoma, wenyewe wazazi wameajiri Walimu, lakini Serikali mpaka leo hii

wameshindwa kuzisajili hizo shule. Naomba Serikali kwa fursa ya pekee kabisa muwasapoti wananchi wa Ulanga kwa kuzisajili shule hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la nne, katika Halmashauri ya Wilaya ya Ulanga Wakuu wa Idara wengi wanakaimu, hii inachelewesha maamuzi. Kwa hiyo, naomba Utumishi kwa kushirikiana na TAMISEMI, mfanye mchakato wa haraka hawa Wakuu wa Idara wathibitishwe ili kutochelewesha maamuzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala langu la tano; katika historia yangu ya maisha nilimsikia mtu mmoja marehemu aliyekuwa anaitwa Kombe. Kombe kwa nilivuosoma kwenye vitabu ni kwamba alipigwa risasi na watu, Maofisa wa Serikali; lakini kwa macho yangu nimeshuhudia hivi karibuni Waziri mstaafu na Katibu Mwenezi Mstaafu wa Chama cha Mapinduzi alitolewa bastola hadharani, bila kificho na watumishi wanaosadikiwa kuwa ni wa Serikali. Nilitegemea Mheshimiwa Waziri Mkuu atatoa kauli, Mawaziri mtatoa kauli, Wabunge mtatoa kauli. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa basi, kama yule Waziri mstaafu ametolewa bastola hadharani Serikali ikakaa kimya, leo hii tutakuwa na uhakika gani hawa wanaoua maaskari si Watumishi wa Serikali?...

MHE. BAKARI M. MUSSA: Mheshimiwa Naibu Spika taarifa.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Mussa muda wetu umekwisha, kwa hiyo, madamu ni taarifa hiyo inaweza ikasubiri, lakini suala la utaratibu kwa sababu ni uvunjifu wa kanuni hilo nitaruhusu, taarifa mtaniwia radhi Waheshimiwa Wabunge. Endelea Mheshimiwa Mlinga.

MHE. GOODLUCK A. MLINGA: Mheshimiwa Naibu Spika, hoja yangu niliyokuwa najaribu kujenga, hawa askari

na wananchi ambao wanauawa tutakuwa na imani gani kama wanaofanya vitendo hivyo si watumishi wa Serikali walewale waliomtishia Nape bastola?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye hilo hilo; kuna mtu amepotea mwanachama wa CHADEMA kwa muda mrefu sasa, lakini gazeti linalomilikiwa na Mbunge wa CHADEMA limeandika mara mbili, moja nanukuu, kichwa cha habari *Mbowe ategwa*, gazeti linalomilikiwa na Mbunge wa CHADEMA, *article namba mbili gazeti hilo hilo Msaidizi wa Mbowe kuibuka*. Huyu Mbunge kwa nini anaachiwa mpaka leo kutokana na upotevu wa huyu Ben Saanane? kwa nini Serikali isimchukue na kumhoji? Atakuwa anajua vitu vingi kuhusiana na Ben Saanane. Nawashangaa Wabunge wa CHADEMA wanavyolalamika huku Bungeni suala la Ben Saanane kwa nini wasimuulize Kubenea?

MHE. SAED A. KUBNEA: Mheshimiwa Naibu Spika taarifa (*Kicheko*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Kubenea taarifa nimezikataa labda kama nikuhusu utaratibu, Mheshimiwa Mlinga malizia.

MHE. SAED A. KUBNEA: Mheshimiwa Naibu Spika nampa taarifa Mheshimiwa Mlinga kwamba...

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Kubenea sijakuruhusu kuzungumza; Waheshimwa Wabunge nimesema hivi nitaruhusu utaratibu kwa sababu ni uvunjifu wa Kanuni, taarifa kwa sasa sitaziruhusu.

Mheshimiwa Mlinga malizia mchango wako.

MHE. SAED A. KUBNEA: Mheshimiwa Naibu Spika nimetajwa kwenye Bunge, Mheshimiwa Naibu Spika tafadhali...

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa kuna watu wengi humu ndani wametajwa, huko nyuma nilishawaruhusu wengi hata

wa upande wako, uwe unaangalia sawasawa, mimi na wewe wote tunavaa miwani, uwe unaangalia sawasawa tafadhali. Mheshimiwa Mlinga naomba uendelee, Mheshimiwa Kubenea sijakuruhusu. (*Makof!*)

MHE. GOODLUCK A. MLINGA: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimalizie kwa kusema hivi; Waheshimiwa Wabunge tuwe tunaangalia vitu vya kutumia kabla hatujaingia humu Bungeni. Kuna Wabunge wameingia wamelewa.

MBUNGE FULANI: Wee ukimaliza ujie picha huku.

MHE. GOODLUCK A. MLINGA: Mheshimiwa Naibu Spika, nina ushahidi Mheshimiwa Nasari ameingia na Konyagi amezuiliwa hapo getini na mpaka saa hizi amelewa. Naomba tuangalie vitu vya kutumia kabla hatujaingia humu ndani.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. (*Makof!*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Dkt. Shukuru Kawambwa.

MHE. DKT. SHUKURU J. KAWAMBWA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa ya kuchangia hoja ya Mawaziri Ofisi ya Rais, TAMISEMI na Utumishi wa Umma na Utawala Bora.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote naomba nichukue fursa hii kuipongeza sana Serikali ya Awamu ya Tano kwa kazi nzuri ambayo inayofanya katika sekta mbalimbali. Pia nimpongeze sana Mheshimiwa Rais kwa uongozi mzuri na kuhakikisha kwamba Taifa letu linasonga mbele. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa kuchukua fursa hii kuchangia hoja katika suala la elimu. Kwanza katika Sekta ya Elimu niungane na Waheshimiwa Wabunge ambao wameipongeza Serikali kwa kutekeleza mpango wa elimu bila malipo. Huu ni uthubutu mkubwa ambao umehitaji

ujasiri kuweza kuutekeleza. Ni mpango ambao umewahusisha wananchi wetu wengi. Watoto wa kiume na wa kike wa Taifa letu hili jumla yao wanazidi milioni 10; milioni kama tisa katika shule za msingi na milioni mbili katika shule za sekondari, wote wakisoma bila ya malipo. Jambo hili limewafanya wanafunzi wa tabaka mbalimbali kuweza kushiriki katika elimu, lakini ni jambo ambalo limewapa imani na uhuru wananchi wetu wasio na uwezo wa kuwapeleka watoto wao katika shule na kuwafanya watoto wao waendelee na masomo yao ya msingi na sekondari.

Mheshimiwa Naibu Spika, hili jambo ni la ukombozi, elimu ni msingi wa maendeleo ya Taifa letu. Hatuwezi kufika mwaka 2025 kama Taifa la uchumi wa katil bila wananchi wetu kuwa wameelimika.

Mheshimiwa Naibu Spika, nia hii thabiti ya Serikali na juhudhi hii ya Serikali katika kuelimisha Taifa hili, tunaiona pia katika bajeti. Inatenga bajeti nzuri kwa Sekta ya Elimu ambayo inaendana na mahitaji katika shule zetu. Hata hivyo, tunajua kwamba changamoto katika shule zetu za msingi na sekondari ni kubwa mno, kwa hivyo bajeti hii ambayo tunaijadili hivi sasa tunaihitaji mno iweze kufika katika Halmashauri zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wangu ni katika wasilisho la bajeti ndani ya Halmashauri zetu. Katika Halmashauri ya Bagamoyo hili limekuwa changamoto moja kubwa sana na ili tufanikiwe katika elimu tafsiri ya bajeti lazima itekelezwe katika utekelezaji wa bajeti yenye ndani ya Halmashauri. Kwa mfano Halmashauri ya Wilaya ya Bagamoyo katika mwaka huu wa fedha 2016/2017 imetengewa pesa maalum kwa ajili ya ujenzi wa nyumba za Walimu, jumla ya Shilingi milioni 200 lakini hivi sasa tunaingia *quarter* ya nne bado hatujapokea .

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia tuna fedha za MMES kwa ajili ujenzi wa nyumba za Walimu na kwa ajili ya usambazaji wa umeme katika shule za sekondari, jumla ni

Sh. 466,000,000,000. Pesa hizo hivi tunavyoongea *quarter* ya nne bado hela hizi hazijaingia katika Halmashauri.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile fedha za *LGCD*, jumla Sh. 147,000,000 kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya shule. Fedha hizi Sh. 147,000,000 mpaka tunamaliza *quarter* tatu tumepata asilimia 49. Kwa ujumla bajeti ya miradi ya elimu kwa mwaka huu wa fedha kwa Halmashauri ya Bagamoyo jumla ya Sh. 814,000,000 tumepokea Sh. 72,000,000 ambayo ni chini ya asilimia 10.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa bila Serikali kusimamia utekelezaji wa bajeti katika Halmashauri zetu kwenye sekta ya elimu hatutoweza kufanikiwa katika elimu. Tutaizungumzia elimu na tutawapa matumaini wananchi wetu lakini mwisho wa siku pesa haikutoka hakuna kitu tutaweza kumudu. Sasa hivi tuna upungufu wa vyumba nya madarasa 291 katika Halmashauri yetu, ni fedha nyingi sana, lakini kama tungeweza kupata pesa hizi za mwaka huu wa fedha maana yake hatua kwa hatua tungeweza kuanza kupunguza shida hii ya vyumba nya madarasa na miundombinu mingine muhimu ya kuwezesha elimu bora iweze kupatikana kwa watoto wa kike na kiume wa nchi yetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Serikali yetu tutakapoingia katika bajeti hii ya mwaka 2017/2018, ihakikishe kwamba tunapomaliza mwezi wa Sita bajeti hii utekelezaji wake uwe kwa wakati na ukamilifu kufuatana na mafungu yale ambayo tumeyapanga. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa kuzungumzia kuhusu huduma ya afya. Hospitali ya Wilaya ya Bagamoyo ni hospitali ya zamani sana, tangu tumepata uhuru tulikuwa na hospitali hii. Miundombinu yake ni chakavu, tuna upungufu mwingi; tunahitaji wodi za kulala wanaume, wodi za kulala wanawake, chumba cha kujifungulia na vifaa nya tiba, tuna upungufu pia mkubwa wa dawa katika hospitali ya Bagamoyo. Hata hivyo, hospitali hii inatoa huduma kwa wananchi wengi, Halmashauri ya Wilaya nzima ya Bagamoyo

inaitegemea hospitali hii. Kwa maana kila mtu anapotoka kwenye zahanati, kata mbalimbali na vijiji mbalimbali tegemeo lake ni hospitali hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, Halmashauri yetu ya Bagamoyo haina uwezo wa kujengwa upya au kuikarabati au kuijengea miundombinu inayohitajika katika hospitali ili iweze kutoa huduma inayofanana na mahitaji ya wananchi wa Halmashauri ya Wilaya ya Bagamoyo. Naisihi Serikali, katika bajeti hii ihakikishe kwamba inatupa uwezo Halmashauri ya Bagamoyo ili tuweze kuipandisha kufikia ngazi au huduma ambao inafanana na mahitaji ya wananchi wa Wilaya hii ya Bagamoyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto ya miundombinu na upatikanaji wa madawa ipo pia katika zahanati zetu. Naishukuru Serikali kwa hatua ambazo imeweza kuzichukua katika mpango wa *RBF*, lakini naomba iongeze juhudini katika suala hili la afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuyasema hayo, nakushukuru sana na naunga mkono hoja. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Jesca Kishoa.

MHE. JESCA D. KISHOA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwanza kabla ya kuendelea nianze na *quotation* moja alittoa mtaalam mmoja wa masuala ya uongozi anaitwa *John Maxwell*, anasema hivi:-

"If you want to recognize the intelligence of the leader look people around him."

Mheshimiwa Naibu Spika, kama Mkuu wetu wa Nchi amezungukwa na watu aina ya Goodluck amezungukwa na watu aina ya Bashite *what do we expect.* (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sikutegemea kama tunaweza kuwa na aina ya viongozi ambao wanaweza kuja

humu ndani na kutoa maneno ya namna hii. Inasikitisha kutoa maneno ya kejeli kwa Kiongozi mkubwa wa Kambi Rasmi ya Upinzani. Waheshimiwa Wabunge wa CCM mnatidisappoint sana, tuko hapa kwa ajili ya kutetea maslahi ya wananchi hatupo hapa kwa ajili ya vijembe, hatupo hapa kwa ajili maneno ya umbea na unafiki. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niendelee kuchangia, nianze na.....

MHE. GOODLUCK A. MLINGA: Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Mlinga nimekataa taarifa, naruhusu kuhusu utaratibu kwa sababu inahusu uvunjifu wa kanuni, Mheshimiwa Jesca Kishoa.

MHE. JESCA D. KISHOA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Naomba niendelee katika suala zima la utawala bora baadaye nitamalizia na utumishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi yetu kwa sasa hivi imekumbwa na tatizo kubwa sana katika suala la uchumi na tatizo hili linatokana na ukosefu wa utawala bora katika Taifa letu. Leo hii nchi yetu tumekosa fedha za MCCtakriban Dola 463,000,000 kutoka Marekani kwa sababu ya ukosefu wa utawala bora. Leo hii tumekosa mikopo kutoka nje. Mheshimiwa shemeji yangu naona hayupo hapa leo, Mheshimiwa Waziri wa Fedha, amekwenda Ulaya, amezunguka nchi zote, amekosa mikopo kwa sababu kigezo namba moja cha mkopo ni lazima kuwe na *good governance* katika Taifa, lakin tunakosa fursa hizi kwa kutokuwepo na utawala bora. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mpaka leo Bajeti ya Mwaka 2016/2017, imetekelzeza kwa asilimia 34 tu kwa sababu kubwa ya ukosefu wa utawala bora. Wakati huo huo tunakosa misaada kutokana na ukosefu wa utawala bora katika Taifa hili. Wawekezaji wanakimbia, wafanyabiashara wanakimbia; kwa sababu hakuna mwekezaji ambaye ana

akili timamu anaweza kuwekeza kwenye nchi ambayo muda wowote mkataba unaweza ukavunjwa kwenye majukwaa. Hakuna mwekezaji ambaye anaweza kuwekeza kwenye nchi ambayo haifuati misingi ya utawala wa Sheria , hakuna. (*Makofi*)

MHE. CONSTANTINE J. KANYASU: Mheshimiwa Naibu Spika taarifa...

MBUNGE FULANI: Hakuna taarifa, we endelea, avumilie tu.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Kanyasu taarifa zimezuiliwa, muda wetu umekwisha.

MHE. JESCA D. KISHOA: Mheshimiwa Naibu Spika yapo mambo humu ndani tunaweza kutofautiana kwa sababu ya itikadi zetu, lakini yapo mambo ambayo lazima tuungane kwa ajili ya maslahi ya wananchi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, utawala wa sasa unaendeshwa kwa *double standard*, Serikali haina *consistency*. Kwa mfano unaweza kukuta kwamba watu ambao wako ngazi ya chini wanavunja Sheria na wanachukuliwa hatua kali, lakini wapo watu ambao wapo kwenye mamlaka kubwa wanavunja sheria na wakati mwingine wanalindwa mpaka na mitutu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi binafsi ni mdau mkubwa sana wa vita juu ya ufisadi, lakini jitihada za Mheshimiwa Rais wetu zinakosa uhalali kwa sababu ya kuwa na *double standard*. Kuna maeneo anaonekana anachukua hatua na kuna maeneo anaonekana hachukui hatua. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mukutano uliopita kuna suala nililzungumza humu ndani, nilizungumzia suala la uvunjaji wa Sheria ya *Finance Act* ambayo iliundwa mwaka

2012 section namba 29 inasema kwamba hakuna *transfer share* yoyote ambayo itafanyika bila kulipwa *Capital Gain Tax*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna kampuni inaitwa *Shell* ilifanya *transfer share* kutoka kampuni ya *BG*. *Shell* ilinunua vitalu vya gesi kutoka kampuni ya *BG*, lakini hakuna *Capital Gain Tax* ambayo imelipwa. Cha kusikitisha sana wakati tupo kwenye Kamati, Mkutano uliopita niliuliza viongozi wa *FCC* wakasema kwamba swali lako tutajibu kwa maandishi mpaka leo hawajajibu. Nika-take trouble kupitia Sheria ya Haki, Kinga na Madaraka ya Bunge, section namba 29 nikasema kwamba, toeni sababu kwa nini mpaka leo *Capital gain tax* haijalipwa lakini mpaka leo, toka tarehe nne *TRA* nao hawajajibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri Muhongo alijaribu kupiga bla bla, lakini nashukuru alikiri kwamba kuna wizi unafanyika kwenye makampuni haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii kampuni ya *Shell*, hii ni kampuni ambayo wiki mbili zilizopita, nina ushahidi hapa, imekuwa *reported* kwenye vyombo vyote duniani kwamba imetoa rushwa ya trillioni mbili kwa ajili ya kukidhi maslahi yake kwenye Serikali ya Nigeria. Baada ya kugundulika ndipo wakaamua kuitumbua.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa sisi kwenye Serikali yetu kampuni hii lazima tuone kwamba kuna harufu ya rushwa hapa. Haiwezekani fedha za wananchi takribani dola milioni 500, takribani kama trillioni moja na ushee, ni hela nyingi sana, zinaweza kutengeneza hiyo *standard gauge* ambayo Mheshimiwa Rais anataka kuitengeneza kutoka Dar es Salaam mpaka Morogoro; lakini imepotea katika mazingira hayo na hakuna ambaye amechukuliwa hatua na vitu vinafunikwa funikwa na hakuna ambaye anahoji. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kama kweli Mheshimiwa Rais wetu anataka tutengeneza imani na yeye, aanze kuchukua hatua ambazo zinalenga kote kote, achukue

hatua kwa watu wake, achukue hatua kwa watu ambao anafikiri kwamba hawamuhusu, wote kwa pande zote mbili achukue hatua kwa sababu mnatupotezea imani. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa haraka haraka naomba pia nichangie upande wa utumishi. Kuna uhusiano mkubwa sana kwenye suala la uwajibikaji na maslahi, hivi vitu viwili vinakwenda sambamba. Hapa nilipo nina chati kutoka Chuo cha Walimu, Kanda ya kati lakini nitaongelea *specifically* Singida. Walimu wa Mkoa wa Singida toka mwaka 2013 mpaka leo hawajapa stahiki zao, takribani bilioni 2.4.

Mheshimiwa Naibu Spika, hatuwezi kutegemea matokeo makubwa Singida na ndiyo maana elimu imekuwa ikianguka kila siku, tumegundua miongoni mwa sababu ni pamoja na hili. Naomba niishauri Serikali jambo moja; kama ambavyo wanafanya kwa wakandarasi, mkandarasi anapokuja kulipwa fidia zake, anapokuja kulipwa malipo yake analipwa kwa riba. Vivyo hivyo tupeleke utaratibu huu kwa upande wa watumishi wa Serikali, *specifically* Walimu pale mnapokuja kuwalipa muwalipe kwa riba kwa sababu fedha zile kwa wakati ule *value* yake ni tofauti na wakati huu. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sana Mheshimiwa Waziri atutazame upya kwa sababu inasikitisha sana elimu yetu imekuwa ikisuasua kwa muda mrefu sana na Walimu wamekuwa wakilalamika sana, wanaishi maisha magumu, wanakosa stahiki zao. Moja kwa moja hiyo *automatically* inapelekea utendaji mbovu kwenye elimu wanayoitoa kwa wanafunzi wetu. Tutaendelea kuzalisha watoto ambao hawana vigezo, hawana sifa, kwa sababu tunashindwa kuwasaidia Walimu kupata stahiki zao (*makof*)

(*Hapa kengele ililia kuashiria kwisha
kwa muda wa mzungumzaji*)

NAIBU SPIKA: Ahsante Mheshimiwa Kishoa muda wako umekwisha.

NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI, TEKNOLOJIA NA UFUNDI: Mwongozo wa Spika.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Stella Manyanya, kwanza nianze na hili, muda wetu wa kuchangia umekwisha lakini nimeletemwa hapa maandishi, ama niseme malalamiko na Kambi ya *CUF* ikitembe kwamba wachangiaji walikuwa wachangie wanne sasa wamekuwa wawili.

Waheshimiwa Wabunge taarifa, utaratibu na miongozo imekuwa mingi na Kambi pekee iliyochangia kwa kupitiliza humu ndani ni upande wa CHADEMA ambao amebakishwa mtu mmoja, watu watano wamechangia, *CUF* bado wawili, CCM bado watu kama saba hivi ama nane kufikia ule uwiano. Kwa hiyo, si kwamba *CUF* pekee ndio ambao hawajafikia uwiano, CHADEMA bado Mbunge mmoja.

Baada ya kusema hayo niwasomee majina ya wale ambao walipaswa kukamilisha ule uwiano wa Wabunge wanaopaswa kuchangia, ambao sasa wataanza kuchangia kesho na watu wa meza hapo muyapate haya majina. Mheshimiwa Masoud unaonekana bado una jambo.

Kwa upande wa CCM yupo Mheshimiwa Hassan Masala, Mheshimiwa Aysharose Mattembe, Mheshimiwa Flatei Massay, Mheshimiwa Jacqueline Msongozi, Mheshimiwa Hasna Mwilima, Mheshimiwa Dotto Biteko, Mheshimiwa Subira Mgali, Mheshimiwa Japhet Hasunga, Mheshimiwa Omary Mgumba, Mheshimiwa Boniventure Kiswaga, Mheshimiwa Omari Kigua na Mheshimiwa Livingstone Lusinde.

Upande wa CHADEMA ni Mheshimiwa Paschal Yohana Haonga, kwa upande wa Chama cha wananchi *CUF* ni Mheshimiwa Khalifa Mohamed Issa na Mheshimiwa Salma Mwasa.

Sasa kwa upande wa *CUF* kwa changamoto zilizopo kwa siku ya kesho atachangia pia Mheshimiwa Maftaha Nachuma.

*(Hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge
waliongea bila mpangilio)*

Waheshimiwa Wabunge tusiende huko hatuwezi kuwa tunarudia hadithi moja kila siku, kwa sababu haiwezekani michango yote mpaka mtu aombe hapa mbele wakati ninyi ni chama kimoja. Mngekubaliana huko mlete majina, kila siku mnakata majina ndiyo changamoto yenye.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, naahirisha shughuli za Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi.

(Saa 1.45 usiku Bunge lilahirishwa Mpaka Siku ya Alhamisi, Tarehe 20 Aprili, 2017, Saa Tatu Asubuhi)